# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

# MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2021/22

**FEBRUARI, 2021**

# YALIYOMO

SURA YA KWANZA....1
UTANGULIZI....1
1.1 Umuhimu wa Mapendekezo ya Mpango....1
1.2 Miongozo Iliyozingatiwa Katika Maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango....2
1.3 Ushirikishwaji wa Wadau....2
1.4 Mpangilio wa Kitabu....3

SURA YA PILI....4
HALI YA UCHUMI....4
2.1. Utangulizi....4
2.2. Mapitio ya Hali ya Uchumi....4
2.2.1. Ukuaji wa Uchumi wa Dunia....4
2.2.1.1. Uchumi wa Nchi Zilizoendelea....4
2.2.1.2. Uchumi wa Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea....5
2.2.2. Uchumi wa Nchi Kusini mwa Jangwa la Sahara....5
2.2.3. Mapitio ya Hali ya Uchumi....5
2.2.3.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi....5
2.2.3.2 Mfumuko wa Bei Nchini....6
2.2.3.3 Sekta ya Nje....7
2.2.3.4 Deni la Serikali....8
2.2.3.5 Sekta ya Fedha....9
2.2.3.6 Mwenendo wa Masoko ya Mitaji....11
2.3 Maendeleo ya Watu....12
2.3.1 Ongezeko la Idadi ya Watu....12
2.3.2 Viashiria vya Maendeleo ya Watu....12
2.3.2.1 Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini....13
2.3.2.2 Upatikanaji wa Chakula....14

SURA YA TATU....15
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO....15
3.1 Utangulizi....15
3.2 Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 na Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2020/21....15
3.2.1 Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2019/20....15
3.2.2 Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2020/21....15
3.3 Hatua za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo....16
3.3.1 Miradi ya Kielelezo....16

3.3.2 Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda ....... 20
3.3.3 Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu ....... 33
3.3.4 Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji ....... 55
3.3.5 Kuimarisha Usimamizi na Utekelezaji wa Mpango ....... 72

SURA YA NNE ....... 74
MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2021/22 ....... 74
4.1 Utangulizi ....... 74
4.2 Misingi ya Mpango na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi ....... 74
4.2.1 Misingi *(Assumptions)* ya Mpango kwa Mwaka 2021/22 ....... 74
4.2.2 Shabaha za Ukuaji wa Uchumi ....... 74
4.3 Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka 2021/22 ....... 75
4.3.1 Miradi ya Kielelezo ....... 75
4.3.2 Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi ....... 76
4.3.2.1 Kuimarisha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji ....... 76
4.3.2.2 Biashara na Masoko ....... 79
4.3.2.3 Mapinduzi ya TEHAMA ....... 80
4.3.3 Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma ....... 80
4.3.3.1 Uzalishaji Viwandani ....... 80
4.3.3.2 Uongezaji Thamani ....... 81
4.3.3.3 Huduma ....... 83
4.3.4 Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji ....... 84
4.3.5 Kuchochea Maendeleo ya Watu ....... 84
4.3.5.1 Afya, Ustawi na Maendeleo ya Jamii ....... 84
4.3.5.2 Elimu ....... 85
4.3.5.3 Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ....... 86
4.3.5.4 Huduma za Maji Safi na Maji Taka ....... 86
4.3.5.5 Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi ....... 86
4.3.5.6 Kinga ya Jamii ....... 87
4.3.5.7 Usalama wa Chakula na Lishe ....... 87
4.3.6 Kuendeleza Rasilimali Watu ....... 87
4.3.7 Maeneo Mengine Yatakayopewa Kipaumbele ....... 88
4.3.7.1 Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ....... 88
4.3.7.2 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa ....... 88
4.3.7.3 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ....... 89
4.3.7.4 Uzalendo na Ushiriki wa Jamii katika Maendeleo ....... 89

SURA YA TANO ....... 90

UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2021/22 ................90
5.1 Utangulizi ........................................................................................90
5.2 Gharama za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2021/22 ..........90
5.3 Vyanzo vya Mapato kwa Mwaka 2021/22 ..........................................91
5.4 Vyanzo Vingine vya Mapato ................................................................92

SURA YA SITA ..........................................................................................93
UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA ..................................93
6.1 Utangulizi ........................................................................................93
6.2 Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17– 2020/21 ..........................................................93
6.3 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 ..........................................................................94
6.4 Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini ......................................................94
6.5 Mgawanyo wa Majukumu ....................................................................94
6.5.1 Wizara ya Fedha na Mipango ............................................................94
6.5.2 Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali ...........................95
6.5.3 Ofisi ya Rais – TAMISEMI ................................................................95
6.5.4 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ...95
6.5.5 Sekta Binafsi ..................................................................................96

Kiambatisho I: Ratiba ya Maandalizi ya Mpango 2021/22 ...........................97

Kiambatisho II: Mradi Iliyofuatiliwa katika Mwaka 2019/20.........................100

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Umuhimu wa Mapendekezo ya Mpango

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 ni ya kwanza katika hatua za utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 wenye dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Aidha, Mapendekezo haya yameandaliwa ikiwa ni kukidhi matakwa ya Ibara ya 63 (3) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni ya 113 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la Juni 2020. Mpango wa Tatu utajumuisha maeneo ya utekelezaji pamoja na miradi ambayo haikukamilika katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21. Vile vile, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 utakuwa ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo ina lengo la kufanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati na hali bora ya maisha ifikapo mwaka 2025. Hivyo, mapendekezo haya yanajenga msingi wa maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22.

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 yatajikita katika maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu ambayo ni:

(i) **Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi.** Eneo hili linajumuisha miradi ambayo itajikita katika: kujenga jamii yenye uwezo wa kushindana kikanda na kimataifa; kuimarisha utulivu wa uchumi jumla; kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuimarisha uvumbuzi na uhawilishaji wa teknolojia kutoka nje; na kuendeleza miundombinu na huduma katika maeneo ya reli, barabara, madaraja, usafiri wa majini, usafiri wa anga, TEHAMA, nishati, bandari na viwanja vya ndege.

(ii) **Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma**: Eneo hili linajumuisha miradi ya viwanda inayolenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na madini pamoja na kuzalisha bidhaa zitakazotumia malighafi na rasilimali zinazopatikana kwa wingi nchini. Aidha, eneo hili linajumuisha miradi na programu zinazolenga kuboresha sekta ya utalii, huduma za fedha na bima.

(iii) **Kukuza Biashara na Uwekezaji:** Eneo hili linajumuisha programu zitakazoimarisha masoko ya ndani na kutumia fursa za masoko kikanda na kimataifa. Aidha, masoko yanayolengwa ni yale yatakayotoa fursa kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini ikiwemo bidhaa na huduma

zitokanazo na kilimo, viwanda na utalii.

(iv) **Kuchochea Maendeleo ya Watu:** Eneo hili linajumuisha utekelezaji wa miradi ambayo inajikita katika kuboresha maisha ya watu ikiwemo kuboresha elimu na mafunzo katika ngazi zote; afya na ustawi wa jamii; kinga ya jamii; huduma za maji na usafi wa mazingira; mipango miji, nyumba na maendeleo ya makazi. Aidha, eneo hili linajumuisha kuimarisha juhudi za uzingatiaji wa sheria, mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi ikiwemo kuimarisha utoaji haki pamoja na ukuzaji wa maadili.

(v) **Kuendeleza Rasilimali Watu:** Eneo hili linajumuisha programu na mikakati inayolenga kuendeleza ujuzi wa rasimali watu nchini, kuanzia ngazi za elimu ya awali hadi elimu ya juu ikiwemo kuwawezesha vijana kujiajiri. Vile vile, eneo hili linajumuisha hatua za kuboresha viwango vya utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na ujuzi adimu kwa lengo la kuongeza tija na ushindani wa wananchi katika kutumia rasimali zilizopo nchini ili kuleta maendeleo.

## 1.2 Miongozo Iliyozingatiwa Katika Maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 yamezingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Sera na Mikakati mbalimbali ya kisekta, kikanda na kimataifa zikiwemo Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika 2050; Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 unalenga kuwezesha nchi kutumia kikamilifu fursa zilizopo kwa kuuza zaidi bidhaa za viwandani na huduma nje ya nchi na kuboresha maisha ya watu. Mpango huu umejengwa katika misingi ya mipango ya awali iliyolenga kuimarisha na kukuza uchumi wa kisasa, fungamanishi, jumuishi na shindani ambao unahimili utandawazi. Aidha, Mpango utazingatia mipango iliyojengwa katika msingi wa huduma za kiuchumi, viwanda na miundombinu wezeshi. Vile vile, Mpango unaendeleza utekelezaji wa malengo mengine ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, hususan utawala bora, amani, utulivu, umoja na kujenga jamii iliyoelimika na yenye utamaduni wa kujifunza.

## 1.3 Ushirikishwaji wa Wadau

Maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 yameshirikisha wadau mbalimbali ikijumuisha Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi. Aidha, Washirika wa

Maendeleo wameshirikishwa kupitia majadiliano katika maeneo ya ushirikiano, ufadhili wa miradi mahsusi na misaada ya kisekta.

### 1.4 Mpangilio wa Kitabu

Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango kimegawanyika katika sura sita (6): Sura ya kwanza ni utangulizi; Sura ya pili inaainisha mapitio ya hali ya uchumi; Sura ya tatu inaelezea mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2019/20 na nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21; Sura ya nne inaelezea maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2021/22; Sura ya tano inaelezea ugharamiaji wa Mpango; na Sura ya sita inaainisha mfumo na utaratibu wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa za utekelezaji wa Mpango.

# SURA YA PILI

# HALI YA UCHUMI

## 2.1. Utangulizi

Sura hii inaelezea kwa muhtasari mwenendo wa viashiria mbalimbali vya hali ya uchumi na maendeleo ya watu katika mwaka 2019 na maoteo kwa mwaka 2020. Mwenendo wa viashiria hivi ndiyo msingi wa malengo ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22. Baadhi ya viashiria hivyo ni pamoja na Pato la Taifa; Pato la wastani la kila mtu; mfumuko wa bei; mwenendo wa sekta ya nje; sekta ya fedha; deni la Serikali; idadi ya watu; na hali ya umaskini nchini.

## 2.2. Mapitio ya Hali ya Uchumi

### 2.2.1. Ukuaji wa Uchumi wa Dunia

Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Januari 2021 inaonesha kuwa, katika mwaka 2019, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 2.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.5 mwaka 2018. Kasi ndogo ya ukuaji kwa mwaka 2019 ilichangiwa na kuendelea kwa mgogoro wa kibiashara kati ya China na Marekani, vuguvugu la Uingereza kujitoa kwenye Umoja wa Ulaya, kuongezeka kwa machafuko ya kijamii katika baadhi ya nchi zikiwemo Argentina, Iran, Uturuki, Venezuela, Libya na Yemen pamoja na majanga yanayohusiana na hali ya hewa kama vile Kimbunga Humberto katika eneo la Caribbean, ukame na kuungua kwa misitu nchini Australia, mafuriko katika maeneo ya mashariki mwa Afrika na ukame maeneo ya kusini mwa Afrika.

Mwaka 2020, uchumi wa dunia unatarajiwa kuwa na ukuaji hasi wa asilimia 3.5 na kuimarika kufikia ukuaji wa asilimia 5.5 mwaka 2021. Hii inatokana na hatua za kufufua chumi mbalimbali dunia hususan mataifa yaliyoendelea zinazochukuliwa ikijumuisha upatikanaji na usambazaji wa chanjo ya COVID-19 kwa mataifa mbalimbali.

#### 2.2.1.1. Uchumi wa Nchi Zilizoendelea

Uchumi kwa nchi zilizoendelea ulikua kwa wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.2 mwaka 2018. Mwaka 2020 uchumi unatarajiwa kuwa na ukuaji hasi wa asilimia 4.9 na kuimarika kufikia asilimia 4.3 mwaka 2021.

#### 2.2.1.2. Uchumi wa Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea

Uchumi wa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.5 mwaka 2018. Hii inatokana na kuongezeka kwa masharti ya China kwenye usimamizi wa masuala ya fedha, wasiwasi wa vita ya kibiashara kati ya China na Marekani, kushuka kwa uwekezaji binafsi nchini Mexico, ukuaji hafifu wa uzalishaji wa mafuta na migogoro ya kisiasa hususan katika nchi za Mashariki ya Kati. Mwaka 2020 matarajio ni kupungua kwa ukuaji kufikia ukuaji hasi wa asilimia 2.4 na kuimarika kufikia ukuaji wa asilimia 6.3 mwaka 2021. Hii inatokana na matarajio ya kuendelea kusambazwa kwa chanjo ya COVID-19 kwa nchi mbalimbali na hatua za kuinua chumi husika.

### 2.2.2. Uchumi wa Nchi Kusini mwa Jangwa la Sahara

Uchumi wa Nchi Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikua kwa wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.3 mwaka 2018. Kushuka kwa ukuaji wa uchumi kumetokana na kupungua kwa shughuli za kibiashara baina ya nchi washirika, mafuriko maeneo ya Mashariki mwa Afrika na ukame maeneo ya Kusini mwa Afrika. Matarajio ni kuendelea kupungua kwa ukuaji kufikia ukuaji hasi wa asilimia 2.6 mwaka 2020 kutatokana na athari za COVID-19 na kushuka kwa uhitaji wa mafuta. Aidha, mwaka 2021 uchumi unatarajiwa kuimarika hadi ukuaji wa asilimia 3.2 kutokana na hatua mbalimbali zitakazochukuliwa kuimarisha ukuaji katika nchi zenye utajiri mkubwa wa rasilimali pamoja na matarajio ya kuimarika kwa bei za mafuta ghafi katika soko la dunia. **Jedwali Na. 2.1** linaonesha mwenendo wa ukuaji wa pato halisi la dunia.

**Jedwali 2.1: Ukuaji wa Pato halisi la Dunia 2016 - 2019, na Matarajio 2020 – 2021**

| Kundi/Mwaka | Ukuaji Halisi (asilimia) | | | | Matarajio (asilimia) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 |
| Dunia | 3.2 | 3.8 | 3.5 | 2.8 | -3.5 | 5.5 |
| Nchi Zilizoendelea | 1.7 | 2.4 | 2.2 | 1.6 | -4.9 | 4.3 |
| Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea | 4.3 | 4.8 | 4.5 | 3.6 | -2.4 | 6.3 |
| Nchi Zinazoibukia Barani Asia | 6.4 | 6.6 | 6.3 | 5.5 | -1.7 | 8.0 |
| Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara | 1.3 | 2.9 | 3.3 | 3.2 | -2.6 | 3.2 |

***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Januari 2021*

### 2.2.3. Mapitio ya Hali ya Uchumi

#### 2.2.3.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi

Ukuaji wa Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.0 mwaka 2019 kama ilivyokuwa mwaka

2018. Ukuaji huu ulitokana na kuendelea kuimarika kwa sekta ya madini, kuboreshwa kwa huduma za usafiri na usafirishaji pamoja na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa barabara, reli, viwanja vya ndege, miradi ya nishati ya umeme pamoja na ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya. Shughuli za kiuchumi zilizokuwa na ukuaji mkubwa katika kipindi cha mwaka 2019 ni: madini (asilimia 17.7); ujenzi (asilimia 14.8); sanaa na burudani (asilimia 11.2); na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (asilimia 8.7). Shughuli za uchumi zilizokuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa ni pamoja na: kilimo (asilimia 26.6), ujenzi (asilimia 14.3), biashara na matengenezo (asilimia 8.8) na uzalishaji viwandani (asilimia 8.5).

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Septemba 2020, uchumi ulikua kwa asilimia 4.7. Sekta zilizokua kwa kasi zaidi ni pamoja na ujenzi (asilimia 13.6) uchimbaji madini (asilimia 9.9); habari na mawasiliano (asilimia 9.0); uchukuzi na uhifadhi wa mizigo (asilimia 8.9); na shughuli za kiufundi, kitaalam, na kisayansi (asilimia 8.8).


Kutokana na ukuaji imara wa uchumi kwa zaidi ya wastani wa asilimia 6 katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, mwezi Julai 2020 Benki ya Dunia iliitangaza Tanzania kuwa miongoni mwa nchi za kipato cha kati cha chini. Hatua hii ilitokana na kuongezeka kwa pato la mtu (GNI) kutoka shilingi 2,452,406 (sawa na dola za Marekani 1,020) mwaka 2018 hadi shilingi 2,577,967 (sawa na dola za Marekani 1,080) mwaka 2019, kiasi hicho ni juu ya kiasi kilichowekwa cha dola za Marekani 1,036 ili nchi iweze kufikia hadhi ya kipato cha kati cha chini (*lower-middle income status*).

#### 2.2.3.2 Mfumuko wa Bei Nchini

**(a) Mfumuko wa Bei Nchini**

Katika kipindi cha mwaka unaoishia Desemba 2020 mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 3.4 kwa mwaka ulioishia Desemba 2019. Mwenendo wa mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu kutokana na usimamizi thabiti wa Sera ya Fedha na Bajeti, kuimarika kwa ugavi wa chakula nchini, upatikanaji wa nishati ya umeme wa uhakika na kupungua kwa bei ya mafuta katika soko la dunia. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei za vyakula ulipungua kutoka wastani wa asilimia 6.9 kufikia wastani wa asilimia 4.0. Aidha, mfumuko wa bei za nishati uliongezeka kutoka wastani wa asilimia 2.8 hadi asilimia 8.0.

**Kielelezo Na. 2.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei (Januari 2018 – Desemba 2020)**




***Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2021*

**(b) Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki**

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2020, wastani wa mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Mashariki ulifikia asilimia 5.9. Katika kipindi hicho, Tanzania ilikuwa na wastani mdogo zaidi wa asilimia 3.3 wakati Rwanda ikiwa na mfumuko mkubwa zaidi wa asilimia 9.9. **Jedwali Na. 2.2** linaonesha mwenendo wa mfumuko wa bei kwa nchi za Ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Jedwali Na. 2.2: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki (Januari - Desemba 2020)**

| **Nchi/Mwezi** | Januari | Februari | Machi | Aprili | Mei | Juni | Julai | Agosti | Septemba | Oktoba | Novemba | Desemba | Wastani |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tanzania | 3.7 | 3.7 | 3.4 | 3.3 | 3.2 | 3.2 | 3.3 | 3.3 | 3.1 | 3.1 | 3.0 | 3.2 | 3.3 |
| Kenya | 5.8 | 6.4 | 5.5 | 5.6 | 5.5 | 4.6 | 4.4 | 4.4 | 4.2 | 4.84 | 5.46 | 5.62 | 5.2 |
| Uganda | 3.4 | 3.4 | 3 | 3.2 | 2.8 | 4.1 | 4.7 | 4.6 | 4.5 | 4.5 | 3.7 | 3.7 | 3.8 |
| Rwanda | 11.5 | 13.5 | 13.1 | 10.1 | 9.9 | 10.3 | 11.5 | 10.9 | 10.8 | 9.3 | 4.5 | 3.9 | 9.9 |
| Burundi | 5.2 | 7.6 | 7.1 | 7.6 | 9.2 | 8.5 | 7.7 | 6.4 | 6.3 | 7.0 | 9.0 | _ | 7.4 |

***Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Taarifa za Nchi Husika*

**2.2.3.3 Sekta ya Nje**

**(a) Urari wa Malipo ya Kawaida**

Mwaka 2020, urari wa malipo ya kawaida uliimarika kufikia nakisi ya dola za Marekani milioni 661.9 kutoka nakisi ya dola za Marekani milioni 1,292.6 mwaka 2019. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na kupungua kwa uagizaji

wa bidhaa kutoka nje. Katika kipindi hicho, urari wa jumla wa malipo ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 764.8 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 587.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Hii ilichangiwa na uingiaji mdogo wa fedha kutoka nje.

Mwaka 2020, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilifikia dola za Marekani milioni 8,809.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 9,658.6 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, thamani ya mauzo ya bidhaa asilia ilikuwa dola za Marekani milioni 819.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 834.6 mwaka 2019. Thamani ya bidhaa zisizo asilia zilizouzwa nje iliongezeka kwa dola za Marekani milioni 1,124.8 kufikia dola za Marekani milioni 5,294.0 mwaka 2020 kutoka dola za Marekani milioni 4,169.2 mwaka 2019. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji kwenye kilimo cha maua na mbogamboga, bidhaa za viwandani na madini yote isipokuwa almasi. Katika kipindi husika, mauzo ya dhahabu nje yaliongezeka kwa asilimia 33.5 kufikia dola za Marekani milioni 2,957.5 kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji pamoja na bei.

Katika kipindi cha mwaka 2020, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ilifikia dola za Marekani milioni 8,908.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 10,361.7 mwaka 2019. Kushuka kwa uagizaji wa bidhaa na huduma nje kulitokana na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa za kukuza mtaji na bidhaa za matumizi ya kati. Aidha, katika kipindi husika thamani ya uagizaji wa mafuta ilishuka kwa asilimia 30.4 kufikia dola za Marekani milioni 1,253.3 ikichangiwa na kushuka kwa bei na kiasi cha bidhaa zilizoagizwa. Vile vile, thamani ya uagizaji wa mashine na mitambo ya usafirishaji ilipungua kwa asilimia 29.6 kufikia dola za Marekani milioni 748.8.

**(b) Akiba ya Fedha za Kigeni**

Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kutosha kuweza kukidhi mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi. Hadi Desemba 2020, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani bilioni 4.8. Kiasi hiki kinatosheleza mahitaji ya fedha za kigeni za kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 5.6. Kiasi hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya kutosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa muda wa miezi 4.0 na pia ni juu ya lengo la miezi 4.5 lililowekwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**2.2.3.4 Deni la Serikali**

Hadi Desemba 2020, deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 59,009.8. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi bilioni 16,179.6 na la nje ni shilingi bilioni 42,830.2.

Mikopo hii imetumika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo: ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli na viwanja vya ndege; na utekelezaji wa miradi ya maji. Aidha, Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Novemba, 2020 imeonesha kuwa deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu kwa kuzingatia ukomo unaokubalika kimataifa kwa viashiria vyote muhimu. Katika tathmini hiyo viashiria vinaonesha kuwa thamani halisi ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 27.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 70; thamani halisi ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 17.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; na thamani halisi ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 113.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 240. Aidha, ulipaji wa deni la nje kwa mauzo ya bidhaa nje ni asilimia 13.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 23. Kwa kuzingatia vigezo hivyo, Tanzania bado ina uwezo wa kuendelea kugharamia shughuli zake za maendeleo na kulipa mikopo ya nje na ndani inayoiva kwa kutumia mapato yake kwa wakati.

**2.2.3.5 Sekta ya Fedha**

**(a) Ujazi wa Fedha na Karadha**

Katika kipindi cha mwaka unaoishia Desemba 2020, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 5.7. Aidha, katika kipindi hicho ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa wastani wa asilimia 8.2. Ukuaji huu ulichangiwa na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi katika uchumi.

**(b) Mwenendo wa Mikopo**

Kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kuongezeka na kufikia asilimia 3.0 katika kipindi cha mwaka unaoishia Desemba 2020. Ukuaji huu ulichangiwa na kuendelea kuimarika kwa uzalishaji katika uchumi pamoja na utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara nchini.

Sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi iliendelea kuelekezwa katika shughuli binafsi ambazo zilipata asilimia 34.3 ya mikopo yote ikifuatiwa na shughuli za biashara (asilimia 15.4), uzalishaji viwandani (asilimia 9.5) na usafirishaji na mawasiliano (asilimia 8.7).

**(c) Mwenendo wa Viwango vya Riba**


Hadi Desemba 2020, wastani wa riba za mikopo ya benki kwa ujumla umepungua na kufikia asilimia 16.74 ikilinganishwa na asilimia 16.76 Desemba 2019. Vile vile, riba za mikopo ya kipindi cha mwaka mmoja zimepungua na kufikia wastani wa asilimia 15.72 Desemba 2020 kutoka asilimia 16.28 Desemba 2019. Aidha, wastani wa

riba za amana kwa ujumla uliongezeka kufikia asilimia 7.09 Desemba 2020, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.79 Desemba 2019. Riba za amana za kipindi cha mwaka mmoja zilipungua na kufikia asilimia 8.41 Desemba 2020 kutoka asilimia 8.90 Desemba 2019. Hivyo, tofauti kati ya riba za mikopo na za amana kwa mwaka mmoja ilipungua kufikia nukta za asilimia 7.31 Desemba 2020 kutoka nukta za asilimia 7.38 Desemba 2019. Hii inaashiria kuendelea kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji na ustawi wa sekta binafsi nchini.

**(d) Mwenendo wa Thamani ya Shilingi**

Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani imeendelea kuwa tulivu kutokana na hatua mbalimbali za Sera za Fedha na Bajeti zilizochukuliwa na Serikali, kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nje ya nchi pamoja na mwenendo mzuri wa shughuli mbalimbali za kiuchumi. Aidha, hatua zilizotekelezwa na Benki Kuu ya Tanzania katika kuhakikisha uwazi na utaratibu mzuri wa ununuzi na uuzaji wa fedha za kigeni nchini, zimeendelea kuchangia utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya sarafu nyingine kubwa duniani. Dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,309.83 Desemba 2020 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,300.58 Desemba 2019.

**Kielelezo Na. 2.2: Mwenendo wa Thamani ya Shilingi Dhidi ya Dola ya Marekani (Wastani wa Mwezi Husika)**




*Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania*

#### 2.2.3.6 Mwenendo wa Masoko ya Mitaji

Mauzo katika Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka kufikia shilingi bilioni 184.9 katika kipindi cha mwaka kilichoishia Oktoba 2020. Aidha, mtaji wa Soko la Hisa kwa kampuni za ndani yaani *Domestic Market Capitalisation* katika kipindi kilichoishia Oktoba 2020 uliongezeka kwa asilimia 1.1 na kufikia Shilingi trilioni 9.11 kutoka Shilingi trilioni 9.01 katika kipindi kilichoishia Oktoba 2019. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa bei ya hisa ya baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa.

**Soko la Upili la Hatifungani za Serikali**

**(a) Hatifungani za Serikali**

Kwa upande wa hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam, mauzo yaliongezeka kwa asilimia 110.93 na kufikia shilingi trilioni 2.02 katika kipindi kilichoishia Oktoba 2020, ikilinganishwa na mauzo ya shilingi bilioni 958.88 yaliyorekodiwa katika kipindi kilichoishia Oktoba 2019. Kuongezeka kwa mauzo ya hatifungani za Serikali kumetokana na jitihada za Serikali kuendeleza soko la upili pamoja na wawekezaji kuhamisha uwekezaji wao kutoka kwenye uwekezaji ambao unaonekana unaweza kupata athari za kiuchumi (perceived risk) kwenda kwenye uwekezaji unaoonekana kuwa salama zaidi yaani *risk free* ambao ni hatifungani za Serikali.

**(b) Hatifungani za Kampuni**

Mauzo ya hatifungani za kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka kwa asilimia 116.94 na kufikia shilingi bilioni 1.32 katika kipindi kilichoishia Oktoba 2020, ikilinganishwa na mauzo ya shilingi milioni 608.76 yaliyorekodiwa katika kipindi kilichoishia Oktoba 2019. Kuongezeka kwa mauzo ya hatifungani za Kampuni kumetokana na kuimarika kwa biashara katika soko la Hatifungani.

**(c) Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja**

Mwenendo wa uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (Collective Investment Schemes) katika kipindi kilichoishia Desemba 2020 ulikuwa wa kuridhisha. Kwa ujumla thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja katika kipindi hicho iliongezeka kwa asilimia 44 kutoka shilingi bilioni 329.64 Desemba 2019 hadi shilingi bilioni 476.98 Desemba 2020.

## 2.3 Maendeleo ya Watu

### 2.3.1 Ongezeko la Idadi ya Watu

Idadi ya watu nchini imeendelea kuongezeka kwa wastani wa asilimia 3.1 kwa miaka miwili mfululizo yaani mwaka 2019 na mwaka 2020. Makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 2020 yanaonesha kuwa idadi ya watu imeongezeka kutoka watu 54,265,158 mwaka 2019 hadi watu 55,966,030 mwaka 2020. Kati ya watu hao, wanawake ni 28,550,590 sawa na asilimia 51.0 na wanaume ni 27,415,440 sawa na asilimia 49.0.

Makadirio hayo yanaonesha kuwa watoto wenye umri kati ya miaka 0-14 wamefikia 24,284,055 sawa na asilimia 43.4. Vile vile, nguvu kazi ya Taifa inayojumuisha watu wenye umri wa miaka 15-64 ni jumla ya watu 30,021,683 ambao ni sawa na asilimia 53.6 ya idadi ya watu wote. Ongezeko hili ni mtaji mkubwa kwa nchi katika shughuli mbalimbali za uzalishaji katika sekta zote za huduma na uzalishaji. Umri wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 62 (2015/16) hadi miaka 66 (2019/20) na unakadiriwa kuwa miaka 66.6 mwaka 2021. Serikali imeendelea kuweka mikakati na sera madhubuti za kuboresha huduma za kijamii kuendana na mahitaji ya ongezeko la watu.

### 2.3.2 Viashiria vya Maendeleo ya Watu

Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kupunguza umaskini ikijumuisha: utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi kwa kuongeza ujenzi wa Zahanati na vituo vya afya, ujenzi wa hospitali za halmashauri na watalaamu wa afya na dawa na vifaa tiba; utoaji wa elimu msingi bila ada; utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi; kutolewa kwa huduma ya maji kwa wananchi; na usambazaji wa umeme mijini na vijijini.

Hatua hizo zimewezesha kuongezeka kwa kipato cha wastani cha mtu (GNI per-Capita) na kuchangia kupungua kwa umaskini. Mathalani, **Umaskini wa Mahitaji Muhimu** umepungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 26.4 mwaka 2017/18 sawa na wastani wa asilimia 6.7 katika kipindi husika (wastani wa asilimia 1.3 kwa mwaka). Aidha, **Umaskini wa Chakula** umepungua kutoka asilimia 9.7 mwaka 2011/12 hadi asilimia 8.0 mwaka 2017/18 sawa na asilimia 17.5 katika kipindi husika (wastani wa asilimia 3.8 kwa mwaka).

Matokeo yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo yamewezesha mabadiliko chanya katika viashiria vya maendeleo ya watu ikiwa ni pamoja na:

(i) Kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 62 (2015/16) hadi miaka 66 (2019/20), idadi ya watanzania wenye bima ya afya kutoka asilimia 27 (2016/17) hadi asilimia 34 (2018/19) na kupungua kwa idadi ya vifo vya akina mama wakati wa kujifungua kutoka 432 (2015/16) hadi 321 (2018/19) kwa kila vizazi hai 100,000;
(ii) Vifo vya Watoto chini ya miaka mitano vimepungua kutoka vifo 67 (2015/16) hadi 50 (2019/20) kwa vizazi hai 1,000;
(iii) Hali ya upatikanaji wa maji vijijini imeongezeka kutoka asilimia 47 mwaka 2015 hadi asilimia 70.1 mwaka 2020 na mijini imeongezeka kutoka asilimia 74 mwaka 2015 hadi asilimia 84 mwaka 2020;
(iv) Kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya msingi kutoka asilimia 93.3 mwaka 2015 hadi asilimia 110.6 mwaka 2020;
(v) Hali ya upatikanaji wa umeme imeongezeka kwa asilimia 16 katika kipindi cha 2016/17 - 2019/20, ongezeko kubwa likiwa maeneo ya vijijini (asilimia 41.6) ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 2.4 maeneo ya mijini;
(vi) Idadi ya vijiji vilivyounganishwa na umeme vimeongezeka kutoka 2,018 mwaka 2015 kufikia 10,018 Desemba 2020; na
(vii) Idadi ya kaya zilizounganishwa na umeme imeongezeka kwa asilimia 14.9 huku ongezeko kubwa likiwa maeneo ya vijijini (asilimia 45) ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 12.1 maeneo ya mijini.

**2.3.2.1 Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini**

Idadi ya wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini iliongezeka kufikia kaya 1,118,752 zenye jumla ya wanufaika 5,259,503. Hadi Juni 2020, jumla ya shilingi bilioni 968.73 zilitolewa kwa kaya 1,118,752 kutoka vijiji/Mitaa/Shehia 9,989 katika halmashauri 161 za Tanzania Bara na Wilaya zote Zanzibar.

Aidha, jumla ya kaya 288,837 zilishiriki katika ajira za muda na miradi midogo 7,775 yenye thamani ya shilingi milioni 112.7. Jumla ya shilingi bilioni 80.8 zilitumika kulipa ujira kwa wanufaika wa miradi ikilinganishwa na shilingi bilioni 83.3 zilizolipwa mwaka 2018. Vile vile, utekelezaji wa programu ya ajira za muda (Public Works Programme - PWP) umewezesha kaya wanufaika kupata kipato cha ziada kutokana na ujira uliolipwa.

Katika utekelezaji wa Mpango wa Kuweka Akiba na Kuwekeza, walengwa wamepata mafunzo ya stadi za ujasiriamali na mbinu za kuunda vikundi endelevu vya kuweka akiba na kuwekeza. Hadi Disemba 2020, jumla ya vikundi 23,618 vya kuweka Akida na kuwekeza vyenye jumla ya wanachama 319,940 viliundwa. Vikundi hivyo vilikusanya akiba ya shilingi bilioni 5.9 ambapo shilingi bilioni 2.5

zilitumika kutoa mikopo kwa wanachama kwa ajili ya shughuli za kujiongezea kipato, ikilinganishwa na vikundi 16,366 vilivyoanzishwa mwaka 2018 vikiwa na wanachama 226,050, akiba ya shilingi bilioni 2.5 na kufanikiwa kutoa jumla ya mikopo ya shilingi bilioni 1.1.

Kadhalika, katika kutekeleza Mpango wa kuendeleza Miundombinu ya Huduma za Jamii, jumla ya miradi 772 ya kuboresha na kuendeleza miundombinu yenye thamani ya shilingi bilioni 36.6 imetekelezwa na kukamilika katika sekta za elimu, afya na maji. Kutokana na utekelezaji wa miradi hiyo, wananchi wamenufaika kwa kujenga madarasa (125), nyumba za walimu (95), mabweni ya wanafunzi (22), matundu ya vyoo (421), madawati (2,498), ofisi za walimu (3), zahanati (39), nyumba za watumishi wa afya (27), mifereji ya umwagiliaji, mabwawa ya kuhifadhi maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo pamoja na uhifadhi wa mazingira na misitu kupitia upandaji wa miti.

**2.3.2.2 Upatikanaji wa Chakula**

Tathmini ya awali ya hali ya Uzalishaji wa Mazao ya Chakula kwa msimu wa 2019/20 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2020/21 inaonesha kuwa hali ya uzalishaji wa chakula inatarajiwa kufikia kiasi cha tani 17,742,388 kwa mlinganisho wa nafaka *(Grain Equivalent)* ikilinganishwa na tani 16,408,309 zilizozalishwa msimu wa mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 7.5. Katika msimu wa uzalishaji wa mwaka 2019/20, uzalishaji wa mazao ya nafaka unatarajiwa kufikia tani 10,453,823 ikilinganishwa na uzalishaji wa tani 9,007,909 kwa msimu wa mwaka 2018/19, sawa na asilimia 16.05.

Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2020/21 yanakadiriwa kuwa tani 14,347,955 (tani 9,131,803 ni za mazao ya nafaka na tani 5,216,152 ni mazao yasiyo ya nafaka) ikilinganishwa na tani 13,842,536 kwa mwaka 2019/20. Kwa kuzingatia makadirio ya mahitaji ikilinganishwa na uzalishaji, nchi itakuwa na ziada ya chakula kiasi cha tani 3,394,434, ambapo tani 1,322,020 ni za mazao ya nafaka na tani 2,072,413 ni za mazao yasiyo ya nafaka.

Kwa kuzingatia Kigezo cha Upimaji wa Kiwango cha Utoshelevu wa Chakula *(Self Sufficiency Ratio – SSR),* kwa mwaka 2020/21 nchi inatarajiwa kuwa na kiwango cha utoshelevu wa asilimia 124 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 118 katika msimu wa 2019/20. Kiwango cha utoshelevu wa chakula kimetokana na uzalishaji mzuri wa mazao ya chakula ikilinganishwa na mahitaji ya chakula.

# SURA YA TATU

# MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza kwa muhtasari utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/20 na nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21. Aidha, inaainisha bajeti iliyopangwa, kiasi cha fedha kilichotumika kwa kipindi husika na hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

## 3.2 Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 na Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2020/21

### 3.2.1 Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2019/20

Katika mwaka 2019/20, Serikali ilitenga shilingi bilioni 12,248.6 sawa na asilimia 37.0 ya Bajeti ya Serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 9,737.7 sawa na asilimia 79.5 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2,510.9 sawa na asilimia 20.5 ni fedha za nje. Hadi Juni 2020, jumla ya shilingi bilioni 8,365.1 zilitolewa kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali. Kati ya fedha zilizotolewa, shilingi bilioni 6,678.7 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1,686.4 ni fedha za nje. Vile vile, jumla ya shilingi bilioni 1,462.6 zilipelekwa moja kwa moja na Washirika wa Maendeleo kwenye utekelezaji wa miradi, na hivyo kufanya utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kufikia asilimia 80.2. Katika kipindi husika, Serikali ilitumia shilingi bilioni 8,109.1 kwa ajili ya kulipa madeni ya fedha zilizotumika kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

### 3.2.2 Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2020/21

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21 ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 12,779.3 sawa na asilimia 37 ya bajeti ya Serikali. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 10,043.2 sawa na asilimia 78.6 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2,736.0 sawa na asilimia 21.4 ni fedha za nje.

Hadi Desemba 2020, jumla ya shilingi bilioni 2,599.0 zimetolewa kugharamia miradi ya maendeleo ikijumuisha shilingi bilioni 2,512.8 fedha za ndani na shilingi bilioni 86.2 fedha za nje. Katika kipindi husika, Serikali imetumia shilingi bilioni 4,019.3 kulipa madeni ya fedha ambazo zilitumika kugharamia miradi ya maendeleo. Vile vile, kiasi cha shilingi bilioni 712.5 ni fedha za Washirika wa Maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi na hivyo kufanya utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kufikia asilimia 69.0. Baadhi ya miradi iliyopokea

fedha za maendeleo ni pamoja na: Shilingi bilioni 351.0 kwa ajili ya ujenzi wa ya reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (Standard Gauge Railway); Shilingi bilioni 531.9 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja; Shilingi bilioni 21.05 kwa ajili mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere katika mto Rufiji - MW 2,115; Shilingi bilioni 171.9 kwa ajili ya miradi ya umeme; Shilingi bilioni 12.8 kwa ajili ujenzi na ukarabati wa meli katika maziwa makuu; na shilingi bilioni 124.8 kwa ajili ya elimu msingi bila ada.

### 3.3 Hatua za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Katika mwaka 2019/20 na nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21 Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya kielelezo na miradi mingine katika maeneo ya kipaumbele yaliyobainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni pamoja na:

#### 3.3.1 Miradi ya Kielelezo

Utekelezaji wa baadhi ya miradi ya kielelezo hadi nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21 ulikuwa kama ifuatavyo:-

**(a) Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa - *Standard Gauge Railway***

Ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (km 300) unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90 na kipande cha Morogoro - Makutupora (km 422) utekelezaji umefikia asilimia 49.2. Aidha, Serikali imesaini mkataba na Mkandarasi ili kuanza ujenzi wa kipande cha Mwanza – Isaka (km 341) wenye thamani ya shilingi trilioni 3.07. Vile vile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vipande vya Makutupora – Tabora (km 294) na Tabora – Isaka (km 133). Katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 901.8 zimetumika na shilingi bilioni 351.0 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21.

**(b) Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania**

Katika mwaka 2019/20, Serikali imepokea ndege mbili (2) aina ya Boeing 787-8 Dreamliner na Bombardier Dash 8 Q400 ambazo zimeanza kazi; kukamilika kwa malipo ya awali ya ununuzi wa ndege mpya tatu (3) ambapo ndege mbili (2) ni aina ya Airbus A220-300 na moja (1) ni aina ya De Havilland Dash 8-400; kukamilika kwa ufungaji wa jenereta pamoja na ukarabati wa mfumo wa umeme na mfumo wa kupambana na majanga ya moto katika karakana ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA); kukamilika kwa taratibu za ununuzi wa jozi ya injini za akiba kwa ndege aina ya Dash 8 Q400; na kulipa bima za ndege za Boeing 787-8 Dreamliner na Dash 8 Q400. Aidha, ATCL imeanza kutoa huduma *(ground*

*handling services)* katika kiwanja cha ndege cha Dodoma. Katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 315.2 zimetumika na shilingi bilioni 2.5 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21.

**(c) Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa tuta kuu la bwawa (Main Dam); kukamilika kwa ujenzi wa handaki la kuchepusha maji (*Diversion Tunnel*) na kuanza kuchepusha maji kupisha ujenzi wa tuta kuu la bwawa; kuanza ujenzi wa mihimili ya handaki (*Tunnel Concrete Lining*) na matuta ya kuelekeza maji kwenye handaki (Coffer dam); kuendelea kwa ujenzi wa mgodi wa kuzalisha umeme; na kuendelea na ujenzi wa njia za kupeleka maji kwenye mitambo ya kufua umeme. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 25.8. Utekelezaji wa mradi huu ulitumia shilingi bilioni 693.2 katika mwaka 2019/20 na shilingi bilioni 128.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21.

**(d) Kanda Maalum za Kiuchumi**

- **(i) Eneo Maalum la Uwekezaji Bagamoyo:** Kazi zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa rasimu ya mikataba ya utekelezaji wa mradi wa Bagamoyo SEZ; na kupatikana kwa Mshauri Mwelekezi (Chuo Kikuu Ardhi) atakayepima na kuweka alama za mipaka katika eneo lililolipiwa fidia (hekta 2,600).
- **(ii) Eneo Maalum la Uwekezaji Kigoma:** Kazi zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa upembuzi yakinifu na Mpango Kabambe wa uendelezaji wa eneo pamoja na kuendelea na jitihada za kutafuta wawekezaji watakaowekeza katika eneo hilo. Hadi sasa kampuni tatu (3) zimepewa leseni na kuanza uwekezaji katika eneo hilo. Makampuni hayo ni *Third Man Limited* kwa ajili ya uchakataji wa asali na nta, *Next Gen Solawazi Ltd* ya uzalishaji wa nishati ya umeme wa nguvu ya jua na *SGC* Investment Ltd inayochakata zao la michikichi na ghala.
- **(iii) Eneo Maalum la Uwekezaji Mtwara Free Port Zone:** Kazi zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme na barabara za ndani ya eneo la mradi yenye urefu wa kilomita tatu (3); na kukamilika kwa michoro ya jengo la kituo cha pamoja cha huduma *(One Stop Center Building).*

**(e) Kuongeza Rasilimali Watu Wenye Ujuzi Adimu na Maalumu (Ujuzi wa Kati na Wabobezi) kwa Maendeleo ya Viwanda na Watu**

- (i) **Wizara ya Nishati:** Hatua iliyofikiwa ni kugharamiwa kwa mafunzo ya vijana 24 katika fani za mafuta na gesi kwa ngazi za Shahada ya

Uzamivu (3), Shahada ya Uzamili (19) na Shahada ya kwanza (2); na mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 8 wa TPDC na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 50 wa Wizara ya Nishati, PURA, EWURA, TRA na Timu ya Majadiliano ya mradi wa LNG kuhusu usimamizi na uendeshaji wa miradi ya mafuta na gesi;

(ii) **Wizara ya Madini:** Hatua iliyofikiwa ni kupatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu watumishi 45 katika fani za Jiolojia, Jemolojia, Uhandisi migodi na utunzaji wa kumbukumbu na utafutaji wa madini. Kati ya hao, watumishi 18 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada ya kwanza (1), Shahada ya Uzamili (13), Shahada ya Uzamivu (4) na watumishi 27 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi katika fani husika;

(iii) **Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto:** Hatua iliyofikiwa ni kugharamiwa madaktari 311 kuendelea na masomo ya kibingwa na kuratibu mafunzo kwa wanafunzi 50 kupitia ufadhili kutoka Serikali ya China kwenda China kwa masomo ya udaktari;

(iv) **Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia:** Hatua iliyofikiwa ni kuendelea kudhamini mafunzo kwa wanafunzi madaktari 158 katika fani za ubobezi kwa magonjwa ya damu na utoaji damu (1), magonjwa ya utumbo na ini (2), upasuaji wa utumbo na ini (3), magonjwa ya figo (1), magonjwa ya kifua (1), udaktari bingwa (102), ufamasia (6), uuguzi (14), afya ya jamii na mazingira, menejimenti na taarifa za afya (28);

(v) **Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili – MUHAS:** Hatua iliyofikiwa ni kuhitimu kwa wataalamu 15 katika fani ya udaktari bingwa maalum (Master of Science Super-specialty) kwa magonjwa ya: Moyo (4), ubongo na mishipa ya fahamu (3), damu na utoaji damu (1), utumbo na ini (4), figo (2), na njia ya mkojo (1). Vile vile, madaktari bingwa 131 wamehitimu mafunzo katika fani mbalimbali zikiwemo udaktari bingwa katika huduma za usingizi, magonjwa ya dharura na mahututi, mifupa na mivunjiko, watoto, radiolojia, upasuaji na njia ya mkojo. Mafanikio mengine ni kuhitimu kwa wataalamu 102 wasaidizi wa madaktari bingwa katika nyanja za sayansi ya uuguzi wa afya ya akili, magonjwa mahututi na ajali, ukunga na afya ya akinamama, ufamasia, afya ya jamii na mazingira na sayansi ya menejimenti ya taarifa za afya. Aidha, Chuo kwa kushirikiana na Ubalozi wa China kimepeleka wataalamu 18 nje ya nchi kusomea ubingwa na ubobezi katika fani za upandikizaji figo, ini na uboho (*bone marrow*); na

(vi) **Hospitali ya Mloganzila:** Hatua iliyofikiwa ni kugharamiwa mafunzo

kwa watumishi 55 katika fani mbalimbali za kibingwa (NmeD) ambao wanaendelea na masomo katika Chuo cha Muhimbili (MUHAS) na Bugando. Vile vile, Hospitali kwa kushirikiana na Serikali za China na Korea ya Kusini imepeleka wataalamu sita (6) katika nchi hizo kwa ajili ya mafunzo mbalimbali.

**(f) Kiwanda cha Sukari Mkulazi**

Katika shamba na kiwanda cha **Mbigiri (Mkulazi II) kinachotekelezwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Jeshi la Magereza**: kulimwa na kupandwa miwa eneo lenye hekta 2,061 kwenye shamba la Mbigiri; kukamilika kwa ufungaji wa mifumo ya umwagiliaji shamba la Mbigiri kwenye eneo la hekta 700 na kuanza eneo lingine lenye ukubwa wa hekta 756; kununua vifaa na mashine mbalimbali za kilimo ikijumuisha e*xcavator* moja (1) ya tani 21, matrekta makubwa matano (5), *roller compacter* moja (1) ya tani 10, *bull dozer* moja (1); kukamilisha ufungaji wa umeme umbali wa kilomita 11.18; kukamilika ujenzi wa jengo la zahanati, ofisi, uzio, nyumba saba (7) za wafanyakazi na barabara ya urefu wa kilomita 19 (asilimia 85), ukamilishaji wa ujenzi wa bwawa kubwa lenye ujazo wa mita za ujazo 1,600,000 na mabwawa matatu yenye mita za ujazo 50,000 kila moja; na ujenzi wa mtaro wa maji utakaokuwa na uwezo wa kumwagilia hekta 1000 unaendelea. Mafanikio mengine ni kupatikana kwa mshauri elekezi wa mifumo ya umwagiliaji na mitambo ya kiwanda katika eneo la **Mkulazi I**.

**(g) Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia - Lindi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ulipaji wa fidia ya shilingi bilioni 5.2 kwa wananchi watakaopisha mradi; kuendelea na maandalizi ya majadiliano baina ya Serikali na kampuni za uwekezaji kuhusu Mikataba Hodhi ya utafutaji na uendelezaji wa mradi.

**(h) Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa tathmini ya athari za mazingira; kuendelea na utoaji wa elimu kwa umma kwa maeneo ya pembezoni mwa eneo la mradi; kukamilika kwa majadiliano ya maeneo mawili (2) kati ya matatu (3) ya mikataba ikiwemo ya Nchi Hodhi na wawekezaji, mkataba wa ubia, mkataba wa bandari na mkataba wa pango la ardhi. Katika mwaka 2019/20 na nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21 kiasi cha shilingi bilioni 1 kimetumika.

**(i) Makaa ya Mawe Mchuchuma na *Vanadium, Titanium* na Chuma Liganga**

Kazi zilizotekelezwa ni: Kukamilika kwa uhakiki wa mali za wananchi

watakaopisha ujenzi wa miradi hii. Aidha, upitiaji wa mikataba kati ya NDC na mwekezaji unaendelea; na kulipwa kwa ada za leseni za kuchimba madini katika maeneo yaliyo chini ya NDC katika eneo la mradi.

### 3.3.2 Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda

#### 3.3.2.1 Viwanda

**(a) Shirika la Viwanda Vidogo - SIDO**

Kazi zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa majengo 12 ya viwanda (Industrial Shades) katika Mitaa ya Viwanda ya SIDO iliyopo mikoa ya Dodoma (3), Manyara (3), Kagera (1), Mtwara (1) na Geita (4) ambapo viwanda 29 vimesimikwa katika majengo hayo na kuzalisha ajira 648; kutolewa kwa mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara kwa wajasiriamali 5,640; kutolewa kwa mikopo 2,020 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.9 kwa wajasiriamali mbalimbali kote nchini. Kati ya mikopo hiyo, asilimia 51.3 ilitolewa kwa wanawake na asilimia 48.7 ilitolewa kwa wanaume. Aidha, asilimia 39.2 ya mikopo hiyo ilitolewa maeneo ya vijijini na asilimia 60.8 ilitolewa mijini. Mikopo hiyo iliwezesha kuanzishwa kwa viwanda 551 na ajira 6,193.

**(b) Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC)**

Kazi zilizotekelezwa ni: kubuni na kuunda sampuli kifani (Prototypes) na kuzalisha mashine ya kupura na kupepeta alizeti (3), mashine ya kupukuchua mahindi (2), mashine ya kupandia (11), mashine ya kukata majani ya kulisha mifugo iendeshwayo kwa umeme (5), mashine za kupura mazao mchanganyiko (3), mashine ya kusaga karanga (1) na mashine za kufyatua matofali ya udongo saruji; kuzalishwa kwa mashine 36 za kubangua korosho zinazoendeshwa kwa kutumia miguu pamoja na viti; kutengenezwa kwa matoroli sita (6) ya kusombea korosho; kutengenezwa kwa meza sita (6) pamoja na viti kwa ajili ya kubangua na kupanga korosho; ukarabati wa mitambo ya bayogesi iliyojengwa chini ya ufadhili wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) katika Shule ya St. Bakanja Wilayani Buhigwe - Kigoma na Shule ya *Queen of Apostles* Wilayani Ushirombo - Geita; uhakiki wa jumla ya mitambo 259 ya bayogesi ya TDBP na mitambo 817 ya watekelezaji wenza wa TDBP; kukamilika kwa awamu ya tatu ya mafunzo ya ujasiriamali katika bayogesi kwa wanawake vijana 100 wa jamii za kifugaji katika wilaya ya Ngorongoro kwa kufanya mafunzo ya awali ya biashara katika sekta ya bayogesi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mitambo ya bayogesi na matumizi ya mbolea hai (bioslurry) inayotoka kwenye mtambo wa bayogesi; kutolewa kwa mafunzo kwa vitendo kwa wakulima wa Halmashauri ya Meru kuhusu namna ya kutumia teknolojia za kukata na

kufunga majani ya malisho ya mifugo; na kutoa elimu kwa wakulima 15 katika wilaya ya Mbozi mkoani Songwe kuhusu namna ya kutumia kipandio *(Planter)* kikubwa cha mazao mbalimbali kinachovutwa na trekta.

**(c) Kuendeleza Kongane ya Viwanda TAMCO - Kibaha**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa mita 980; kuendeleza eneo la ekari 201.6 ili kuvutia uwekezaji ambapo ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha chanjo za wanyama cha *Hester-Bioscience* umekamilika; kuanza kwa uzalishaji wa kiwanda cha kuunganisha magari cha *GF Trucks motors*; na kukamilika kwa kazi ya usanifu wa ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme pamoja na tathmini ya mahitaji ya maji kwa ajili ya eneo lote la TAMCO.

**(d) Mradi wa Kuunganisha Matrekta TAMCO - Kibaha**

Kazi zilizofanyika ni: kukamilika kwa ujenzi wa jengo la kiwanda kipya cha kuunganisha matrekta; kuunganishwa kwa matrekta 822 kati ya 2,400 aina ya URSUS yaliyoingizwa nchini kutoka Poland yakiwa katika vipande (*semi knocked down);* na kuuzwa kwa matrekta 756, majembe 511 ya kulimia na majembe 233 ya kusawazisha.

**(e) Mradi wa Magadi Soda – Bonde la Engaruka - Arusha**

Kazi zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa uthaminishaji wa ardhi na mali za wananchi pamoja na uhakiki wa uthaminishaji; kukamilika kwa uchambuzi wa kiwango cha magadi soda kilichopo, teknolojia inayohitajika (faida na hasara), uthibitisho wa teknolojia itakayochaguliwa pamoja na kuandaa michoro ya uzalishaji magadi soda na chumvi ya kawaida; kufanyika kwa Tathmini ya Athari za Kimazingira (EIA) na utafiti wa masoko ya Magadi Soda; na kuendelea kutangaza mradi ili kuvutia wawekezaji.

**(f) Kongane ya Viwanda vya Ngozi – Dodoma**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa kazi ya usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na majengo ya viwanda kwa ajili ya wajasiriamali; na kuanza kwa ujenzi ambapo utekelezaji upo katika hatua za kukamilisha msingi.

**(g) Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO)**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kusimamia ujenzi wa viwanda nchini kama vile kiwanda cha kimataifa cha bidhaa za ngozi Kilimanjaro *(Kilimanjaro International Leather Products - KILP)*; kutengeneza ramani za viwanda nchini (industrial mapping); kufanya ukaguzi wa kitaalamu kwa viwanda vilivyokufa na vinavyoongeza uzalishaji (*technical, economical and environmental Audit*); kufanya

tafiti nne (4) na kuatamia wabunifu wapatao 6 (*incubation*); kununuliwa kwa vifaa vya maabara kwa ajili ya tafiti mbalimbali zikiwemo za mazao ya korosho na mchikichi; kuhakiki ubora wa sampuli 174 za bidhaa mbalimbali za chakula na maji kutoka viwandani, wajasiriamali na kampuni mbalimbali hapa nchini; kubuni na kutengeneza mashine kwa ajili ya kiwanda cha mfano cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua kilo 300 kwa saa; kutekeleza mradi wa ubunifu na usambazaji wa vitofali lishe vya kuzalishia uyoga wenye virutubisho *(mushroom substrate blocks).*

**(h) Shirika la Uhandisi na Usanifu Mitambo (TEMDO)**

Kazi zilizofanyika ni: kununuliwa na kufungwa kwa mitambo na vifaa vya kisasa kwa ajili ya maabara za utafiti; kununuliwa kwa mtambo mdogo wa kuchakata tani 1.25 za mafuta ya mawese kwa siku; kutengeneza mtambo (prototype) wa kukamua mafuta; kufanyika kwa majaribio ya teknolojia zilizohakikiwa na kusambaza mashine ya kukamua mbegu za alizeti kwa wajasiriamali; kusanifu uundaji wa mtambo wa kuchakata na kukausha muhogo; kubuni mtambo wa kukamua miwa na kutengeneza Sukari kwa ajili ya wajasiriamali wa kati na wadogo; kubuni teknolojia ya kukamua mchuzi wa zabibu (*Grapes Distemer*); na kukamilisha uundaji wa mashine ndogo (Korona) kwa ajili ya kuchakata mkonge.

**(i) Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools (KMTC)***

Kazi zilizotekelezwa ni: kuzalisha matrela 50 kwa ajili ya matrekta ya URSUS; kuzalisha mashine za kuchakata mbao; kuunda mashine za kuchakata mazao ya kilimo; na kuunda viambata kwa ajili ya matrekta, pampu za maji na kuzalisha vipuli kwa matumizi ya viwandani.

**(j) Kuendeleza Shirika la *Tanzania Automotive Technology Centre* (TATC)**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kuboresha gari la NYUMBU na kuliwezesha kutembea kwa kutumia magurudumu manne (*Four Wheel Drive*), kuliongezea uwezo wa kubeba tani tatu kutoka kilo mia tano za awali na kuliongezea mwendokasi kutoka kilomita 50 hadi km 110 kwa saa; kukamilika kwa gari moja (1) la zimamoto na kuendelea kuunganisha gari la pili ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80; na kununuliwa kwa mitambo na vipuri kwa ajili ya uundaji wa magari ya zimamoto.

**(k) Kiwanda cha *Kilimanjaro International Leather Industries Co Ltd***

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa awamu ya kwanza wa kiwanda kipya unaojumuisha majengo ya kiwanda cha viatu chenye uwezo wa kuzalisha jozi na soli za viatu 1,200,000 kwa mwaka na kuchakata ngozi futi za mraba 13,000,000 kwa mwaka; na kuendelea na ujenzi wa majengo ya awamu ya pili yanayojumuisha

kiwanda cha kuchakata ngozi (tannery), maabara na kantini ambao umefikia asilimia 35. Kiwanda kinazalisha kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.

**(l) Kiwanda cha Kuchakata Tangawizi**

Mfuko wa PSSSF kwa kushirikiana na Chama cha Wakulima wa Tangawizi wa Mamba-Same Mkoani Kilimanjaro unajenga kiwanda cha kuchakata tangawizi. Kukamilika kwa mradi huu utaongeza idadi ya wakulima wa tangawizi kutoka 3,000 waliopo sasa hadi kufikia 10,000. Mashine kwa ajili ya kuchakata tangawizi zimenunuliwa na kupelekwa eneo la kiwanda na zinasubiri ukarabati wa jengo ukamilike ili zifungwe na kuanza uzalishaji Aprili 2021.

**(m) *Nguru Hills Ranch Ltd***

Kiwanda cha Nguru Hills Ranch Ltd kipo Mvomero mkoani Morogoro ambapo mfuko wa PSSSF uliingia makubaliano na Makampuni ya *Eclipse LLC na Busara Investment LLP* mwaka 2017 ili kuendesha na kuzalisha kwa pamoja nyama ili kuiuza katika soko la Mashariki ya Kati na maeneo mengine ya Afrika. Kiwanda kitaajiri jumla ya wafanyakazi 350 na kitatoa mafunzo ya mafunzo ya ufugaji bora.

**(n) Kiwanda cha Kuchakata Mazao**

Mfuko wa NSSF umewezesha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) kuanzisha viwanda vya kusaga nafaka na kukamua mafuta ya alizeti vilivyo Kizota-Dodoma kwa kuwapatia mkopo wa shilingi bilioni 3.676. Uwekezaji huu umewezesha kununua mashine na mitambo ya kisasa ya kusaga mazao ya nafaka na kukamua mbegu za alizeti. Viwanda hivi viwili vina uwezo wa kusaga tani 18,000 za mahindi na tani 12,000 za mbegu za alizeti kwa mwaka. Viwanda vimeanza kuzalisha Desemba, 2019 na hadi kufikia mwezi Januari 2021 vimetoa ajira kwa Watanzania wapatao 182.

**3.3.2.2 Kilimo**

**(a) Kilimo cha Kahawa**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendeshwa kwa minada nane (8) ya kahawa katika mikoa ya Kilimanjaro (2), Songwe (4) na Ruvuma (2); kukaguliwa kwa viwanda 24 na maghala 30 na kutolewa leseni za kuendesha biashara ya kahawa; kutolewa kwa mafunzo ya mfumo wa masoko ulioboreshwa katika kanda nne (4) za uzalishaji wa kahawa; kutolewa kwa mafunzo ya utayarishaji wa kahawa ngazi ya awali (*primary processing*) kwa vyama 102 vya msingi vya ushirika vinavyomiliki viwanda vya kuchakata kahawa mikoa ya Ruvuma na Songwe; kutolewa kwa mafunzo ya kilimo bora cha kahawa kwa wakulima 4,567 ambapo walihamasishwa kubadili mashamba

yao na kupanda miche bora; na kufanyika kwa uhamasishaji wa unywaji wa kahawa kwa kushiriki maonesho ya wakulima ya nanenane katika mikoa ya Arusha, Mbeya, Kagera na Simiyu.

**(b) Kilimo cha Mpunga**

Shughuli zilizofanyika ni: kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 36,614 mwaka 2015 hadi tani 71,000 mwaka 2020; kukamilika kwa ujenzi wa maabara ya mbegu katika Makao Makuu ya Wakala wa Mbegu za Kilimo – Morogoro; kuzalishwa kwa kilo 14,700 za mbegu za mpunga za daraja la awali (*pre-basic*) aina ya TXD 306, TXD 88, Komboka, Tai, Supa na NERICA 1; kusafishwa (*purification*) kwa aina 11 za mbegu za mpunga ambapo jumla ya kilo 1,810 za daraja la mtafiti zilipatikana; kukamilika kwa uhakiki wa usafi wa mbegu za mpunga kupitia mashamba maalumu (*control plots*); kukaguliwa kwa hekta 164.54 za uzalishaji mbegu za madaraja mbalimbali katika vituo vya ASA – Morogoro (hekta 85.84), TARI - Ifakara (hekta 26.4), TARI - Dakawa (hekta 24) na halmashauri za wilaya (hekta 28.3); kutolewa kwa mafunzo kwa wakulima 400 wa halmashauri za wilaya za Kilombero, Ulanga, Kilosa, Mvomero na Morogoro pamoja na kufanyika kwa tathmini ya matumizi na usambazaji wa teknolojia ya kilimo shadidi cha mpunga; mafunzo ya usimamizi wa mpunga kabla na baada ya kuvuna ili kupunguza upotevu na kuimarisha ubora yalitolewa kwa wakulima viongozi wapatao 210 (wanaume 111 na wanawake 99) na Maafisa Ugani 75 (wanaume 51 na wanawake 22) kutoka skimu 40 za umwagiliaji; na kusambazwa kwa nakala 2,105 za Mwongozo wa Mkulima wa Udhibiti Husishi wa Visumbufu na Magonjwa kwenye zao la Mpunga.

**(c) Kilimo cha Korosho**

Hatua iliyofikiwa ni: kusambazwa kwa tani 40,592.6 za Salfa na lita 1,314,465 za viuatilifu maji kwa wakulima wa korosho ambapo tani 2,170.5 za Salfa na lita 88,693 za viuatilifu vya maji zimesambazwa na Bodi ya Korosho, tani 29,691.5 za Salfa na lita 1,076,458 za viuatilifu vya maji zimesambazwa na Sekta Binafsi, na tani 8,730.6 za Salfa na lita 149,314 za viuatilifu vya maji zimesambazwa na vyama vikuu vya ushirika; kuendelea na usimamizi wa mauzo ya korosho ghafi na utoaji wa vibali vya kusafirisha korosho ndani na nje ya nchi; kukusanywa kwa tani 232,681.7 za korosho ghafi katika maghala ya mnada na ya vyama vya ushirika vya msingi ambapo jumla ya tani 228,142.9 zenye thamani ya shilingi bilioni 579.2 zimeuzwa; kusafirishwa kwa tani 215,280 za korosho ghafi na tani 780,832 za korosho zilizobanguliwa kwenda nchi za India, Vietnam, China na Sri Lanka; kutolewa kwa mafunzo kwa wakulima 163 na maafisa ugani 249 kuhusu kilimo bora cha korosho ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi na salama ya viuatilifu; kuhakikiwa kwa

wakulima 285 waliozalisha miche 5,815,519 katika mikoa ya Pwani, Tanga, Morogoro, Kilimanjaro, Mbeya, Iringa, Njombe, Songwe pamoja na halmashauri za Mbinga Mji, Masasi Mji na halmashauri ya wilaya ya Masasi; na kusajiliwa kwa kampuni 49 kushiriki minada ya korosho.

**(d) Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kujengwa na kuboreshwa kwa miundombinu ya umwagiliaji ambayo imeongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 461,376 mwaka 2015 hadi hekta 694,715 mwaka 2020; kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za Kigugu – Mvomero yenye hekta 200 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98, Mvumi – Kilosa yenye hekta 249 (asilimia 100), Msolwa Ujamaa – Morogoro yenye hekta 675 (asilimia 98), Njage – Kilombero yenye hekta 325 (asilimia 100), Shamba la Mbegu Kilangali – Kilosa yenye hekta 400 (asilimia 80). Aidha, wanachama 311 wa Umoja wa Umwagiliaji kutoka katika skimu za umwagiliaji za Njage, Msolwa Ujamaa, Mvumi, Kigugu na Mbogo Komtonga wamepatiwa mafunzo ya kuimarisha na kuendesha umoja wao, usimamizi na matengenezo ya miundombinu ya umwagiliaji, utunzaji wa kumbukumbu, usimamizi wa fedha na usuluhishi wa migogoro.

**(e) Ujenzi wa Maghala na Kuboresha Hifadhi ya Taifa ya Chakula**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kukamilisha ujenzi wa maghala matano (5) ya kuhifadhi mpunga kupitia mradi wa kuongeza uzalishaji wa mpunga – *Expanded Rice Production Project* ikiwemo Msolwa Ujamaa lenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,700 (asilimia 96), Njage lenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,700 (asilimia 99), Kigugu lenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 (asilimia 98) na Mbogo Komtonga lenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 (asilimia 98); kuendelea kwa ujenzi wa vihenge na maghala katika maeneo ya Songea (asilimia 74.45), Makambako (asilimia 71.09), Mbozi (asilimia 73.4), Dodoma (asilimia 85.64), Shinyanga (asilimia 69.02), Mpanda (asilimia 88.1), Sumbawanga (asilimia 58.57) na Babati (asilimia 95.82); kununuliwa kwa tani 25,682 za mahindi ikilinganishwa na lengo la tani 18,182 sawa na asilimia 141.2; na kukarabatiwa kwa maghala 105 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 31,500 katika halmashauri za Mbozi (46), Momba (4), Mbeya (13), Iringa (11), Mufindi (10), Njombe (4), Kalambo (9) na Madaba – Songea (8).

**(f) Utafiti wa Kilimo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuzalishwa kwa mbegu mpya bora za mazao 40; kuongeza uzalishaji wa mbegu za awali katika vituo vya utafiti kutoka tani 641.79 mwaka 2018/19 hadi tani 1,011.75 mwaka 2019/20; kuzalishwa na kusambazwa kwa jumla ya miche 11,830,444 ya mazao ya korosho, michikichi, muhogo, mkonge, mgomba,

miwa, nazi na zabibu kwa wakulima; na kukarabatiwa kwa maabara mbili (2) za baioteknolojia za vituo vya utafiti TARI - Makutupora na TARI -Tengeru.

**(g) Mkakati wa Uzalishaji wa zao la Michikichi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa kwa mbegu za awali kwa ajili ya kuzalisha miche ya michikichi ambapo miche 322,521 imeendelea kukuzwa katika mashamba ya mbegu ya ASA (Bugaga Kigoma - miche 79,440, Shamba la Mwele, Tanga - miche 72,000, shamba la msimba Morogoro - miche 126,781 na shamba la mbozi Songwe - miche 44,300). Vile vile, kupitia TARI na Sekta Binafsi jumla ya mbegu 4,205,335 zinazotosha kupanda ekari 84,106.7 zimezalishwa. Kati ya hizo, mbegu 2,184,111 zimesambazwa kwa wakulima ili kuoteshwa ambapo mbegu 1,370,318 zimeoteshwa na kupandwa kwenye viriba. Miche hiyo iliyopatikana inatosha kupanda ekari 27,406.36 ambapo hadi sasa ekari 270 zimepandwa (Gereza la Kwitaga 50, Gereza la Ilagala 80 na JKT Bulombora 140).

**(h) Uzalishaji wa Mbegu Bora za Mazao**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa maabara ya mbegu katika Makao Makuu ya Wakala wa Mbegu za Kilimo Morogoro; kununuliwa kwa matrekta mawili (2), zana za kupandia, jembe la kupandia pamoja na mabomba ya kunyunyizia dawa kwa ajili ya taasisi ya ASA; kutengenezwa kwa matenga ya kubebea miche kupeleka kwa wakulima; ununuzi wa viriba vya kuzalishia michikichi; kuendelea na uboreshaji wa shamba la mbegu la Bugaga kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji pamoja na ujenzi wa ofisi, ghala la kupokea na kuhifadhi mbegu na eneo la kuanikia mbegu *(Shed house).*

**(i) Uboreshaji wa Soko la Mazao kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko na Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA)**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa viwanda vya kusaga mahindi na kukamua mafuta ya alizeti vilivyopo Kizota – Dodoma; na kununuliwa kwa tani 13,415.713 za nafaka na mazao mengine kutoka kwa wakulima, vikundi vya wakulima, vyama vya ushirika na Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA). Aidha, NFRA imenunua mazao ya mahindi na mpunga na kuiwezesha Mamlaka hiyo kuwa na akiba ya nafaka ya tani 110,289,000.

**3.3.2.3 Mifugo**

(i) **Miundombinu ya Uzalishaji na Masoko**: Shughuli zilizotekelezwa ni: Kufikiwa kwa asilimia 40 ya ukarabati wa minada ya Ipuli, Igunga na Nata; kukamilika kwa uchimbaji wa kisima kirefu katika mnada wa mifugo wa upili wa Kirumi Butiama - Mara.

(ii) **Vituo vya Utafiti, Mafunzo na Ugani wa Mifugo:** Shughuli zilizotekelezwa ni: kuimarisha kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha NAIC kilichopo USA River Arusha kwa kununua kifaa (*Chiller*) kwa ajili ya mtambo wa kuzalisha kimiminika cha naitrojeni; kutolewa kwa elimu ya mafunzo rejea na maarifa mapya kuhusu uzalishaji wa kibiashara wa mifugo kwa wadau 8,158 katika halmashauri za Mvomero, Sumbawanga Mji, Sumbawanga Vijijini, Nkasi, Kalambo, Mpanda, Chato, Tanganyika, Mpimbwe, Nsimbo, Mlele, Meatu, Songwe, Ileje, Tunduma Mji, Mbozi, Momba, Mkuranga, Mbeya Jiji, Mbeya Vijijini, Mbarali, Chunya, Kyela, Busokelo na Rungwe; ukarabati wa hosteli 10 za kampasi za Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo - LITA, madarasa matatu (3), kumbi mbili (2) za mihadhara, maabara mbili (2), maktaba mbili (2) na kujenga vyoo vipya vitatu (3) vya wanafunzi.

Aidha, mashamba darasa 31 ya malisho ya mifugo yameanzishwa katika halmashauri 13 za Ikungi, Itigi, Mkalama, Iramba, Singida Manispaa, Singida Vijijini, Manyoni, Monduli, Rungwe, Njombe vijijini, Mufindi, Kahama na Kishapu. Vile vile, wachunaji 735 wa ngozi za mifugo na wataalamu 94 wa mifugo wamejengewa uwezo kuhusu uchunaji bora wa ngozi unaozingatia mahitaji ya soko kutoka katika mikoa nane (8); na kupatiwa elimu ya ufugaji wa kibiashara kwa wafugaji na wadau 115,979.

(iii) **Usimamizi wa Ardhi, Maji na Upatikanaji wa Malisho:** Shughuli zilizotekelezwa: Kupimwa na kuwekewa alama kwa mashamba na vituo vinane (8) vya kupumzishia mifugo vyenye ukubwa wa hekta 23,066.94. Mashamba hayo ni Hanga Ngadinga (4,200), Mahukuru Lilahi (3,100), Chibe (2,054), Shishiyu (3,170), Mkwese (5,036), Kinyangiri (3,419.94), Nachingwea (1,497) na Kelema (590); kutengwa kwa hekta 2,818,687.17 na kupimwa kwa hekta 108,427.49 za halmashauri za wilaya; kutengwa kwa vitalu 64 kwenye maeneo ya kupumzishia mifugo za Kinyangiri 12, Mkwese 23 (Singida), Chibe 10 (Shinyanga) na Shishiyu 19 (Simiyu); kutengwa kwa vitalu tisa (9) vyenye ukubwa wa zaidi ya hekta 7,000 kwa ajili ya SUMA JKT na takriban hekta 22,000 kwa ajili ya vijiji vya ranchi ya Missenyi.

Aidha, ujenzi wa kisima kirefu katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa (Usolanga) umefikia asilimia 50 na ukarabati wa malambo ya Chamakweza (Chalinze), Kimokua (Longido) na Narakauo (Simanjiro)

umefikia asilimia 15, asilimia 35 na asilimia 40 mtawalia.

**(iv)** **Tiba na Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo:** Shughuli zilizotekelezwa ni ujenzi wa jengo la kuzalisha chanjo za bakteria katika Kituo cha Kuzalisha Chanjo cha Kibaha (TVI) ambao umefikia asilimia 75; kuzalishwa na kusambazwa kwa dozi 49,008,325 za chanjo za mifugo katika halmashauri 40 dhidi ya magonjwa ya Mdondo (47,347,700), Kimeta (626,000), Chambavu (113,000), Homa ya Mapafu ya Ng'ombe - CBPP (756,600), Kutupa Mimba (19,275) na Chanjo Mchanganyiko wa Kimeta na Chambavu - TECOBLAX (145,750).

**3.3.2.4 Uvuvi**

**(i)** **Bandari ya Uvuvi (Mbegani):** Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi.

**(ii)** **Kuimarisha Tafiti, Huduma za Ugani na Mafunzo ya Uvuvi:** Hatua iliyofikiwa ni: kusambazwa kwa matenki 22 kwa ajili ya kukuza vifaranga pamoja na kukarabati mabwawa nane (8) katika vituo vinne (4) vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji vya Kingolwira - Morogoro, Mwamapuli - Tabora, Ruhila - Ruvuma na Nyengedi – Lindi; ununuzi na upandikizaji wa samaki wazazi 27,640 katika vituo vya Ruhila (2,100), Nyengedi (8,000), Mwamapuli (5,900) na Kingolwira (11,640); uwekaji wa vizimba vya kusimika (*Happa nets*) 60 (Ruhila - 50 na Mwamapuli – 10); na kupatikana kwa eneo lenye ukubwa wa ekari 25 Rubambagwe - Geita kwa ajili ya kujenga kituo cha kuendeleza ukuzaji viumbe maji kitakachokuwa na uwezo wa kuzalisha vifaranga vya samaki milioni 2 kwa mwaka na kutoa mafunzo ya teknolojia ya ufugaji katika vizimba; uanzishwaji wa Agenda ya Taifa ya Utafiti wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji; uanzishwaji wa Kanzidata ya Tafiti za Uvuvi na Ukuzaji viumbe maji ambao umesaidia kuweza kukusanya taarifa za tafiti za uvuvi na ukuzaji viumbe maji kutoka tafiti 22 mwaka 2015 hadi tafiti 500 mwaka 2020; na kutungwa kwa Kanuni za kusimamia tafiti katika Tasnia ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji ambao umesaidia kutoa miongozo ya namna ya kufanya tafiti, usambazaji na matumizi ya taarifa za tafiti.

**(iii)** **Kusimamia na Kuhamasisha Uwekezaji katika Uvuvi na Viwanda vya Kuchakata Mazao ya Uvuvi:** Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa mkopo wa shilingi milioni 323.8 kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa vyama viwili (2) vya ushirika, kampuni saba (7) za ukuzaji viumbe maji pamoja na kutolewa kwa injini za boti tano (5) kwa vyama vitano (5) vya ushirika; kuanzishwa vituo vya ubora na uthibiti

wa mazao ya uvuvi vya Singida, Kisesya na Murusagamba; kutolewa kwa vitendea kazi vya uchunguzi wa sampuli katika maabara ya samaki ya Nyegezi (Mwanza) na maabara ya viuatilifu ya Dar es Salaam ambapo sampuli 2,848 za minofu ya samaki, dagaa, maji na udongo zilichunguzwa ili kubaini uwepo wa vimelea, kemikali na madini tembo.

**(iv)** **Ujenzi wa miundombinu ya Uvuvi (Mialo na Masoko):** Hatua iliyofikiwa ni kuimarishwa kwa mialo 13 ya kupokelea samaki na kuwa ya kisasa katika Ukanda wa Ziwa Victoria **6**, Ukanda wa Ziwa Tanganyika minne (4); katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi mitatu (**3**); kuimarishwa kwa soko la feri, Soko la Samaki la Kasenda, Chato (Geita); kukamilika kwa ujenzi wa Soko la Samaki Nyakaliro, Sengerema (Mwanza); na kuwekwa kwa mizani katika Soko la Kimataifa Kirumba (Mwanza).

**(v)** **Uvuvi wa Bahari Kuu:** Kuendelea na juhudi za kufufua Shirika la Uvuvi la Taifa (TAFICO) ambapo uandaaji wa Mpango Biashara (*Business Plan*) umekamilika; kupatikana kwa ufadhili kutoka Serikali ya Japan kupitia Programu ya Maendeleo ya Uchumi na Jamii wenye thamani ya kiasi cha shillingi bilioni 4.2 ambapo sehemu ya fedha hizo zitatumika katika ujenzi wa meli yenye urefu wa mita 22 itakayovua katika maji ya Kitaifa na usimikaji wa mtambo wa kuzalisha barafu na ujenzi wa ghala la baridi la kuhifadhia samaki *(cold room).*

**(vi)** **Uzalishaji wa Mazao ya Uvuvi kwenye Maji ya Asili**

(a) Kuongezeka kwa uzalishaji/uvunaji wa samaki katika maji ya asili kutoka tani 362,645 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.48 mwaka 2015/16 hadi tani 497,567 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 2.34 mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la asilimia 37.2; kuongezeka kwa usindikaji wa minofu ya samaki aina ya Sangara kutoka tani 23,000.58 mwaka 2015/16 hadi tani 27,596.27 mwaka 2019/20; kuongezeka kwa huduma za usafirishaji wa mazao ya uvuvi kwenda masoko ya Ulaya ambapo katika mwaka 2019/20, jumla ya kilo 777,750.0 za mabondo zilisafirishwa; na

(b) Kuongezeka kwa mauzo ya samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi kutoka mauzo yenye thamani ya shilingi bilioni 379.25 mwaka 2015/16 hadi shilingi bilioni 506.24 mwaka 2019/20.

**3.3.2.5 Maliasili na Utalii**

(i) Kuongeza mapato yatokanayo na utalii kutoka Dola za Marekani milioni 1,901.95 mwaka 2015 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 2,612.99 mwishoni mwa mwaka 2019;

(ii) Kuanzisha na kupandisha hadhi maeneo ya wanyamapori kutoka Hifadhi za Taifa 16 mwaka 2015 hadi kufikia Hifadhi 22 mwaka 2020;

(iii) Kuimarisha ulinzi wa rasilimali zetu kwa kubadili mfumo wa usimamizi kutoka ule wa kiraia kwenda wa Kijeshi (Jeshi Usu). Katika kutekeleza hilo tayari Wizara imetoa mafunzo ya utayari kwa watumishi 4,556 kutoka taasisi za TANAPA, NCAA, TAWA na TFS;

(iv) Kufuta mapori tengefu 12 yenye ukubwa wa ekari 707,660 na misitu ya hifadhi saba (7) yenye ukubwa wa hekta 46,715 yaliyopungukiwa sifa kama njia mojawapo ya utatuzi wa migogoro ili kuwawezesha wananchi waliokuwa na uhaba wa ardhi kutumia maeneo hayo kwa shughuli za maendeleo kama vile kilimo na mifugo;

(v) Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhifadhi mazingira kwa kupanda takriban miti milioni 40 ikiwemo miti 2,960,000 iliyopandwa katika Jiji la Dodoma kupitia Kampeni ya Dodoma ya Kijani;

(vi) Kuhifadhi maeneo mbalimbali ya malikale ikiwa ni pamoja na kukarabati miundombinu ya vituo saba (7) vya mambo ya kale katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Lindi;

(vii) Wizara imeandaa na kuzindua Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Migongano baina ya Wanyamapori na Binadamu wa mwaka 2020 – 2024. Mkakati huo unalenga kuweka njia bora na endelevu za kukabiliana na migongano baina ya binadamu na wanyamapori.

(viii) Kuendelea kutumia mfumo wa Serikali wa minada ya kielektroniki (electronic tendering) katika kugawa vitalu vya uwindaji na uvunaji wa mazao ya wanyamapori ambao umewezesha kuongeza uwazi na kuondoa mianya ya rushwa;

(ix) Kuendelea kutekeleza Mradi wa REGROW ili kuimarisha utalii katika mikoa ya kusini;

(x) Programu ya Misitu na Uendelezaji wa Mnyororo wa Thamani ya Mazao ya Misitu (FORVAC): Kazi zilizotekelezwa ni kuandaliwa kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji 25; kuanzishwa kwa misitu yenye ukubwa wa hekta 32,245 katika vijiji 32; kuandaliwa kwa mwongozo wa kuandaa mpango wa usimamizi wa misitu ya Asili Tanzania; kuandaliwa kwa mtaala wa kuongeza thamani mazao ya misitu, mifumo ya masoko na kuendeleza biashara utakaotumika

katika vyuo vya Mafunzo ya Misitu; na kuanzishwa kwa mfumo wa Taarifa na tovuti ya Programu ya FORVAC. Kazi nyingine zilizofanyika ni kuunda na kujenga uwezo wa Kamati za Hifadhi ya mazingira za vijiji 12; kuunda na kutoa mafunzo kwa vikundi 10 vya ujasiriamali vyenye jumla ya wanachama 520; na kugawa miche 230,000 ya mitiki katika vijiji vinne (4) vya Wilaya ya Nyasa kwa lengo la kupandwa kwenye mashamba ya wananchi.

**3.3.2.6 Madini**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupitia na kutunga Sheria, Sera na mikataba ya madini; kuanzishwa kwa Kampuni mpya ya Twiga Minerals Corporation inayomilikiwa kwa ubia kati ya Tanzania (hisa asilimia 16) na Kampuni ya Barrick (hisa asilimia 84) ambapo imetoa gawio la shilingi bilioni 100; kusainiwa kwa mkataba wa ubia wa kampuni ya LZ NICKEL na Serikali ya Tanzania kwa ajili ya kuendeleza na kuchimba madini ya Nickel ambapo chini ya mkataba huo imeundwa kampuni ya ubia ya Tembo Nickel Corporation Limited (kwa umuliki wa hisa 84 asilimia kwa Kampuni ya LZ Nickel na Serikali ya Tanzania Hisa 16 asilimia); kujengwa kwa masoko 39 ya madini na vituo 41 vya kuuzia madini; kukamilika kwa ujenzi wa vituo vinne (4) vya umahiri katika maeneo ya Bariadi, Musoma, Bukoba na Handeni na kuendelea na ujenzi wa vituo vya Songea, Mpanda na Chunya; kuimarishwa kwa ulinzi wa rasilimali za madini kwa kujenga ukuta wa Mirerani (km 24) na kufungwa kwa mitambo ya CCTV Camera; na kukamilisha ujenzi wa Vituo Vitatu (3) vya Mfano vya uchenjuaji wa madini ya dhahabu kwa ajili ya wachimbaji wadogo katika maeneo ya Lwamgasa (Geita), Katente (Bukombe) na Itumbi (Chunya). Jitihada hizi zimechangia Sekta ya Madini kukua kwa wastani wa asilimia 8.0 kati ya mwaka 2016 na 2019; mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa kufikia asilimia 5.2 mwaka 2019/20 kutoka asilimia 4.6 mwaka 2015/16 na kuimarika kwa utolewaji wa ushuru wa huduma na huduma kwa jamii zinazozunguka migodi. Aidha, mapato ya fedha za kigeni kutokana na mauzo ya madini yaliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 1,912 (sawa na shilingi bilioni 4,464.71) mwaka 2015/16 hadi dola za Marekani milioni 2,898.8 (sawa na shilingi bilioni 6,769.0) mwaka 2019/20; na maduhuli kutoka shilingi bilioni 196 mwaka 2015/16 hadi kufikia shilingi bilioni 528.3 mwaka 2019/20.

**3.3.2.7 Biashara na Masoko**

**(a) Biashara**

Kazi zilizotekelezwa ni: kutoa leseni za biashara (Kundi A na B) kwa njia ya kielektroniki, kuanzishwa kwa vituo nane (8) vya kutolea huduma za pamoja

mipakani; kukamilisha baadhi ya majadiliano na kuendeleza majadiliano ya kibiashara kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa ili kupata na kutumia fursa za masoko; kuimarisha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji kupitia utekelezaji wa *Blueprint*; kuimarisha udhibiti wa bidhaa na huduma nchini; kuunganisha wakulima na fursa za masoko; kutoa taarifa za masoko ya mazao ya chakula, biashara na bidhaa mbalimbali; kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya masoko; na ujenzi wa jengo la maabara ya kisasa – Dar es Salaam *(TBS Test House).*

**(b) Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania - TANTRADE**

Kazi zilizotekelezwa ni: kuratibu mkutano wa wadau wa zao la embe nchini kwa lengo la kujadiliana mikakati mbalimbali juu ya kuanzishwa kwa Mradi wa Ghala la Kuhifadhia Embe *(Pack House)* katika Wilaya ya Mkuranga; kuratibu maonesho ya 44 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) kwa lengo la kuwapatia fursa wadau wa biashara kutangaza na kuuza bidhaa na huduma mbalimbali zinazozalishwa ndani na nje ya nchi ambapo kampuni 43 kutoka nchi tano (5) zilishiriki, jumla ya kampuni 2,837 za ndani kupata fursa ya kutangaza na kuuza bidhaa na huduma mbalimbali zinazozalishwa nchini, jumla ya watembeleaji 60,000 walipata huduma ya vitambulisho vya Taifa, 109 leseni za biashara, 7 vitambulisho vya wajasiriamali wadogo, 7 leseni za vileo, 62 ada ya huduma *(Service Levy)* na 3 walilipia ada ya huduma *(Hotel & Guest levy )*; 2,050 kupata huduma za afya, 1,700 kupata huduma za kibenki na zaidi ya watu 1,524 kupata huduma za ATM; kuzalishwa kwa ajira za muda zipatazo 15,912; kutangaza fursa za mazao 9 ya korosho, kahawa, pareto, mkonge, pamba, tumbaku, nafaka, chai na sukari kupitia banda maalum.

**(c) Masoko**

Kazi zilizotekelezwa ni: kufanyika kwa tafiti za kutambua fursa za masoko ili kuongeza mauzo ya bidhaa za Tanzania katika masoko ya nje ambapo kipaumbele kimetolewa kwa masoko ya China – (madini, vito, nyama, tumbaku, korosho na muhogo), India – (mikunde, korosho, ngozi na nafaka), Ulaya – (mbogamboga na matunda, asali, kahawa na korosho), nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - (nafaka, bidhaa za ujenzi, bidhaa za ngozi na bidhaa za viwandani, vyakula vya mifugo); nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - (Madini, nafaka, bidhaa za viwandani, bidhaa za ujnzi); kukamilika kwa Mwongozo wa Kuuza Bidhaa Nje ya Nchi; kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi ikijumuisha wanachama wa Umoja wa Wazalishaji wa Mafuta ya Alizeti (TASUPA) katika maonesho ya bidhaa za mafuta ya alizeti Mjini Nampula - Msumbiji; na kuratibu na kusimamia Maonesho ya Wiki ya Viwanda ya SADC katika Jiji la Dar es Salaam ambapo wafanyabiashara 574 walishiriki.

**(d) Kuchochea Uongezaji Thamani wa Bidhaa za Kilimo na Kuimarisha Miundombinu ya Masoko**

Kazi zilizofanyika ni: kubuni teknolojia rafiki mbalimbali ambazo zitatumika katika kuongeza thamani ya mazao ya kimkakati ya korosho, chikichi, mkonge, zabibu na miwa kwa ajili ya kutengeneza sukari, mbegu za mafuta hususan alizeti na karanga na mazao ya ngozi; kuingiza jumla ya mazao 10 katika mfumo wa stakabadhi za ghala ambayo ni mbaazi, dengu, soya, mpunga, ufuta, kakao, kahawa, alizeti, korosho, na mahindi ambapo mazao yaliyouzwa kupitia mfumo huo ni ufuta tani 5,926.726, mbaazi tani 775.543, dengu tani 80.804, soya tani 2,892.004, kahawa tani 1,406.205, kakao tani 6,603.240 na tani 187,273.252 zimeuzwa; kusajiliwa kwa maghala 21 na kupewa leseni ya kushiriki katika Mfumo wa Stakabadhi ghalani kwa zao la korosho; kutolewa kwa leseni 55 kwa waendeshaji wa ghala katika sekta ndogo ambapo mgawanyo wa wa leseni kwa mazao ni pamoja na korosho (34), Kahawa (5), Ufuta (6), Kakao (2), Soya (4), Mbaazi (2), Dengu (1) na Mpunga (1); kutoa mafunzo ya mfumo wa stakabadhi za ghala kwa jumla ya wakulima na viongozi wa AMCOS 3,000 wa zao la Kahawa Mkoani Kagera na kupewa ushauri wa namna mbalimbali ya kuwezesha kuboresha kilimo chao kuwa chenye tija zaidi; kuandaliwa kwa miongozo minne (4) mipya ambayo ni Mwongozo Namba 10 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika zao la Soya Toleo Namba 1, Mwongozo Namba 11 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala zao la Dengu Toleo Namba 1, Mwongozo Namba 15 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala zao la Mbaazi Toleo Namba 1 na Mwongozo Namba 16 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala zao la Pamba Toleo Namba 1.

### 3.3.3 Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu

#### 3.3.3.1 Elimu

**(a) Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo – EP4R)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa na kusambazwa kwa magari 39 katika vyuo vya ualimu 35; kuendelea na ujenzi wa ofisi mpya 55 za Wathibiti Ubora wa Shule ili kuimarisha mazingira ya utendaji kazi; kuendelea na ujenzi wa Sekondari ya Iyumbu – Dodoma; kukarabatiwa kwa vyuo vya ualimu 26 na kujenga upya chuo kimoja (1); na kukamilika kwa ujenzi wa ofisi mpya 100 za Uthibiti Ubora wa Shule za wilaya.

**(b) Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu ya Msingi (MMEM) – Kuimarisha Mafunzo ya Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuhuishwa kwa Mwongozo wa Mafunzo ya Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto kwa Walimu wa Shule za Msingi, Sekondari na Wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu; na ufuatiliaji wa programu za Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi hususan programu ya Elimu Changamani kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi katika halmashauri za Makete, Tabora, Njombe, Ludewa, Kasulu, Kakonko, Momba, Kibondo na Urambo.

**(c) Elimumsingi Bila Ada**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada ambapo Serikali imetoa ruzuku kwa ajili ya chakula cha wanafunzi wa bweni na kutwa kwa shule za msingi, fidia ya ada kwa wanafunzi wa bweni na kutwa kwa shule za sekondari na posho ya madaraka kwa walimu wakuu, wakuu wa shule na Maafisa Elimu Kata.

**(d) Mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni – SWASH**

Hatua iliyofikiwa ni: Kujengwa kwa vyoo vyenye matundu 9,712 (wasichana matundu 5,539, wavulana matundu 3,645 na walimu matundu 528), miundombinu ya maji, matanki ya maji 911 na miundombinu ya kunawia mikono katika shule za Msingi 602; na kufanyika kwa uhakiki na ufuatiliaji wa huduma ya maji, elimu ya afya, usafi wa mazingira shuleni, miundombinu ya vyoo na maji kwa kuzingatia mwongozo wa SWASH.

**(e) Mamlaka ya Elimu Tanzania - TEA**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza ujenzi wa vyumba vya madarasa 81 (madarasa matatu (3) kwa kila shule) katika shule 23 za msingi na shule nne (4) za sekondari zenye uhitaji mkubwa; kuendelea na ujenzi wa vyumba vya madarasa 81 (madarasa matatu (3) kwa kila shule) katika shule za msingi 22 na shule za sekondari tano (5); kujengwa kwa mabweni 16 ya wasichana katika shule 16 za sekondari (kidato cha 5 na 6) zilizo katika mazingira hatarishi; kuendelea na ujenzi wa nyumba 40 za walimu (nyumba 4 kwa kila shule) katika shule za sekondari 10; kujengwa kwa mabweni matatu (3) katika shule 3 za msingi na ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa na chumba maalum (*Audiology room*); na kuendelea na ujenzi wa matundu ya vyoo 528 (matundu 24 kwa kila shule) katika shule za msingi 18 na shule za sekondari nne (4) zenye uhitaji mkubwa.

**(f) Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la ghorofa nne (4) kwa ajili ya madarasa, maabara na ofisi za walimu katika Chuo cha Ufundi Arusha na ujenzi wa mabweni mawili (2) katika Chuo cha Walimu wa Ufundi Stadi cha Morogoro yapo kwenye hatua ya kuezekwa.

**(g) Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na upanuzi wa miundombinu katika vyuo vitano (5) vya ualimu vya Mpwapwa, Kleruu, Marangu, Tabora na Dakawa; na kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi katika Chuo cha Ualimu Mpuguso kwa kujenga majengo mawili (2) ya ghorofa yenye vyumba 16 vya madarasa, maktaba, jengo la mihadhara, maabara yenye vyumba viwili na ukarabati wa mabweni ambapo ujenzi upo katika hatua za ukamilishaji.

**(h) Kuendeleza Elimu ya Ualimu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kudahiliwa kwa wanachuo 9,346 wa mwaka wa kwanza na kufanya jumla ya wanachuo kuwa 17,509 katika vyuo 35 vya ualimu vya Serikali; kuendelea kugharamia chakula na malazi kwa wanachuo wote katika vyuo vya Serikali 35; kutolewa kwa mafunzo kazini ya TEHAMA na teknolojia saidizi kwa walimu 530 kutoka katika vyuo 17 vya ualimu; kununuliwa na kusambazwa katika vyuo vya ualimu vya Serikali machapisho 449 ya vitabu yenye jumla ya nakala 25,709 kwa ajili ya masomo yote yanayofundishwa vyuoni; na kutolewa kwa mafunzo kazini kwa walimu 771 katika halmashauri 20 zenye ufaulu wa chini katika somo la hisabati kwa lengo la kuwapa walimu mbinu na njia fanisi katika kufundishia na kujifunzia.

**(i) Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuongezeka kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kutoka wanafunzi 125,126 mwaka 2015 hadi kufikia 132,392 mwaka 2020. Mikopo iliyotolewa ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 450 sawa na asilimia 100 ya fedha iliyoidhinishwa kwa mwaka 2019/20; na kuendelea na ukusanyaji wa mikopo iliyoiva ambapo kiasi cha shilingi bilioni 191.7 zimekusanywa kati ya lengo la shilingi bilioni 221.5 la mwaka 2019/20, sawa na asilimia 87. Aidha, waajiri 2,406 nchi nzima wamekaguliwa na kuwezesha kutambuliwa kwa wanufaika wapya 14,731 wenye mikopo iliyoiva yenye thamani ya shilingi bilioni 100.7 ambapo kati yao wanufaika 13,969 (asilimia 94) wameanza kulipa.

**(j) Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,209 kwa wakati mmoja na ofisi 14 zenye uwezo wa kuhudumia wahadhiri 28; kuboresha maktaba ya Chuo kwa kununua vitabu, kufunga mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa maktaba na mfumo wa CCTV kwa ajili ya kuboresha ulinzi na usalama; na kuendelea na ujenzi wa maabara za sayansi zenye uwezo wa kuhudumia jumla ya wanafunzi 240 kwa wakati mmoja.

**(k) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma katika Hosteli za Dkt. J.P. Magufuli ambapo jengo hilo linahusisha maduka, mashine za kutolea fedha (*ATM),* saluni, huduma za udobi kwa kutumia mashine *(dry cleaner),* zahanati, mgahawa na *supermarket;* na kuendelea na ukarabati wa mabweni namba 2 na 5 yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 788 na hivyo kuongeza idadi ya wanafunzi wanaopata huduma ya malazi na kufikia jumla ya wanafunzi 11,103 katika Kampasi ya Mwl. J.K. Nyerere.

**(l) Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la utawala kwa lengo la kuboresha mazingira ya utendaji kazi; kununuliwa kwa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum; na kufanyika kwa tafiti 14 za sayansi na teknolojia zenye lengo la kutatua changamoto za kijamii.

**(m) Ukarabati na Ujenzi wa Chuo Kikuu Mzumbe**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati na uwekaji samani katika majengo ya Kampasi ya Tegeta - Dar es Salaam kwa awamu ya kwanza na ya pili; kukamilika kwa ukarabati wa hosteli mbili (2) katika Kampasi ya Mbeya pamoja na hosteli tatu (3) na nyumba 10 za watumishi katika Kampasi Kuu; na kuendelea na ujenzi wa madarasa katika Kampasi Kuu ambapo ujenzi umefikia asilimia 54.

**(n) Ujenzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Ardhi**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa bweni lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 592 kwa wakati mmoja.

**(o) Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa mabweni tisa (9) ambapo mabweni sita (6) yapo katika Kampasi Kuu ya Moshi na matatu (3) katika kituo cha kufundishia Kizumbi - Shinyanga; kukamilika kwa ujenzi wa bwalo la

chakula lenye uwezo wa kuchukua watu 100 kwa wakati mmoja; na kujengwa kwa ukuta wenye urefu wa mita 200 ili kuimarisha usalama wa wanafunzi na mali za chuo.

**(p) Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Kituo cha Umahiri wa Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu ambapo kazi ya ujenzi wa mihimili ya jengo na uwekaji wa dari katika chumba cha mikutano zimekamilika na uwekaji wa umeme na mifumo ya mtandao unaendelea; na kuendelea na maboresho katika shule ya tiba ya mfumo wa meno hususan chumba cha kutolea huduma binafsi na kuendelea na mchakato wa kupatikana kwa vifaa tiba.

**(q) Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaaam – DIT**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upanuzi wa jengo la maktaba pamoja na kuweka samani na miundombinu ya TEHAMA katika Kampasi Kuu ya Dar es Salaam na hivyo kuongeza uwezo wa maktaba kuhudumia wanafunzi 450 kutoka wanafunzi 150 kwa wakati mmoja; ukarabati wa miundombinu ya maabara ya Kampasi ya Mwanza pamoja na ununuzi wa mashine ya kuchakata na kutengeneza bidhaa za ngozi; ujenzi wa jengo la maabara ya kompyuta, darasa na bwalo la chakula katika Kampasi ya Myunga - Songwe; na kukamilika kwa miradi saba (7) ya tafiti za kijamii ambayo inajumuisha: Kutengeneza mtambo maalumu wa kuwezesha mazingira rafiki ya kilimo mjini; kukamilisha utengenezaji wa mfumo wa kilimo cha umwagiliaji unaotumia nguvu za jua kwa kutumia maji ya kisima; na kutengeneza mfumo wa kuhifadhi, kusambaza na kuchakata taarifa za baioanuai nchini.

**(r) Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika na kuanza kutumika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja; kufungwa kwa taa 20 za kisasa za ulinzi na usalama zinazotumia nishati ya jua kuzunguka eneo la chuo, kampasi ya Mbeya; kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa madarasa mawili (2) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 800 kwa wakati mmoja; kukarabatiwa kwa ofisi 80 zilizo chini ya majengo ya chuo *(basement offices)* ambazo zitaongeza nafasi za ofisi kwa wafanyakazi 320; na kuboresha mazingira ya wanafunzi ya kujifunzia kwa kufungwa kwa viti visivyohamishika katika madarasa matano (5).

**(s) Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine – SUA**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa asilimia 75 ya ujenzi wa jengo la maabara nane (8) lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,400 kwa wakati mmoja; kukamilika kwa ujenzi wa jengo la utafiti wa wanyama na wadudu (*Animal House)*; kukarabatiwa kwa madarasa pamoja na jengo la kuhifadhia nyasi kwa lengo la kuongeza nafasi za kufundishia na kujifunzia; na kuendelea na ukarabati wa karakana za uhandisi kilimo ambayo itatoa fursa kwa wanafunzi kufanya mafunzo kwa vitendo.

**(t) Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuboreshwa kwa mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kutekeleza awamu ya pili ya ukarabati na upanuzi wa vyuo 20 vya maendeleo ya wananchi; na kuwezeshwa kwa vijana 2,534 kupata mafunzo ya uanagenzi na utarajali katika taasisi mbalimbali kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi, SUGECO, *Marine Fisheries*, USA RIVER *Agrotech*, VETA Kagera, MoCU na *Bakhresa Food and Packaging* ili kuwajengea uwezo.

**3.3.3.2 Afya**

**(a) Hospitali ya Taifa ya Muhimbili**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea kutoa huduma za kupandikiza uloto (bone marrow transplant) na kukamilika kwa ujenzi wa jengo la wodi namba 18 ya Sewa Haji pamoja na ujenzi wa wodi za kulaza wagonjwa binafsi.

**(b) Ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda**

Shughuli zilizotekelezwa ni:

**(i)** **Hospitali ya Kanda ya Burigi (Chato):** Ujenzi wa jengo la huduma kwa wagonjwa wa nje, jengo la uchunguzi kwa njia ya maabara, jengo la huduma za dharura (EMD), jengo la huduma za uangalizi maalumu (ICU), jengo la upasuaji (Theatre), jengo la famasia, uzio na kazi za nje pamoja na njia za kuunganisha majengo ambapo kwa ujumla utekelezaji wa awamu ya kwanza umefikia asilimia 98; ujenzi wa *power house*, kisima cha maji na jengo la nyumba ya walinzi umefikia asilimia 32; na ujenzi wa barabara za ndani ya hospitali umefikia asilimia 15;

**(ii)** **Ujenzi wa Hospitali Mpya ya Kanda ya Kusini – Mtwara:** kuendelea na ujenzi wa jengo la mwanzo la hospitali lenye huduma za wagonjwa wa nje, uchunguzi, upasuaji na wagonjwa wa ndani ambalo lipo katika hatua za umaliziaji; na kuendelea na ujenzi wa jengo la genereta, ujenzi wa tenki la maji, ufungaji wa mifumo mbalimbali ndani na nje ya jengo na kazi za nje

ambapo kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 86; na kukamilika kwa upauaji wa boma;

**(iii) Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya:** kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa sita (6) la afya ya uzazi ambapo ujenzi umefikia asilimia 72;

**(iv) Hospitali ya Kanda ya Kaskazini (KCMC):** kukamilika kwa ujenzi wa wodi ya wagonjwa wa saratani; kuendelea na ujenzi wa vyumba vya upasuaji ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80; kununuliwa kwa kinu cha kufua hewa ya Oksijeni chenye uwezo wa kufua mitungi 400, kufungwa kwa mtambo mpya wa MRI, CT – Scan na X – ray; ujenzi wa jengo la kutengeneza dawa katika idara ya ngozi umefikia asilimia 97; na kuanza kwa ujenzi wa upanuzi wa jengo la huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo (dialysis); na

**(v) Hospitali ya Rufaa Kanda ya Ziwa, Bugando:** Kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa majengo ya kliniki ya wagonjwa wa nje, jengo la kutolea tiba ya Saratani na jengo la kliniki ya wanachama wa Bima ya Afya; kukamilika kwa ukarabati wa chumba cha mashine ya MRI na wodi ya wagonjwa wa kifua kikuu sugu; kukamilika kwa ujenzi wa maabara ya kisasa ya uchunguzi wa magonjwa kupitia Vinasaba; kununuliwa kwa *CT – Scan*, *Ultrasound 12*, mashine za *Radiotherapy*, *Digital X-ray*, mtambo wa kusafishia Damu (dialysis) na mashine ya tiba ya mionzi (Brachytherapy).

**(c) Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**

Hatua iliyofikiwa ni kununuliwa kwa mashine tatu (3) za AngioSuite/C-arm, Mobile C-ARM moja (1) ya *routine Orthopedic and general application*, Digital X-Ray moja (1), Mobile X-Ray moja (1) na MRI tatu (3) ambapo vifaa vyote vinatumika kutoa huduma za kibingwa hospitalini.

**(d) Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)**

Hatua iliyofikiwa ni: kununuliwa kwa mashine za X-ray, X-ray mobile, CR na Ultrasound mbili (2); kununuliwa na kufungwa kwa mtambo maalumu wa kisasa wa Cathlab kwa ajili ya tiba za mfumo wa umeme wa moyo.

**(e) Hospitali ya Taifa Muhimbili – Mloganzila**

Shughuli zilizofanyika ni: kudhamini watumishi 55 katika fani mbalimbali za kibingwa katika masomo ya uzamili ndani na nje ya nchi; upandikizaji wa vifaa vya usikivu (cochlear implants) kwa wagonjwa watatu (3) na hivyo kupunguza rufaa za nje ya nchi; na kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwemo huduma za kuhifadhi maiti.

**(f) Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI)**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Ununuzi wa mashine ya *Positron Emmission Tomography* (PET Scan); kununuliwa kwa dawa za kutibu saratani ambazo zimesaidia kupunguza rufaa nje ya nchi, mashine za kuchunguza matokeo ya tiba saratani kwa njia ya damu (tumor markers), majokofu manne (4) kwa ajili ya maabara na mashine za *Oxygen Concentrators* tisa (9) kwa ajili ya wagonjwa wanaolazwa wenye uhitaji maalumu wa hewa ya oxygen; kufungwa kwa mashine yenye uwezo mkubwa wa vipimo vya kikemia na X-ray ya upimaji wa matiti (Mammography); na kupata mashine ya kupima virusi mbalimbali hususan vinavyosababisha saratani (PCR Machine).

**(g) Hospitali ya Rufaa ya Magonjwa ya Kifua Kikuu – Kibong'oto (Kilimanjaro)**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kununuliwa kwa mashine za *Digital X-Ray* na *Ultrasound*, vifaa vya maabara na mashine za uchunguzi wa kifua kikuu kwa kuotesha vimelea *BACTEC 960* (Mycobacteria Growth Indicator Tube - MGIT) na *Blood Culture Machine*.

**(h) Mradi wa Kuboresha Hospitali za Rufaa za Mikoa**

Shughuli zilizotekelezwa ni:

(i) **Hospitali ya Rufaa Dodoma:** Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za dharura na ukarabati wa jengo la X-ray; na ukarabati wa jengo la upasuaji umefikia asilimia 90.

(ii) **Hospitali ya Rufaa Mawenzi - Kilimanjaro**: Ujenzi wa jengo la huduma za dharura na jengo la mama na mtoto umefikia asilimia 45.

(iii) **Hospitali ya Rufaa Mwananyamala – Dar es Salaam:** Ujenzi wa jengo la mama na mtoto umefikia asilimia 98.

(iv) **Hospitali ya Rufaa Sekou Toure - Mwanza**: Ujenzi wa jengo la ghorofa sita (6) la huduma za afya ya uzazi na mtoto umefikia asilimia 49.

(v) **Hospitali ya Rufaa Njombe**: Kukamilika na kutumika kwa jengo la wagonjwa wa nje; ujenzi wa jengo la mama na mtoto umefikia asilimia 53; ujenzi wa jengo la maabara umefikia asilimia 73; ujenzi wa jengo la EMD na ICU umefikia asilimia 69; ujenzi wa jengo la upasuaji, mifupa na magonjwa ya ndani umefikia asilimia 55; ujenzi wa eneo la kuchomea taka umefikia asilimia 86; ujenzi wa nyumba 5 za watumishi umefikia asilimia 76; ujenzi wa jengo la kufulia umefikia asilimia 73; na ujenzi wa jengo la Damu Salama umefikia asilimia 50.

(vi) **Hospitali ya Rufaa Songwe**: Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la dharura; ujenzi wa jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD) umefikia asilimia 69; Ujenzi wa

Jengo la Maabara umefikia asilimia 59; na ujenzi wa jengo la wazazi (maternity) upo katika hatua ya kuchimba msingi.

(vii) **Hospitali ya Rufaa Simiyu:** kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za upasuaji, radiolojia na maabara na kufikia asilimia 50 ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto.

(viii) **Hospitali ya Rufaa Geita:** Ujenzi wa majengo ya huduma za wagonjwa wa nje, radiolojia na upasuaji, jengo la kufulia na jengo la mgahawa umefikia zaidi ya asilimia 90.

(ix) **Hospitali ya Rufaa Katavi:** Kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa moja lenye pande mbili (Wing "A" na "B") linalojumuisha huduma za Wazazi, dharura, wagonjwa wa nje, famasia, radiolojia, upasuaji na wagonjwa mahututi ambapo ujenzi wa msingi, nguzo za ghorofa ya chini na ujenzi wa kuta kwa sakafu ya kwanza umekamilika.

(x) **Hospitali ya Rufaa Mara (Kwangwa):** Ujenzi wa jengo moja lenye vitalu vitatu (Blocks) A, B na C zilizoungana (Semidetached Blocks) umekamilika na kuanza kutumika; kukamilika kwa uwekaji wa mifumo ya maji na Gesi Tiba awamu ya kwanza (first fix); kukamilika kwa ujenzi wa karakana, jengo la kufulia na jengo la kuhifadhi maiti; na kukamilika kwa ujenzi wa jengo la mashine ya kufua umeme (power house) na kichomea taka.

(xi) **Hospitali ya Rufaa Sumbawanga - Rukwa:** Ujenzi wa jengo la dharura umefikia asilimia 90.

**(i) Ujenzi wa Hospitali za Wilaya**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa hospitali za halmashauri 96, kati ya hizo hospitali 67 ujenzi umefikia asilimia 60 hadi 98 na hospitali za halmashauri 29 ujenzi umefikia asilimia 0.5 (kuchimba msingi na mitaro) hadi 44 (kupaua). Hospitali za halmashauri 56 kati ya 67 zimeanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje. Vile vile, hospitali ya Uhuru, Chamwino (Dodoma) imekamilika kwa asilimia 98.2 na kuanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje. Kwa ujumla Hospitali za Halmashauri za Wilaya zimeongezeka kutoka 77 mwaka 2015 hadi 179 mwaka 2020.

**(j) Huduma ya Afya ya Msingi (Vituo vya Afya)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kujengwa na kuboreshwa kwa vituo vya kutolea huduma za afya 1,786; na kununuliwa na kusambazwa kwa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika mikoa ya Shinyanga, Pwani, Mwanza, Simiyu, Tabora, Kagera, Geita, Kigoma na Mara na halmashauri 68 zinazotekeleza mradi.

**(k) Mapambano Dhidi ya VVU na UKIMWI**

Shughuli zilizotekelezwa ni ununuzi na usambazaji wa dawa za kufubaza makali ya

UKIMWI katika ngazi mbalimbali za utoaji wa huduma za afya nchini ambapo waathirika milioni 1.3 wamepatiwa dawa za kufubaza makali ya UKIMWI.

**(l) Udhibiti wa Kifua Kikuu na Ukoma**

Shughuli zilizotekelezwa ni ununuzi na usambazaji wa dawa za kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma pamoja na utekelezaji wa afua mbalimbali katika ngazi za utoaji wa huduma za afya.

**(m) Udhibiti Magonjwa ya Kuambukiza**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Asilimia 99 ya chanjo zilitolewa kwa watoto, wajawazito na wasichana. Chanjo hizo ni BCG, Tetanus Toxoid (TT), bOPV, Td, IPV, PCV, HPV, Pentavalent, Rota na Surua Rubella. Kununuliwa kwa magari 69 aina ya "Pick up"**,** malori matano (5) ya kusafirishia chanjo, majokofu 1,385, vishikwambi 1,249, vifaa vya kuangalia joto la majokofu 1,880 na jenereta moja (1) la kufua umeme na bidhaa nyingine za chanjo.

**(n) Udhibiti wa Malaria**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kugawa jumla ya vyandarua 6,563,880 vyenye dawa bila malipo kwa jamii, wajawazito na watoto wenye umri wa miezi tisa (9); kusambaza viuadudu (biolarvicides) katika halmashauri mbalimbali nchini ili kuangamiza viluwiluwi vya mazalia ya mbu; na kununuliwa kwa lita 96,000 za viuadudu vya kibailojia na kusambazwa katika mikoa 12 nchini.

**(o) Mfuko wa Pamoja wa Afya**

Hatua iliyofikiwa ni kuboreshwa kwa miundombinu ya vituo 5,479 vya kutolea huduma za afya, ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika mikoa 26 na halmashauri 184.

**(p) Mradi wa Kuboresha Upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa kwa dawa, vifaa tiba na vitendanishi na kusambazwa katika vituo vya umma vya kutolea huduma nchini ambapo upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma za afya umefikia asilimia 94; kusambazwa lita 239,020 za viuadudu vya kuangamiza viluwiluwi vya mbu katika maeneo ya mazalia katika halmashauri zote nchini; na kununuliwa mashine za X-ray 11 za kidigitali ambazo zimesambazwa katika hospitali za mikoa 11.

#### 3.3.3.3 Ustawi wa Jamii

**(a) Ukarabati na Ujenzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii**

Shughuli zilizofanyika ni: Kukamilika kwa ukarabati wa choo chenye matundu manne (4), mabafu ya vyumba vinne (4), miundombinu ya umeme, mabweni mawili (2) ya wavulana katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii na Ufundi Misungwi, ukarabati wa nyumba nne (4) za watumishi, bweni moja (1) la wasichana, maktaba, choo kimoja chenye matundu tisa (9) na uzio katika vyoo vya wanawake katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli; na kukamilika kwa ujenzi wa bwalo la chakula katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi na ujenzi wa maktaba katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole.

**(b) Ujumuishaji wa Masuala ya Jinsia katika Mipango ya Maendeleo**

Shughuli zilizofanyika ni: Kutoa huduma ya mikopo yenye mashrti nafuu kupitia dirisha la wanawake la Posta yenye thamani ya shilingi bilioni 5.6 kwa wanawake 17,306 na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 63.49 imetolewa kwa wajasiriamali 938,802 kupitia asilimia 4 ya pato la halmashauri; kuanzishwa kwa SACCOS 130 za wanawake; kutoa mafunzo kuhusu urasimishaji na uboreshaji wa bidhaa kwa wanawake wajasiriamali 7,713; kushiriki kwa wanawake 13,566 katika Maonesho ya Biashara ya Kitaifa na Kimataifa yakiwemo maonesho ya Sabasaba, Juakali, Nanenane na VICOBA; kuanzisha madawati 427 ya jinsia na watoto katika vituo vya polisi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu Mzumbe, Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na vituo 153 katika Jeshi la Magereza; kuanzisha Dawati la Jinsia katika Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa ajili ya kupambana na vitendo vya rushwa ya ngono kupitia Kampeni ya "Vunja Ukimya"; kuanzishwa kwa vituo 13 vya Huduma ya Mkono kwa Mkono kwa ajili ya wahanga wa ukatili wa kijinsia katika mikoa (9) ya Dar es Salaam, Pwani, Mbeya, Mwanza, Iringa, Kilimanjaro, Arusha, Tabora na Shinyanga.

**(c) Uhai na Maendeleo ya Awali ya Mtoto**

Kazi zilizotekelezwa ni: Kufanyika kwa mafunzo ya uelewa kuhusu madhara ya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto kwa walimu 78, wanafunzi 790, viongozi wa kisiasa 23, viongozi wa dini 16, viongozi wa jadi na watangazaji wa redio kutoka redio za kijamii katika Mkoa wa Mara, Geita, Tanga, Rukwa, Mbeya na Kigoma; kuandaliwa kwa taarifa ya (*Convention on the Rights of the Child* - CRC); kufanyika kwa kampeni ya kutokomeza mimba za utotoni katika mikoa ya Shinyanga, Mara, Tabora, Singida, Rukwa, Tanga na Dodoma ambapo wanafunzi 8,978 wa shule ya msingi, wanafunzi 345 wa sekondari pamoja na walimu 40 walishiriki kampeni

hiyo; na kuandaliwa kwa taarifa ya mwaka 2019/20 ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto - MTAKUWWA.

**(d) Kuwezesha Huduma za Ustawi wa Jamii**

Kutolewa kwa mafunzo kwa maafisa ustawi wa jamii kuhusu utambuzi wa watu wa kuaminika katika halmashauri 40 ambayo yalilenga kuimarisha ulinzi na usalama kwa watoto walio katika mazingira hatarishi. Mafunzo hayo yaliwezesha kutambuliwa kwa watu wa kuaminika 295 na watoto 527 waliwekwa chini ya uangalizi wa watu wa kuaminika. Kuendelea kutoa mahitaji ya msingi (chakula, mavazi, malazi na huduma za afya) ambapo wazee 349 (wanaume 149 na wanawake 200) walipata huduma hizo katika makazi 13 ya wazee; kuendelea na ujenzi wa makazi mapya ya Taifa ya Watoto Kikombo – Dodoma pamoja na kuanzisha programu za kutengamanisha watoto.

### 3.3.3.4 Maji na Usafi wa Mazingira

**(a) Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji Nchini**

Kazi zilizotekelezwa ni: Kujengwa kwa vituo saba (7) vya kufuatilia mwenendo wa maji mitoni; kutolewa kwa leseni mpya 52 za uchimbaji visima na vibali 225 vya kuchimba visima vya maji katika maeneo mbalimbali nchini; kutolewa kwa vibali 793 vya matumizi ya maji; kuanzishwa kwa Jumuiya 23 za watumia maji; kufanyiwa utafiti maeneo 157 ya kuchimba visima; na kuendelea na ujenzi wa ofisi ya Maji ya Bonde la Wami - Ruvu ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60 na ukarabati wa ofisi ndogo ya Bonde la Maji Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90. Aidha, katika maandalizi ya ujenzi wa bwawa la Farkwa shughuli zilizotekelezwa ni ulipaji wa fidia kwa wananchi 2,612 kati ya 2,868 wanaostahili.

**(b) Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji na Usimamizi wa Mfumo wa Ikolojia**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukusanywa na kuhakikiwa kwa usalama wa sampuli 4,218 za maji kutoka katika mifumo ya kusambaza maji ya kunywa vijijini na mijini ambapo matokeo yalionesha sampuli 3,832 sawa na asilimia 90.8 zilikidhi viwango vinavyokubalika; na kutengenezwa na kusambazwa kwa mitambo 200 ya kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji katika maeneo ya Minjingu na Olasiti katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati ambapo imenufaisha wananchi wapatao 1,600 kwa kupata maji safi na salama.

**(c) Kuboresha Huduma za Maji Mijini na Vijijini**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa miradi 1,423 inayotoa huduma kwa wananchi wapatao milioni 24.5. Kukamilika kwa miradi hiyo kumewezesha huduma za maji

kwa wananchi waishio mijini kufikia asilimia 84 na vijijini kufikia asilimia 70.

**(d) Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa**

Kazi zilizotekelezwa ni: Kukamilika kwa mradi wa maji katika Mkoa wa Geita, Njombe na Songwe na kuendelea kwa ujenzi wa miradi ya maji katika mji wa Kigoma asilimia 90; kukamilika kwa mradi wa usambazaji wa maji katika Mji wa Serikali – Mtumba; na kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika majiji ya Mwanza na Arusha umefikia asilimia 76 na asilimia 62 mtawalia.

**(e) Mradi wa Maji Masasi – Nachingwea**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa chujio la Mbwinji ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80.

**(f) Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa mradi wa maji wa Same – Mwanga – Korogwe ambapo utekelezaji umefikia asilimia 65.

**(g) Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria – Igunga, Nzega na Tabora**

Hatua iliyofikiwa ni: Ujenzi wa mradi unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98.

**(h) Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria - Kahama - Shinyanga**

Kazi zilizotekelezwa ni: Kukamilika kwa mradi wa maji katika miji ya Isaka na Kagongwa ambapo wananchi wapatao 115,000 wamenufaika**;** kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji vya Mwakuzuka na Kabondo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 65 na kwa vijiji vya Nyang'homango, Isesa, Igenge na Mbarika umefikia asilimia 75; kukamilika kwa miradi ya maji katika vijiji vya Mwasekagi na Mwakatola; na kuendelea na upanuzi wa mtandao wa maji kwenda Kituo cha Afya Kishapu na Kijiji cha Mwakitolyo.

**(i) Kuboresha Huduma za Maji Jiji la Dar es Salaam (DAWASA)**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa zaidi ya asilimia 90 ya utekelezaji wa miradi katika eneo linalohudumiwa na DAWASA (mikoa ya Dar es Salaam na Pwani) ambao unahusisha maeneo ya Kibamba hadi Kisarawe, Mlandizi hadi Chalinze, Kisarawe-Pugu-Ukonga, Mbezi Luis, Kiluvya, Tegeta, Wazo, Madale, Mivumoni, Mabwepande na Bagamoyo (maeneo ya Vikawe, Zinga, Mapinga na Kerege).

**(j) Mradi wa Maji wa Mpera na Kimbiji**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa visima 19 kati ya 20 vilivyopangwa kuchimbwa katika eneo la Kimbiji na Mpera; na kuanza maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza huduma ya maji kwa wananchi kutoka katika visima vitano vya awali vya Kimbiji.

**(k) Ufuatiliaji na Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP-II)**

Kazi zilizofanyika ni pamoja na: kugharamia ufuatiliaji wa miradi katika mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Pwani, Morogoro, Dar es Salaam, Mtwara na Lindi; na kugharamia wataalamu washauri wanne (4) wanaotoa huduma katika usimamizi wa mradi katika maeneo ya fedha, ununuzi na ufuatiliaji.

**(l) Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa mradi wa Orkusemet kwa kutekeleza kazi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa chanzo cha maji, chujio la maji, ununuzi wa *control panel* na ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 10.2 ambapo hadi Septemba, 2020 utekelezaji ulikuwa umefikia wastani wa asilimia 86.

**3.3.3.5 Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**(a) Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la studio za televisheni Mikocheni Jijini Dar es Salaam ambapo ujenzi wa jengo la studio umekamilika na kazi ya ufungaji wa mitambo ya studio inaendelea; ujenzi wa jengo la kufunga mitambo ya kurushia matangazo ya redio kwa masafa ya FM katika eneo la mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere (Kisaki) umekamilika na mitambo inatarajiwa kuwasili nchini mwezi Februari 2021; na zoezi la malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi wa ujenzi wa Makao Makuu mapya ya TBC jijini Dodoma limekamilika ambapo hatua inayofuata ni umilikishwaji wa eneo hilo.

**(b) Habari kwa Umma**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kukusanywa kwa taarifa zinazohusu utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za Serikali kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi na kununua vifaa vya kukusanya, kuchakata na kutoa habari kwa wananchi.

**3.3.3.6 Ujuzi na Uwezeshaji**

**(i) Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini:** Katika awamu ya kwanza ya kutekeleza Program ya Kukuza Ujuzi nchini, miongozo ya kitaifa ya mafunzo kwa vitendo

mahala pa kazi imetengenezwa. Miongozo hiyo ni Mwongozo wa Kitaifa wa Mafunzo ya Uanagenzi *(National Apprenticeship Framework)* na Mwongozo wa Kitaifa wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahitimu wa Vyuo Mahala pa Kazi *(National Internship Framework)*. Vile vile katika kipindi cha mwaka 2017 hadi 2020, jumla ya vijana 65,008 wamenufaika kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini. Kati yao, vijana 28,941 wamepatiwa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kwa muda wa miezi sita hadi mwaka mmoja kwa dhamana ya Serikali kupitia mafunzo ya Uanagenzi katika fani za ujenzi, useremala, umeme wa majumbani na viwandani, umeme wa jua, ufundi magari, ufundi bomba, utengenezaji wa vifaa kwa kutumia aluminium, uchomeleaji na uungaji vyuma, kilimo na ufugaji, ushonaji, uchorongaji vipuli, uchapaji nyaraka na TEHAMA. Vijana 19,462 wamepewa mafunzo na kurasimishwa ujuzi walioupata nje ya mfumo usio rasmi wa mafunzo na kupatiwa vyeti ili wavitumie kutafuta ajira na kujiendeleza kiujuzi katika taasisi mbalimbali za mafunzo uashi, useremala, ushonaji, ufundi bomba, uchomeleaji na uungaji vyuma, ufundi magari, ufundi umeme, ukarabati wa bodi za magari, upishi na uhudumu katika hoteli. Aidha, wahitimu 5,975 kwa elimu ya juu na kati wamewezeshwa kupata mafunzo ya vitendo mahali pa kazi katika fani mbalimbali walizosomea na miongoni mwao wahitimu 1,800 wamepata ajira moja kwa moja katika taasisi zilizowapatia nafasi za mafunzo kutokana na uzoefu walioupata. Katika sekta ya kilimo, mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa vijana kupitia teknolojia ya kitalu nyumba yametolewa kwa vijana 8,980 kutoka katika Halmashauri 84 za Mikoa 12 ambayo ni Mikoa ya Lindi, Ruvuma, Dodoma, Manyara, Mwanza, Simiyu, Kagera, Shinyanga, Geita, Iringa, Mbeya na Kirimanjaro. Mafunzo ya kukuza ujuzi kwa wafanyakazi walioajiriwa na waliojiajiri *(skills upgrading/updating training)* yametolewa kwa wafanyakazi 1,550. Vile vile, vijana 100 wamegharamiwa na Serikali kuhudhuria mafunzo ya kilimo cha kisasa nchini Israel kwa kipindi cha mwaka mmoja.

**(ii) Kulinda Ajira za Wazawa:** Kupitia Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Na. 1 ya Mwaka 2015, ajira za wazawa zimeendelea kulindwa kwa kuhakikisha kuwa wageni wanaokuja kufanya kazi nchini wanakidhi vigezo vilivyoanishwa katika Sheria hiyo kwa maana ya kuwa na sifa stahiki za kielimu/taaluma, ujuzi na uzoefu wa kazi. Aidha, kupitia Sheria hii, usimamizi juu ya utekelezaji wa Mpango wa Urithishanaji Ujuzi kutoka kwa wageni kwenda kwa wafanyakazi wazawa unasimamiwa ipasavyo ili kuhakikisha wazawa wanarithi nafasi za wageni pindi muda wao wa kufanya kazi nchini utakapoisha.

#### 3.3.3.7 Hifadhi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

**(a) Mradi wa Kuhimili Athari ya Mabadiliko ya Tabia nchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kuanza maandalizi ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi kwenye vijiji 14 katika mikoa ya Morogoro (2), Manyara (4), Dodoma (4) na Shinyanga (4) vinavyotekeleza mradi; kukamilika kwa tathmini ya hali halisi ya ikolojia katika maeneo ya mradi; kuandaliwa kwa rasimu ya Mfumo wa Usimamizi wa Maarifa ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi; kufanyika kwa mafunzo kwa wataalamu na viongozi kuhusu namna ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia Mifumo ya Ikolojia; kuandaliwa kwa mkakati wa ufuatiliaji na tathmini; na kufanya mafunzo ya utengenezaji na matumizi ya majiko banifu katika vijiji vinavyotekeleza mradi yaliyotolewa katika Wilaya za Kishapu na Simanjiro na yanaendelea katika Wilaya ya Mpwapwa, Mvomero na Kaskazini A.

**(b) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi katika Kusimamia na Kupunguza Athari za Mazingira kwa Jamii za Vijijini katika Sehemu zenye Ukame**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa matenki mawili (2) ya mita za ujazo 50 na vituo 12 vya kuchotea maji (vituo vitatu (3) katika kijiji cha Kambi ya Simba na vituo tisa (9) katika kijiji cha Jipe Wilaya ya Mwanga - Kilimanjaro); kukamilika kwa ujenzi wa mfereji wa umwagiliaji wa mita 1,800, ujenzi wa uzio wa kuzuia mafuriko wa mita 450, na Ujenzi wa mageti matatu (3) ya kufungulia maji katika kijiji cha Mabilioni Wilaya ya Same - Kilimanjaro; kukamilika kwa taratibu za ununuzi wa mitambo miwili (2) ya hali ya hewa na kuainishwa kwa Maeneo ya kufunga Mitambo; na kukamilika kwa Taarifa ya Awali ya Utafiti *(Inception Report)* na kuwasilishwa kwa wadau ili kupata maoni yatakayomwezesha Mshauri Elekezi kufanya utafiti kwenye maeneo ya mradi.

**(c) Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Ardhi ya Bonde la Nyasa**

Shughuli zilizotekelezwa ni kufanyika kwa utafiti wa awali wa kuanzisha na kuimarisha jumuiya za watumia maji katika Bonde la Ziwa Nyasa katika Halmashauri za Wilaya ya Mbinga (vijiji 16) na Nyasa (vijiji 10).

**(d) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Upunguzaji wa Kemikali Zinazomong'onyoa Ukanda wa Ozoni**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kushiriki katika maadhimisho ya siku ya Ozoni Duniani kwa kutoa elimu kwa Umma kuhusu udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni; kukusanya na kuingiza takwimu za kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni nchini na kuwasilishwa Sekretarieti ya Itifaki;

kuwezesha Serikali kuridhia Marekebisho ya Kigali katika Itifaki ya Montreal kuhusu kupunguza matumizi ya kemikali aina ya *Hydrofluorocarbons* (HFCs); kutoa mafunzo kwa mafundi sanifu 20 kuhusu teknolojia mpya na njia sahihi za kuhudumia vifaa vya kupoza joto vinavyotumia kemikali zinazoharibu tabaka la ozoni; na kutoa mafunzo kwa maafisa forodha 31 na wasimamizi watano (5) wa sheria kutoka mamlaka za Serikali za udhibiti wa uingizaji wa kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal.

**(e) Mradi wa Kutekeleza Mpango wa Dunia wa Ufuatiliaji wa Taka Zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kuandaliwa kwa kanuni za usimamizi wa matumizi ya zebaki nchini; kukamilika kwa Mkakati wa Miaka Mitano 2020 - 2025 wa Usimamizi wa Kemikali na Taka Hatarishi nchini; kukamilika kwa Mfumo wa Kimtandao wa Upatikanaji wa Taarifa za Kemikali na Taka nchini; kukamilika kwa taarifa ya tathmini ya uwezo wa kitaasisi katika kusimamia kemikali na taka hatarishi nchini; kukamilika kwa Mpango Kazi wa mwaka 2020/21 wa utekelezaji wa mradi wa udhibiti wa kemikali na taka hatarishi; kukusanywa kwa sampuli za mafuta kwenye transfoma 553 zinazohisiwa kuwa na kemikali aina ya *Polychlorinated Biphenyls* (PCBs) na kupelekwa Afrika ya Kusini kwa uchunguzi wa kimaabara; kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara yatokanayo na kemikali ya PCBs; kutoa mafunzo mahsusi ya namna bora ya kudhibiti kemikali aina ya PCBs kwa wafanyakazi wa TANESCO katika mikoa ya Dodoma, Singida, Mwanza, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Pwani, Dar es Salaam na Morogoro; kuendelea na ukusanyaji wa sampuli za maji na udongo kwa mikoa ya Pwani na Singida ili kubaini kiwango cha kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu (*Persistent Organic Pollutants* – POPs); kuchukuliwa kwa sampuli 55 za maziwa ya mama wanaonyonyesha katika mikoa ya Mbeya, Pwani, Arusha, Mwanza na Dodoma na kupelekwa Ujerumani kwa uchunguzi ili kubaini kiwango cha kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu; na kuendelea kuchukua sampuli katika hewa na kupelekwa Uholanzi na Sweden kwa uchunguzi wa kimaabara ili kubaini kiwango cha kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu.

**3.3.3.8 Utawala Bora na Huduma kwa Wananchi**

**(a) Azma ya Serikali Kuhamia Dodoma**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na maandalizi ya awamu ya pili ya ujenzi wa majengo ya ofisi katika Mji wa Serikali Mtumba yatakayotosheleza watumishi wote. Katika mwaka 2019/20, Serikali imekamilisha usanifu wa majengo husika. Aidha, mradi wa ujenzi wa barabara (km 51.2) kwa kiwango cha lami katika Mji wa Serikali Mtumba utakaogharimu jumla ya shilingi bilioni 89.13 unaendelea.

**(b) Mfuko wa Mahakama**

Shughuli zilizotekelezwa kupitia Mfuko wa Mahakama ni kama ifuatavyo:

(i) **Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Wilaya**: Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa Mahakama za wilaya 15 ikiwemo Longido, Chato, Geita, Bukombe, Bariadi, Njombe, Ruangwa, Kilwa, Chunya, Kondoa, Kasulu na Makete; kukamilisha ujenzi wa mahakama za Chemba na Bahi; kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Wanging'ombe, Bunda, Sikonge, Kilindi, Rungwe na Ludewa; na kupata wakandarasi ili kuanza ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Same, Tandahimba, Mwanga, Ngara na Namtumbo. Aidha, ujenzi wa Mahakama tano (5) za Hakimu Mkazi zikiwemo Manyara, Simiyu, Njombe na Geita umekamilika na ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi za Katavi na Lindi unaendelea.

(ii) **Ujenzi na Upanuzi wa Jengo la Chuo cha Uongozi wa Mahakama - Lushoto (IJA)**: Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa awamu ya pili ya ujenzi wa bweni la wavulana Lushoto.

(iii) **Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Mwanzo:** Hatua iliyofikia ni kukamilika kwa mahakama za mwanzo 18 ikiwemo Mkunya (Newala), Magoma (Korogwe), Kibaigwa (Dodoma), Laela, Msanzi na Mtowisa (Sumbawanga), Mtae (Lushoto), Uyole (Mbeya), Mlowo (Songwe) na Ngerengere (Morogoro); na kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Mlimba na Mang'ula (Morogoro).

(iv) **Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama Kuu**: Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa majengo mawili (2) ya Mahakama Kuu katika mikoa ya Kigoma na Mara; na kukamilika kwa ukarabati wa Mahakama Kuu tatu (3).

(v) **Ujenzi na Ukarabati wa Majengo:** Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa nyumba tatu (3) za kufikia Majaji mkoani Mtwara; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba mbili (2) za makazi ya Majaji Kigoma na nyumba mbili (2) Musoma; na kukamilika kwa ujenzi wa nyumba mbili (2) za Mahakimu Loliondo - Arusha.

(vi) **Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama Dodoma**: Hatua iliyofikia ni kuendelea na ujenzi wa majengo ya mahakama kuu Dodoma.

(vii) **Mradi wa Uboreshaji wa Huduma za Mahakama "Citizen Centric Judiciary Modernisation Project":** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa: Mfumo wa Usimamizi wa Mashauri wa JSDS 2.0 Awamu ya Kwanza; Mfumo wa Usimamizi wa Mawakili; Mfumo wa Utambuzi wa Majengo na Takwimu Muhimu za Mahakama; Mfumo wa Kusikiliza Mashauri kwa Njia ya Video katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Mahakama Kuu Mbeya, Chuo

cha IJA - Lushoto, Mahakama Kuu Bukoba na Gereza la Keko - Dar es Salaam. Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni kuunganishwa kwa Mahakama 157 kwenye Mkongo wa Taifa wa mawasiliano na kupata huduma za mtandao kutoka TTCL; kuanzishwa kwa huduma za mahakama inayotembea Dar es Salaam na Mwanza; na ujenzi wa vituo sita (6) vya Haki Jumuishi katika mikoa ya Mwanza, Morogoro, Dar es Salaam, Arusha na Dodoma umefikia hatua ya kuezeka.

**(c) Kuimarisha Shughuli za Mfuko wa Bunge**

(i) **Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Bunge:** Shughuli zilizotekelezwa ni kukamilika kwa ujenzi wa ghorofa ya tano (5) katika jengo la utawala; ujenzi wa makazi ya viongozi wa Bunge, Dodoma ambapo nyumba ya Katibu wa Bunge imekamilika na nyumba ya Naibu Spika ipo katika hatua za awali; na ukarabati wa Ukumbi wa Bunge, Ukumbi wa Msekwa, Kumbi za vikao vya Kamati na ukarabati wa majengo ya Ofisi ya Bunge.

(ii) **Ujenzi wa miundombinu ya Bunge:** Shughuli zilizotekelezwa ni kununuliwa na kufungwa kwa mitambo ya usalama na vifaa vya kituo cha matangazo ya redio na runinga; na kuanzisha Bunge Mtandao (*e-Parliament*) na kuwezesha matumizi yake kwa kununua *Tablets* 460 na *Servers* 2;

(iii) **Mradi wa Kulijengea Bunge Uwezo Awamu ya Pili (LSP II):** Shughuli zilizotekelezwa ni kutolewa kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa Wabunge 393 na Watumishi kwenye maeneo ya uandaaji wa Miswada, Sheria, na Bajeti; kutolewa kwa mafunzo ya utafiti wa Kibunge na ujumuishwaji wa masuala ya jinsia katika shughuli za Bunge; kukamilika kwa mfumo wa kieletroniki wa kutunza kumbukumbu za ofisi na mfumo wa kieletroniki wa Maktaba; na kuandaliwa kwa Mipango Mikakati ya Vyama vya hiari vya kibunge (APNAC, TAPAFE, TYPF); na

(iv) **Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya IV na V (PFMRP IV & V):** Shughuli zilizotekelezwa ni kutolewa mafunzo ya muda mfupi kwa Wabunge na Sekretarieti za Kamati za Bunge kwenye maeneo ya uchambuzi wa Mpango, Bajeti, Vyanzo vya mapato, Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo, uchumi wa kidigitali, namna ya kufanya makisio *(forecasting)* ya ukuaji wa uchumi na viashiria vyake; kuandaa mfumo wa kielektroniki wa kutunza takwimu za Kibajeti na Kiuchumi; Kuandaa mwongozo wa uchambuzi wa Bajeti kwa Wabunge.

**(d) Ujenzi wa Majengo ya Utawala kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Shughuli zilizotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa majengo 57 ya halmashauri kati

ya 70 na ujenzi wa ofisi na makazi ya viongozi katika mikoa, wilaya na tarafa.

**(e) Vitambulisho vya Taifa**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kuendelea na zoezi la usajili wa raia wa Tanzania, wageni wakaazi pamoja na wakimbizi ambapo kufikia Desemba, 2020, jumla ya watu 22,268,170 wametambuliwa na utoaji wa namba za utambulisho wa Taifa kwa wananchi 18,605,102. pamoja na kuchapisha vitambulisho 6,313,787 na kuvigawa kwa wananchi; na ununuzi wa mashine mpya mbili (2) zenye uwezo wa kuchapa vitambulisho 9,000 ikilinganishwa na vitambulisho 750 kwa saa ili kuongeza kasi ya kuchapisha vitambulisho.

**(f) Usalama wa Raia**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa nyumba 402 za makazi ya askari polisi nchi nzima; kukamilika kwa ukarabati wa Chuo cha Taaluma ya Polisi Dar es Salaam (DPA) na kukamilika kwa ujenzi wa majengo sita (6) ya ghorofa tatu (3) kila moja kwa ajili ya kuishi familia 24 za askari Musoma – Mara; kuendelea na ujenzi wa nyumba mbili (2) za makazi ya Askari Wilayani Meatu - Simiyu; kuendelea na ujenzi wa majengo matatu (3) ya ghorofa tatu (3) kwa ajili ya kuishi familia 12 za Askari Byekera – Kagera; na kuendelea na ujenzi wa vituo vya Polisi Mbalizi - Mbeya na Mkokoti – Zanzibar. Vile vile, Ujenzi wa Majengo sita (6) ya ghorofa tatu (3) kila moja ya kuishi familia 24 za Askari Mabatini – Mwanza unaendelea ambapo utekelezaji umefikia hatua za ukamilishaji.

**(g) Magereza**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba 182 za makazi ya askari nchi nzima; ujenzi wa Makao Makuu ya muda eneo la Msalato awamu ya kwanza imekamilika na ujenzi wa kiwanda cha Samani - Msalato ambapo utekelezaji umefikia hatua ya kusafisha jengo kwa kupiga rangi, usimikaji wa mashine za kiwanda, utengenezaji wa mazingira yanayozunguka kiwanda (landscaping) na ujenzi wa miundombinu ya majitaka.

**(h) Zimamoto na Uokoaji**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha Zimamoto na Uokoaji Wilayani Chato - Geita; kufikia asilimia 18 ya ujenzi wa nyumba za makazi ya Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Jijini Dodoma; na kuendelea na ujenzi wa kituo cha zimamoto na uokoaji katika Wilaya ya Chamwino.

**(i) Uhamiaji**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya

Uhamiaji Jijini Dodoma ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 41, ofisi za uhamiaji katika mikoa ya Lindi (asilimia 76), Geita (asilimia 55), Mtwara (asilimia 30), Manyara (asilimia 75); ujenzi wa nyumba ya makazi ya Afisa Uhamiaji Mkoa wa Mwanza umefikia asilimia 95; ujenzi wa nyumba ya Kamishna Jenerali iliyopo Masaki - Dar es Salaam umefikia asilimia 80; ukarabati wa nyumba za makazi ya watumishi zilizopo Ibinzamata - Shinyanga umefikia asilimia 72; na ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji katika Wilaya ya Chato asilimia 50.

**(j) Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

**(a) Ujenzi wa Nyumba za Viongozi Wastaafu wa Kitaifa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi na kukabidhiwa kwa nyumba ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili Mhe. Ali Hassan Mwinyi na kuendelea na ujenzi wa nyumba ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete.

**(b) Ujenzi wa Majengo ya Utawala kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa majengo 57 ya halmashauri kati ya 70 yaliyokuwa kwenye Mpango na ofisi na makazi ya viongozi katika mikoa na wilaya mbalimbali nchini.

**(c) Mifumo ya Kuhifadhi Taarifa za Watumishi wa Umma**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) na utoaji wa mafunzo kwa watumiaji kutoka kwenye Taasisi za Umma; kukamilika kwa usanifu wa Mfumo wa e–OPRAS; kukamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Usaidizi wa Masuala ya Serikali Mtandao – Mji wa Serikali - Mtumba; kuendelea na mafunzo ya Mpango wa Rasilimali watu (e-HRP); na kuimarisha mifumo ya Serikali Mtandao.

**(k) Utawala wa Sheria**

**(i) Usajili wa Vizazi na Vifo:** Hatua iliyofikiwa ni kusajiliwa kwa vizazi 5,183,344 vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5) ambapo kiwango cha usajili kimeongezeka kutoka asilimia 38 mwaka 2018 hadi kufikia asilimia 49.4 mwaka 2020; kuongezeka kwa usajili wa vizazi vya watoto walio shuleni kutoka vizazi 325,583 mwaka 2019 hadi vizazi 372,153 mwaka 2020; kusajili na kutoa vyeti vya vifo 63,167 mwaka 2020 ikilinganishwa na vyeti vya vifo 52,753 mwaka 2019 na kuboreshwa kwa usajili wa vizazi na vifo kwa kutumia Mfumo wa TEHAMA kwa kufunga mfumo wa kielektroniki wa Usajili wa vizazi na vifo katika Wilaya zote nchini.

**(ii) Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Utoaji Haki na kulinda Haki za**

**Binadamu:** Hatua zilizofikiwa ni: kupungua kwa mianya ya rushwa kwenye Mifumo ya Haki-Jinai; kuanza kwa huduma ya mahakama inayotembea kwa mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza; kutolewa kwa mafunzo ya kujenga uwezo wa Kamati za Ulinzi wa wanawake na watoto katika wilaya za Kasulu na Sengerema; kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya msaada wa kisheria ili kutoa fursa na mazingira mazuri ya kupata haki; na kutolewa kwa mafunzo kuhusu sheria ya huduma ya msaada wa sheria kwa watendaji wa Serikali zaidi ya 1,080 ili kuwajengea uwezo watendaji wa vijiji, vitongoji na mitaa.

(iii) **Mradi wa Haki Mtandao (e-Judiciary na e–Justice):** Shughuli zilizotekelezwa ni kuimarishwa kwa matumizi ya TEHAMA katika mifumo ya utoaji haki; na kuanzishwa kwa kanzidata ya Wanasheria walio katika utumishi wa umma ili kuharakisha upatikanaji wa huduma za utoaji haki nchini.

(iv) **Kusimamia Mfumo wa Haki na Utoaji Haki:** Hatua iliyofikiwa ni kusikilizwa na kukamilika kwa mashauri 257,020; kutunga Sheria mpya ya Usuluhishi ili kurahisisha mazingira ya upatikanaji wa Haki nchini; na kuanzisha utaratibu wa makubaliano kati ya Jamhuri na Mshtakiwa katika makosa ya jinai (*Plea Bargaining*).

(v) **Mapambano Dhidi ya Rushwa:** Tanzania imeendelea kufanya vizuri Katika mapambano ya rushwa kwa kufikia kiwango cha asilimia 37 na kushika nafasi ya 96 kati ya 180 duniani ikiwa ni kupanda kwa nafasi 23 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 30 katika nafasi ya 119 ya mwaka 2015.

(vi) **Usuluhishi:** Kutungwa kwa Sheria ya Usuluhishi ya Mwaka 2020 ambayo pamoja na masuala mengine imeweka mfumo wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi kuendana na mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania ni Mwanachama. Sheria hiyo inaanzisha Kituo cha Usuluhishi cha Tanzania ambacho kitasuluhisha migogoro ya ndani na nje ya nchi.

#### 3.3.3.9 Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato katika Halmashauri

Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kimkakati kwa lengo la kuziwezesha halmashauri kuongeza mapato na hatimaye kujitegemea kibajeti ili kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu. Hadi Juni 2020, Serikali imesaini mikataba ya utekelezaji wa miradi 38 ya kimkakati yenye thamani ya shilingi 288,060,194,785 iliyopo kwenye mikoa 17 na halmashauri 33. Miradi hiyo inajumuisha masoko (15), stendi (12), viwanda (4), machinjio (2), maegesho ya malori (2), ghala (1), kituo cha biashara (1) na uendelezaji fukwe (1). Miradi hiyo itakapokamilika inatarajiwa kuwa na manufaa mbalimbali ikiwemo: kuboresha mazingira ya wafanyabiashara wadogo ikiwemo mama lishe na bodaboda;

kuongeza upatikanaji wa mapato; na kuboresha masoko ya mazao na bidhaa za kilimo, mifugo na viwanda ili kuchochea upatikanaji wa ajira kwa vijana.

Katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 50.6 zimetumika na shilingi bilioni 19.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21 kwa ajili ya kugharamia miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato katika halmashauri. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: miradi iliyokamilika na kuanza kutoa huduma inajumuisha Soko la Mburahati (Ubungo), Kiwanda cha Kuvuna Chumvi Itambula (Momba), Ghala la Kisasa (Ruangwa) na Soko la Kisasa (Morogoro); na miradi iliyo katika hatua za umaliziaji inajumuisha Soko la Kisasa la Magomeni (Kinondoni), Soko la Kisasa la Kisutu (Ilala), Machinjio ya Kisasa ya Vingunguti (Ilala), Stendi ya Kisasa Mangaka (Nanyumbu) na Kituo cha Kimataifa cha Mabasi Mbezi Louis (Ubungo).

### 3.3.4 Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji

#### 3.3.4.1 Miundombinu

**(a) Reli**

**(i) Ukarabati wa Njia Kuu ya Reli, Vichwa vya Treni na Mabehewa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa asilimia 94 ya ukarabati wa njia ya reli kutoka Dar es Salaam hadi Kilosa (km 283); kukamilika kwa asilimia 99.8 ya ukarabati wa kipande cha reli kutoka Kilosa hadi Isaka (km 687); na kuendelea na uundaji wa injini 16.

**(ii) Ufufuaji wa Njia ya Reli ya Tanga – Arusha (km 439)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa reli ya Tanga – Moshi - Arusha (km 439) na kuanza kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo. Hatua hizi zimeongeza njia ya usafirishaji na kurahisisha upatikanaji wa huduma za uhakika za usafiri na usafirishaji wa mizigo na abiria.

**(iii) Miradi Inayotekelezwa na Fedha za Mfuko wa Reli (RIF):**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa njia ya reli ya Kilosa - Gulwe; kuendelea na ukarabati wa madaraja yaliyoharibiwa na mvua nyingi zilizonyesha kati ya Oktoba, 2019 na Aprili, 2020 katika maeneo ya Zuzu – Kigwe – Bahi; Kilosa – Gulwe; Kaliua - Mpanda; na eneo la Mto Ugala; pamoja na ukarabati reli ya Tanga hadi Arusha (km 439) ambao umekamilika na huduma zimeanza kutolewa.

**(iv) Ununuzi na Ukarabati wa Vichwa vya Treni na Mabehewa**

Hatua iliyofikiwa ni: kununuliwa kwa vichwa vipya 11 vya treni na kukarabatiwa

mabehewa 347 ya mizigo na mabehewa 20 ya abiria.

**(v) Usafiri wa Treni Jijini Dar es Salaam (Commutter train)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli. Kuendelea kumtafuta Mtaalamu Mshauri *(Transaction Advisor)* ili kushauri namna bora ya kuishirikisha sekta binafsi na utafutaji wa fedha za kuanza mradi.

**(vi) Uboreshaji wa Reli ya TAZARA**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa jengo la stesheni ya Fuga; ununuzi wa mitambo ya kupakia na kushusha mizigo mizito na kuendelea na ukarabati wa njia namba tatu ya reli katika stesheni ya Fuga. Uboreshaji wa kituo cha reli cha Fuga/Kisaki umewezesha usafirishaji wa mizigo na mitambo ya ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere.

**(b) Barabara na Madaraja**

**Barabara za Lami Zinazofungua Fursa za Kiuchumi**

(a) **Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupiro Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499):** Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi kwa sehemu ya Kidatu – Ifakara (km 66.9) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 19.7.

(b) **Barabara ya Tabora - Ipole - Koga - Mpanda (km 383)**: Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa barabara sehemu ya Tabora – Sikonge (km 30); na kuendelea na ujenzi wa barabara sehemu za Usesula - Komanga (km 115) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 56.05, Komanga – Kasinde (km 120) asilimia 74.12, na Kasinde – Mpanda (km 118) asilimia 47.48.

(c) **Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235):** Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa barabara ya Makutano – Natta ambapo utekelezaji umefikia asilimia 86.0; ujenzi wa barabara ya Sanzate – Natta (km 50) upo katika maandalizi; na Mto wa Mbu – Loliondo sehemu ya Waso – Sale (km 50) utekelezaji umefikia asilimia 56.38.

(d) **Barabara ya Manyoni - Itigi – Tabora (km 259.75):** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa barabara sehemu ya Tabora – Nyahua (km 85) na Manyoni - Itigi - Chaya (km 89.35); na kuendelea na utekelezaji wa sehemu ya Nyahua – Chaya (km 85.4) ambapo umefikia asilimia 77.66.

(e) **Barabara ya Itoni – Ludewa - Manda (km 211.4):** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 57.37.

(f) **Barabara ya Handeni - Kibereshi – Kibaya - Singida (km 460):** Hatua

iliyofikiwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

(g) **Barabara ya Dodoma – Mtera - Iringa (km 260):** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Dodoma – Iringa na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mchepuo wa Iringa *(*Iringa Bypass km 7.3*)* kwa kiwango cha lami.

(h) **Mbeya – Chunya – Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa (km 528):** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa barabara za Mbeya – Lwanjilo na Lwanjilo – Chunya; ujenzi wa sehemu za Chunya – Makongolosi (km 43) umefikia asilimia 75.4; na kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu za Mkiwa – Noranga na Mbalizi – Makongolosi.

(i) **Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 353.7):** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa barabara za Kidahwe – Uvinza (km 76.6), Tabora – Ndono (km 42), Ndono – Urambo (km 52), na Kaliua – Kazilambwa (km 56); kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Urambo - Kaliua (km 28) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 91; na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Chagu – Kazilambwa (km 36) kwa kiwango cha lami.

(j) **Barabara ya Mtwara - Masasi - Songea - Mbamba Bay (km 659):** Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi kwa sehemu ya Mbinga - Mbamba Bay (km 66) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85.5 na sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50) asilimia 90; na kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea (km 107).

(k) **Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 535.25):** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa sehemu ya Mbarali – Ubaruku (km 8.9) katika barabara ya Igawa – Mbarali – Ubaruku (km 16); ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Njombe – Moronga (km 53.9) umefikia asilimia 83.73 na Moronga – Makete (km 53.5) umefikia asilimia 60; na kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara za Mafinga – Mgololo, Igawa – Songwe – Tunduma na barabara ya mchepuo wa Uyole – Songwe (Mbeya Bypass).

(l) **Dumila – Kilosa – Mikumi (km 141):** Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi sehemu ya Rudewa - Kilosa (km 24) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 42.27.

**Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani**

(a) **Barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (km 112):** kuendelea na ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98.

(b) **Barabara ya Marangu - Tarakea - Rongai - Kamwanga /Bomang'ombe -**

**Sanya Juu (km 330.31):** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa sehemu ya Sanya Juu – Elerai (km 32.2); na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8) na Kwasadala – Masama – Machame Junction (km 16). Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kijenge – Usa River (Nelson Mandela AIST) unaendelea na kuendelea na maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Mianzini – Ngaramtoni (km 18), ukarabati wa barabara ya Tengeru – Moshi – Himo (km 105) na mizani ya Himo.

**(c)** **Barabara ya Isaka - Lusahunga (km 474)**: hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ukarabati wa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga (km 110); na kuendelea na ukarabati wa maeneo korofi katika barabara ya Lusahunga – Rusumo (km 92); na kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba/Rulenge – Murugarama na barabara ya Rulenge – Kabanga.

**(d)** **Barabara ya Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi (km 517.4):** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Mpanda - Mishamo (km 100) sehemu ya Mpanda - Ifukutwa - Vikonge (km 30); na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Vikonge – Magunga – Uvinza (km 159).

**(e)** **Barabara ya Nyanguge - Musoma, na Michepuo ya Usagara - Kisesa na Bulamba - Kisorya (km 483.9):** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ukarabati wa barabara ya Makutano – Sirari pamoja na uwekaji taa za barabarani katika barabara ya kuelekea uwanja wa ndege wa Mwanza. Aidha, ujenzi wa barabara ya Nansio - Kisorya - Bunda - Nyamuswa sehemu ya Kisorya - Bulamba (km 51) unaendelea na umefikia asilimia 92.12; barabara ya Musoma – Makojo – Busekela sehemu ya Suguti – Kusenyi (km 5) umefikia asilimia 54; na ujenzi wa barabara ya Nyamuswa – Bulamba umeanza.

**(f)** **Barabara ya Mwigumbi - Maswa - Bariadi - Lamadi (km 171.8):** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Maswa - Bariadi (km 49.7) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara za Kolandoto – Mwanhuzi (km 10), Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi na Isabdula (Magu) – Bukwimba – Ngudu – Ng'hungumalwa.

**(g)** **Barabara ya Kidahwe - Kasulu – Kibondo - Nyakanazi (km 434.25**): Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa sehemu ya Kidahwe - Kasulu (km 63); kuendelea na ujenzi wa barabara ya Nyakanazi – Kakonko ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90.8; na kuanza ujenzi wa barabara ya Kakonko (Kabingo) – Kibondo – Kasulu – Manyovu (km 260) na Nduta – Kibondo (km 25.6) sehemu ya njia panda ya Nduta.

**(h)** **Barabara ya Usagara - Geita - Buzirayombo – Kyamyorwa (km 310):** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa usanifu wa kina wa sehemu ya Geita –

Bulyanhulu *Junction* (km 58.3), Bulyanhulu *Junction* – Kahama (km 61.7) na Nyamirembe *Port* – Katoke (km 50).

**Barabara za Kupunguza Msongamano Jijini Dar es Salaam (km 169.66)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.66) sehemu ya Kibamba – Mloganzila (km 4.0) na barabara ya Ardhi – Makongo – Goba (km 9.0) sehemu ya Goba – Makongo (km 4.0); ujenzi wa barabara ya Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7) sehemu ya Kitunda– Kivule (km 3.2) umefikia asilimia 40; Ardhi – Makongo (km 5) asilimia 14; na Wazo Hill – Madale (km 6) asilimia 24; na upanuzi wa Barabara ya New Bagamoyo (Kawawa Junction) – Tegeta sehemu ya Morocco – Mwenge umefikia asilimia 60. Aidha, usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Mjimwema – Kimbiji (km 27.0) na Kongowe – Mjimwema – Kivukoni (km 25.1) umekamilika.
Vile vile, mradi wa upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) ujenzi umefikia asilimia 92.9 kwa sehemu ya Kimara – Kiluvya (km 19.2) kuwa njia nane na upanuzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji.

**Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka**

**(i)** **Awamu ya Pili:** Hatua iliyofikiwa ni ujenzi wa Lot 1 inayohusisha barabara zenye urefu wa km 20.3 (Mbagala - Mzunguko wa Bandari (Bendera Tatu), Bendera tatu – Kariakoo, Sokoine – Zanaki, Kawawa Road – Morogoro Road (Magomeni), Chang'ombe Road – Kilwa Road) pamoja na Lot 2 inayohusisha ujenzi wa majengo (vituo 2, yadi 1 na vituo mlisho 4). Kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 6.93.

**(ii)** **Awamu ya Tatu na Nne**: Awamu ya Tatu itahusisha barabara za Azikiwe na Maktaba, Bibi Titi, Uhuru na Nyerere hadi Gongo la Mboto zenye jumla ya kilometa 23.6 na kituo kikuu cha mabasi Kariakoo, Shaurimoyo na Uhuru kupitia Buguruni hadi TAZARA na awamu ya nne itahusisha barabara za Ali Hassan Mwinyi na Bagamoyo hadi Tegeta pamoja na barabara ya Sam Nujoma (Ubungo - Mwenge) zenye jumla ya km 25.9. Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

**Ujenzi wa Barabara za Juu (*Flyover*) Jijini Dar es Salaam**
Hatua iliyofikiwa ni kukamilika na kuanza kutumika kwa barabara ya juu (interchange) ya Ubungo; kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya Fire, Magomeni, Mwenge, Tabata/ Mandela, Morocco, Buguruni pamoja na makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Junction; na kuanza maandalizi ya ujenzi wa Mabey Flyovers katika jiji la Dar es

Salaam, Dodoma na Mwanza.

**Barabara ya Dodoma University na Barabara ya Mzunguko wa Dodoma**
Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa barabara za Ihumwa - Chuo Kikuu cha Dodoma (km 12) na barabara za Ikulu (Chamwino); kuanza kwa ujenzi wa barabara ya mzunguko ya Mtumba – Veyula – Nala – Matumbulu – Mtumba (km 104); na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kongwa Junction – Ng'ambi – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 98).

**Barabara za Vijijini na Mijini**
Shughuli zilizofanyika ni: kukamilika kwa matengenezo ya muda maalumu kwenye barabara za urefu wa kilometa 2,749.23; kukamilika kwa matengenezo ya sehemu korofi kwenye barabara za urefu wa kilometa 2,995.05; kukamilika kwa matengenezo ya kawaida kwenye barabara za urefu wa kilometa 7,698.04; kukamilika kwa ujenzi wa madaraja 98; na kujenga Makalavati yenye urefu wa mita 1,429.8 na mitaro yenye urefu wa mita 28,350.8.

Vile vile, kupitia Programu ya Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Serikali za Miji (ULGSP) barabara zenye urefu wa kilometa 116.60 zimejengwa kwa kiwango cha lami na ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 44.80 unaendelea. Kupitia mradi wa kuendeleza Jiji La Dar es Salaam (DMPDP) ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 108 kwa kiwango cha lami umekamilika.

**Ujenzi wa Madaraja**

- **(i)** **Ujenzi wa Madaraja Makubwa:** Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa madaraja ya Mara (Mara), na Magara (Manyara); kuendelea na ujenzi wa madaraja ya Ruhuhu ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95, Kitengule (asilimia 50), *New* Wami (asilimia 41.4), Msingi (asilimia 36) na Kigongo/Busisi (asilimia 5.8).
- **(ii)** **Daraja la Nyerere na Barabara Unganishi (km 6.9*):*** Hatua iliyofikiwa ni kufikia asilimia 92 ya ujenzi wa barabara unganishi za Kigamboni (Daraja la Nyerere) – Vijibweni (km 1.5); na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Tungi – Kibada (km 3.8) ambao umefikia asilimia 25.
- **(iii)** **Daraja jipya la Tanzanite (Dar es Salaam):** Hatua iliyofikiwa: ni kuendelea na ujenzi wa daraja jipya (km 1.03) na barabara unganishi zenye jumla ya urefu wa km 5.2 ambapo ujenzi umefikia asilimia 55.2.

**Ujenzi wa Nyumba za Serikali**
Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa nyumba moja ya Jaji Jijini Dar es

Salaam, kuendelea na ujenzi wa nyumba ya jaji katika mikoa mitano (5) ambapo katika mkoa wa Tabora ujenzi upo katika hatua za ukamilishaji, Kilimanjaro, Mtwara na Shinyanga ujenzi umefikia katika hatua ya kupaua, na Kagera ujenzi upo katika hatua za maandalizi.

Aidha, ujenzi wa nyumba za Makazi Magomeni "*Quarters*" umefikia asilimia 90, kukamilika kwa ukarabati wa karakana ya TBA Dodoma na kuendelea na upembuzi yakinifu wa ujenzi wa karakana ya Mkoa wa Manyara. Aidha, ukarabati wa karakana za mikoa ya Arusha, Mwanza, Tabora, Dar es Salaam na Mbeya upo katika maandalizi ya michoro.

**(c) Usafiri Majini**

(i) **Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko:** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu (jengo la abiria, ofisi na uzio) katika kivuko cha Lindi – Kitunda, ujenzi wa maegesho na majengo ya kupumzikia abiria katika kivuko kipya cha Kayenze - Bezi pamoja na ujenzi wa maegesho ya Bwina katika kivuko cha Chato - Nkome; kuendelea na upanuzi wa jengo jipya la abiria ikiwemo hatua za mwisho za uwekaji sakafu na ufungaji mifumo ya umeme katika maegesho ya Kigamboni; kuendelea na upanuzi wa maegesho ya Kigamboni; na kuendelea na ujenzi wa maegesho mapya ya kivuko kitakachotoa huduma kati ya Nyamisati na Mafia.

(ii) **Ununuzi wa Vivuko Vipya:** Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa kivuko kipya cha Kigongo – Busisi (MV Mwanza), Pangani – Bweni (MV Tanga), Magogoni – Kigamboni (MV Kazi), Kayenze – Bezi (MV Ilemela), Bugolora – Ukara (MV Ukara II – Hapa kazi Tu, ), Nyamisati – Mafia, Chato – Nkome, ujenzi wa boti ndogo nne (4) za kubebea abiria katika vituo vya Pangani- Bweni ( MV Bweni), Kilambo na Moto (MV Tangazo), Msangamkuu – Msemo (MV Kuchere), na Utete – Mkongo (MV Mkongo).

(iii) **Ukarabati wa Vivuko:** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ukarabati wa vivuko vya MV Pangani II, MV Sengerema, MV Ujenzi, MV Kigamboni, MV Kome II, na MV Utete; kuendelea kukarabati vivuko vya MV Misungwi na MV Ruhuhu.

(iv) **Ujenzi na Ukarabati wa Meli katika Maziwa Makuu: Ziwa Victoria:** Kukamilika kwa ukarabati wa meli mbili (2) za New Butiama Hapa Kazi Tu na New Victoria Hapa Kazi Tu; kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza Hapa kazi Tu yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo ambao umefikia asilimia 35; kukamilika kwa ujenzi wa Chelezo cha kujengea na kukarabati meli katika Bandari ya Mwanza; kupatikana kwa makandarasi kwa ajili ya ukarabati wa meli za MV Umoja na MV Serengeti na

kukamilika kwa maandalizi ya mikataba kwa ajili ya ukarabati wa meli hizo; na kukamilika ukarabati wa meli za MV Clarias na MT Wimbi. **Ziwa Tanganyika:** kukamilika kwa mikataba kwa ajili ya Ujenzi wa Meli Mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 pamoja na ukarabati wa meli ya MV Liemba; na ukarabati wa meli ya MT Sangara ambapo katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 53.5 zimetumika na shilingi bilioni 12.8 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21.

Aidha, shughuli nyingine zilizokamilika ni: Ujenzi wa magati ya Lushamba, Ntama, Nyamirembe, Magarine na Gati la majahazi Mwigobero; ununuzi wa vifaa vya kuhudumia mizigo na meli; ukarabati wa majengo na ofisi za bandari za Ziwa Victoria; uboreshaji wa eneo la kushukia abiria Mwanza North; na ukarabati wa 'Link Span' ya bandari ya Mwanza South.

**Ziwa Nyasa:** Kukamilika kwa ujenzi wa matishari mawili (2) yenye uwezo wa kubeba tani 1000 kila moja; na ujenzi wa meli moja mpya ya MV Mbeya II yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na mizigo tani 200 umekamilika na kuanza kufanya kazi.

**(d) Bandari**

**(i) Bandari ya Dar es Salaam:** shughuli zilizofanyika ni: Kuboreshwa kwa gati namba 1 – 4 (gati namba 1-3 kwa ajili ya mizigo mchanganyiko na gati namba 4 kwa ajili ya mizigo ya kichele mfano ngano na mbolea); kukamilika kwa ujenzi wa gati la kupakia na kushushia magari (RoRo); na kuendelea na uboreshaji wa gati na 5 hadi 7 (gati namba 5 kwa ajili ya mizigo ya kichele na gati namba 6-7 ni kwa ajili ya makontena). Hatua hizi zimechangia kupungua kwa idadi ya siku za meli kukaa bandarini kutoka siku saba (7) hadi siku tano (5) na kuongezeka kwa shehena ya mizigo iliyohudumiwa kutoka tani milioni 15.4 hadi tani milioni 19.52. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 90.

**(ii) Bandari ya Tanga:** Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa uongezaji wa kina cha lango la kuingia meli pamoja na kutoka mita nne (4) hadi mita 13 na kuweka vifaa vya kuongezea meli; na kukamilika kwa ujenzi wa gati mbili (2) kwenye kina kirefu. Aidha, kazi ya maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya gati la mafuta ghafi kutoka Uganda inaendelea. Kwa upande wa Bandari ya Mwambani uhuishaji wa upembuzi yakinifu wa uendelezaji wa bandari unaendelea.

**(iii) Bandari ya Mtwara**: Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa gati jipya lenye urefu wa mita 300 la kuhudumia shehena mchanganyiko.

**(iv) Bandari Kavu katika eneo la Ruvu:** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa utwaaji wa eneo lenye ukubwa wa hekta 502, ujenzi wa mchepuo wa reli kutoka reli ya kati kwenda Kwala/Vigwaza, ujenzi wa yadi, njia ya reli na ofisi za muda kwenye eneo la hekta tano (5). Aidha, ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita 18 kutoka Vigwaza/Kwala na ujenzi wa sakafu ngumu (pavement) yenye ukubwa wa hekta 5 kwa ajili ya kuhifadhi shehena za mizigo unaendelea.

**(v) Bandari za Maziwa Makuu**

**Ziwa Victoria:** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa magati ya Nyamirembe, Magarine, Lushamba, Ntama na Mwigobelo.

**Ziwa Tanganyika:** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa magati ya Sibwesa na Kabwe; na kuendelea na ujenzi wa Bandari za Karema, Ujiji, Kibirizi na Lagosa.

**Ziwa Nyasa:** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa sakafu ngumu katika bandari ya Kiwira na Itungi; na ujenzi wa sehemu ya kuegesha meli (ramp) katika bandari ya Kiwira.

**(e) Usafiri wa Anga**

**(i) Kuboresha huduma za Ulinzi na Usalama katika Viwanja vya Ndege:** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa: ufungaji wa mifumo ya Kamera za kiusalama (CCTV) katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma; ununuzi wa mitambo miwili (2) ya ukaguzi wa abiria na mizigo (X- Ray Machine) katika Viwanja vya Ndege vya Iringa na Songea; ununuzi wa vifaa vya mawasiliano kwa ajili ya viwanja vya ndege vya Arusha, Songea, Kahama, Mafia na Iringa.

**(ii) Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA)**: Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa karakana ya matengenezo ya ndege na kununuliwa kwa magari mapya matatu (3) ya zimamoto yenye uwezo wa kubeba lita za maji 10,000; kufungwa kwa taa za kuongozea ndege na ukarabati wa maegesho ya magari; na kuendelea na taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa tabaka la juu la barabara ya kuruka na kutua ndege.

**(iii) Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**: Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upanuzi wa maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la mizigo, uzio wa kiwanja, jengo la kuongozea ndege, kituo cha umeme, maegesho ya magari, mfumo wa kuondoa maji ya mvua kiwanjani na kufungwa kwa taa za kuongozea ndege.

**(iv)** **Kiwanja cha Ndege cha Mtwara:** Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege, viungio, maegesho ya ndege, ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani pamoja na maegesho ya magari ambapo utekelezaji umefikia asilimia 49.

**(v)** **Kiwanja cha Ndege cha Kigoma**: Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na taratibu za ununuzi wa Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la abiria, upanuzi na ukarabati wa maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la kuongozea ndege pamoja na miundombinu yake ikiwemo mitambo ya kuongozea ndege, ujenzi wa kituo kidogo cha umeme, ujenzi wa kituo cha uchunguzi wa hali ya hewa pamoja na ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari.

**(vi)** **Viwanja vya Ndege vya Sumbawanga na Shinyanga**: Hatua iliyofikiwa ni kusainiwa kwa mikataba ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani na maegesho ya magari pamoja na ufungaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.

**(vii)** **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe:** Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ukarabati wa tabaka la juu la barabara ya kutua na kuruka ndege, barabara ya kiungio pamoja na ujenzi wa eneo la usalama kwenye barabara ya kutua na kuruka ndege ambapo utekelezaji umefikia asilimia 10.6.

**(viii)** **Viwanja vya Ndege vya Mikoa:** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege kwa kiwango cha changarawe katika kiwanja cha Nachingwea; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya Geita (asilimia 86) na Songea (asilimia 91); ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa upo katika hatua za awali; kukamilika kwa malipo ya fidia kwa wananchi walioathiriwa na mradi wa upanuzi wa kiwanja cha Ndege cha Dodoma, kuendelea kukamilisha upanuzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na kufungwa kwa mfumo wa kuongeza ndege ambapo kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 98.

**(ix)** **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato:** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa maandalizi ya mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ambao utagharimu dola za Marekani milioni 330, sawa na shilingi bilioni 759.

**(x)** **Kiwanja cha Ndege cha Tabora:** Hatua iliyofikiwa ni kusainiwa kwa mikataba ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua, jengo jipya la abiria, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari, barabara ya kiungio na jengo la uchunguzi

wa hali ya hewa. Aidha, taratibu za kuanza utekelezaji wa mradi huu zinaendelea.

(xi) **Ufungaji wa Rada Nne za Kuongozea Ndege za Kiraia JNIA, KIA, Mwanza na Songwe**: Hatua iliyofikiwa ni kununuliwa kwa rada nne (4) za kuongoza ndege za kiraia na kufungwa katika viwanja vya ndege vya Julius Nyerere, Kilimanjaro, Songwe na Mwanza na hivyo kuongeza kiwango cha usalama wa abiria katika viwanja vya ndani.

(xii) **Ununuzi wa Rada tatu (3) za Hali ya Hewa:** Hatua iliyofikiwa ni: kufungwa kwa rada moja (1) eneo la Mtwara; kukamilika kwa malipo ya mkataba wa ununuzi wa rada mbili (2) za hali ya hewa zitakazofungwa Mbeya na Kigoma; na kupokelewa kwa vifaa mbalimbali vya uchunguzi wa hali ya hewa.

(xiii) **Kuboresha mawasiliano katika viwanja vya ndege:** Hatua iliyofikiwa ni kununuliwa na kufungwa kwa vifaa vya mawasiliano ya sauti kati ya Marubani na waongozaji ndege katika Viwanja vya JNIA na KIA; na kununuliwa na kufungwa kwa vifaa vya mawasiliano katika jengo jipya la kuongozea ndege katika kituo cha Mwanza;

(xiv) **Kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume – Zanzibar**: Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa mradi wa kufunga Mfumo wa kuongoza Ndege kutua salama (Instrument Landing System - ILS).

(xv) **Mikataba ya usafiri wa Anga:** Hatua iliyofikiwa ni Tanzania kuingia mikataba mipya ya usafiri wa Anga (Bilateral Air Services Agreements - BASA) kati yake na nchi zipatazo 74 kutoka 70 zilizokuwepo. Mikataba mipya ya BASA kati ya Tanzania na nchi za Mauritius, Rwanda na Hispania ilisainiwa. Aidha, Mikataba ya BASA kati ya Tanzania na nchi za Zambia, Uturuki, Oman, Sri Lanka, Uingereza, Zimbabwe, Ethiopia, Afrika ya Kusini na Jordan ilipitiwa upya.

### (f) Nishati

**Miradi ya Kufua Umeme**

(i) **Mradi wa Kinyerezi I *Extension* – MW 185**: Hatua iliyofikiwa ni: kufungwa kwa mitambo minne (4) ya kuzalisha umeme katika eneo la mradi; kukamilika kwa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi I kV 220; kuendelea na upanuzi wa njia ya msongo wa kV 132 kutoka Kinyerezi I hadi kituo cha kupoza umeme cha Gongo la Mboto. Kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 84.

(ii) **Mradi wa Kufua Umeme wa Rusumo - MW 80 (Kagera):** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa asilimia 67 ya ujenzi wa bwawa la maji katika mgodi wa

kufua umeme; uchorongaji wa mtaro wa handaki (*Head Race Tunnel – HRT)* umefikia asilimia 64.4; kuendelea kwa ujenzi wa mitambo ya kufua umeme *(Power House)* ambapo utekelezaji umefikia asilimia 73.4; ujenzi wa kituo cha kupoza umeme na njia za kusafirisha umeme umefikia asilimia 20; na kuendelea na ujenzi wa nyumba 34 za wafanyakazi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80. Kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 73.

**(iii)** **Mradi wa Kakono - MW 87:** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa usanifu wa mradi.

**(iv)** **Mradi wa Ruhudji - MW 358 (Njombe):** Hatua iliyofikiwa ni kuendelea kuhuisha upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi.

**(v)** **Mradi wa Rumakali - MW 222 (Njombe):** Hatua iliyofikiwa ni kuendelea kuhuisha upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi.

**(vi)** **Mradi wa Kufua Umeme wa Malagarasi – MW 45 (Kigoma):** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa usanifu wa mradi.

**(vii)** **Mradi wa Kikonge – MW 300:** Kazi zilizotekelezwa ni kukamilika kwa tathmini ya mazingira ya kimkakati; na kuendelea na upembuzi yakinifu.

**(viii)** **Umeme wa Jotoardhi – Ngozi (Mbeya)**: Hatua iliyofikiwa ni kuajiriwa kwa mtaalamu mshauri kwa ajili ya kuandaa mpango kazi pamoja na kusimamia shughuli za uchorongaji; kuendelea na uhakiki wa rasilimali ya jotoardhi; kuanza kwa tathmini ya ardhi inayohitajika kwa ajili ya shughuli za uchorongaji; na kuandaa Mkakati wa Usimamizi wa Mazingira.

**Miradi ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme**

**(i)** **Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 Makambako – Songea:** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na kuunganishwa kwa umeme katika vijiji 122 vinavyopitiwa na mradi ambapo wateja 16,281 kati ya 22,700 wameunganishiwa umeme katika mji wa Makambako na wilaya za Njombe, Ludewa, Songea Vijijini, Songea Mjini, Namtumbo na Mbinga; na kukamilika kwa ufungaji wa *Reactor* katika kituo cha kupoza umeme cha Madaba na uunganishaji wa umeme kwa wateja wengine unaendelea.

**(ii)** **Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 -** ***North West Grid Extension*** **(Iringa – Mbeya - Sumbawanga – Mpanda - Kigoma – Nyakanazi):** Hatua iliyofikiwa katika **Awamu ya Kwanza** ni: kuhuishwa kwa taarifa ya awali ya upembuzi yakinifu kati ya Mbeya na Sumbawanga; na kukamilika kwa uhakiki wa uthamini wa mali zitakazopitiwa na mradi na uainishaji wa mipaka ya mkuza wa njia ya umeme.

**Awamu ya Pili:** Kufanyika kwa maboresho ya taarifa za kiufundi (*technical studies updates*); kukamilika kwa uandaaji wa zabuni kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme; kupatikana kwa wazabuni wa vifaa vya umeme ikiwemo mita 5,000 za awali kwa ajili ya kuwaunganisha wateja wa umeme katika mkoa wa Kigoma; na upatikanaji wa eneo la kujenga kituo cha kupoza umeme Kidahwe.

**(iii) Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 Bulyanhulu – Geita:** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa asilimia 98 ya ujenzi na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme pamoja na njia ya kusafirisha umeme.

**(iv) Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 Geita – Nyakanazi (North West Grid):** Hatua iliyofikiwa katika **Lot A** (Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220, Geita – Nyakanazi): kukamilika kwa asilimia 90 ya utafiti wa tabia za udongo; kuendelea na utafiti wa kina na usanifu wa mradi pamoja na kukamilika kwa ulipaji wa fidia.

**Lot B** (ujenzi wa vituo vya kupoza umeme Geita na Nyakanazi): kukamilika kwa asilimia 90 ya utafiti na upimaji udongo na kuendelea na usanifu wa mradi.

**Lot C** (kusambaza umeme katika vijiji vya Geita - Bwanga na Nyakanazi - Kakonko): kuendelea na usanifu wa mradi.

**(v) Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 Rufiji – Chalinze – Dodoma na Kinyerezi – Chalinze:** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu; na kuendelea na uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi.

**(vi) Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Singida - Arusha – Namanga:** Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na utekelezaji wa mradi ambapo utekelezaji umekamilika kwa asilimia 76.

**(vii) Mradi kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini na Makao Makuu ya Wilaya (REA - III):** Hatua iliyofikiwa ni kuunganishwa umeme katika jumla ya vijiji 10,018.

**Miradi ya Gesi Asilia na Mafuta**

**(i) Usambazaji Gesi Asilia Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi na Pwani**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa kilomita 18 za miundombinu ya usambazaji gesi asilia *(trunk-lines)* yenye uwezo wa kuunganisha zaidi ya wateja 10,000 wa majumbani katika Mkoa wa Dar es Salaam ambapo wateja wapatao 500

wa majumbani na viwanda 48 vimeunganishwa; kurekebishwa kwa mifumo ya magari zaidi ya 400 ili kuwezesha magari hayo kutumia gesi asilia; kukamilika kwa ujenzi wa kilomita sita (6) za miundombinu ya usambazaji wa gesi yenye uwezo wa kuunganisha viwanda zaidi ya 20 katika Mkoa wa Pwani; na kuendelea na majadiliano ya kimkataba ya mauziano ya gesi na viwanda mbalimbali.

**(ii) Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia Katika Kitalu cha Eyasi - Wembere**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa uchorongaji wa visima vitatu (3) vifupi katika maeneo ya Kining'inila – Igunga, Nyaranja - Meatu na Luono – Iramba kwa kutumia wataalamu wa TPDC na STAMICO; kufanyika kwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira; na kutoa elimu kwa jamii.

**(iii) Utafiti katika Vitalu vya Songo Songo Magharibi, 4/1B na Mnazi *Bay* Kaskazini**

Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kupatikana kwa Mshauri Elekezi wa kuhakiki ubora wa takwimu za mitetemo za mfumo wa 3D wakati wa uchukuaji na uchakataji wa takwimu katika kitalu cha 4/1B na kukamilika kwa uchukuaji na uchakataji wa takwimu za mitetemo za mfumo wa 3D katika kitalu cha Mnazi *Bay* Kaskazini.

**3.3.4.2 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

**(a) Anuani za Makazi na Postikodi**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na maandalizi ya makadirio ya majenzi pamoja na kumtafuta mzabuni kwa ajili ya kutengeneza na kubandika vibao vya namba za nyumba katika Halmashauri 12 za Dodoma, Tanga, Moshi, Morogoro, Kibaha, Mwanza, Ilemela, Shinyanga, Bahi, Geita, Chato na Chamwino pamoja na kuboresha miundombinu ya Mfumo katika Halmashauri ya Dodoma.

**(b) Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa ujenzi wa kuimarisha Mkongo wa Taifa kwa kuongeza njia nyingine upande wa Kusini, Kaskazini na Magharibi mwa nchi pamoja na kujenga Mkongo kati ya Njombe – Mfrika – Mlimba – Ifakara (km 340), Mpanda – Mlele – Ipole – Tabora (km 370), Mbeya – Makongolosi – Kipambwe – Rungwa – Chabutwa – Manyoni (km 540) na Arusha – Naret – Simanjiro – Kiteto - Kondoa –Dodoma (km 616).

### 3.3.4.3 Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**(a) Kuwezesha Umilikishaji Ardhi**

Hatua iliyofikiwa ni:Kuandaliwa kwa taarifa za mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 59 na taarifa za mipango kina ya makazi ya vijiji 86; kuandaliwa kwa Hati za Hakimiliki za Kimila (CCRO) 20,841 katika wilaya za Kilombero (7,191), Ulanga (7,523) na Malinyi (6,127); kusajiliwa kwa CCRO 35,497 katika wilaya za Kilombero (9,154), Ulanga (14,418) na Malinyi (11,925); kutolewa kwa CCRO 43,897 kwa wamiliki wa ardhi katika wilaya za Kilombero (15,707), Ulanga (11,736) na Malinyi (16,454); na kukamilika kwa ujenzi wa ofisi za ardhi za halmashauri za wilaya za Kilombero na Ulanga na ukarabati wa jengo la baraza la ardhi.

**(b) Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi**

Hatua iliyofikiwa katika mwaka wa fedha 2019/20 na nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21 ni pamoja na: Kupimwa kwa viwanja 41,105 katika mikoa ya Mwanza (6,414), Tabora (6,427), Geita (7,228), Iringa (375), Shinyanga (5,638), Njombe (4,048), Simiyu (3,488), Rukwa (254), Mbeya (521), Ruvuma (4,797), Morogoro (799), Dodoma (138) na Manyara (978); kumilikishwa kwa viwanja 4,857 katika mikoa ya Mwanza (3,233), Geita (111), Iringa (261), Shinyanga (406), Njombe (55), Simiyu (252), Rukwa (50), Mbeya (386), Ruvuma (77), Dodoma (3) na Manyara (23); kuuzwa kwa viwanja 5,253 katika mikoa ya Dodoma (82), Mbeya (515), Njombe (166), Iringa (214), Tabora (6), Ruvuma (7), Rukwa (220), Simiyu (37), Shinyanga (292), Geita (481) na Mwanza (3,233); kurasimishwa kwa viwanja 30,710 katika halmashauri za Lindi DC, Tunduma TC, Songwe DC, Masasi TC, Mtwara DC, Geita DC, Mbeya CC, Mpanda Manispaa, Sumbawanga MC, Rufiji DC, Musoma Manispaa, Morogoro Manispaa, Gairo DC, Arusha Manispaa, Tabora Manispaa, Shinyanga DC, Bariadi TC, Busega DC, Chamwino DC, Dodoma CC, Babati TC, Magu DC na Misungwi DC; kuanzishwa kwa ofisi za ardhi za mikoa (26) na ofisi za ardhi za halmashauri (185) nchini zinazotoa huduma za upangaji, upimaji, uthamini na umilikishaji ardhi; kununuliwa kwa vitendea kazi mbalimbali vikiwemo vifaa vya kisasa vya upimaji, samani, kompyuta, shajala, pikipiki (5), Mould (15) na Plotter (5) ambavyo vimesambazwa katika ofisi za ardhi za mikoa na halmashauri mbalimbali nchini ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya upimaji, upangaji na umilikishaji; uchongaji wa barabara katika eneo la mradi wa viwanja 20,000 Dar es Salaam; kuboreshwa kwa Mfumo Unganishi wa Taarifa za Ardhi (ILMIS) ili kuimarisha usalama wa miliki na kuongeza ufanisi wake kwa kujenga moduli za uthamini, upangaji wa miji, hati za makazi na za kimila, moduli ya vifaa vya kiganjani kwa ajili ya kukusanya taarifa za upimaji uwandani pamoja na miamala ya upimaji, umilikishaji, kodi na usajili. Aidha, katika kuboresha makazi yasiyopangwa

mijini jumla ya makazi 1,496,357 yalirasimishwa katika halmashauri mbalimbali nchini.

**(c) Mradi wa Kuimarisha Mipaka ya Kimataifa**

Shughuli zilizotekelezwa ni:Kufanyika kwa vikao vya wataalamu kati ya Tanzania na nchi za Kenya na Burundi ambapo ilikubaliwa kuimarisha mpaka kati ya Kenya na Tanzania kilomita 28 kutoka Ziwa Natron hadi Namanga pamoja na kilomita 100 kutoka Kagunga hadi Manyovu katika mpaka kati ya Tanzania na Burundi; na kununuliwa kwa vifaa vya kisasa vya upimaji.

**3.3.4.4 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa**

Katika kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa: Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ukarabati wa makazi ya Balozi wa Tanzania Ottawa – Canada, ofisi na makazi ya Balozi wa Tanzania Kinshasa- Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na majengo ya ubalozi wa Tanzania New Delhi, India; na kuendelea na ujenzi wa vyumba vya madarasa tisa (9) vyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,474 katika Chuo cha Diplomasia (Dar es Salaam) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 32.

**3.3.4.5 Kuimarisha Ushiriki wa Sekta Binafsi**

Serikali inatambua umuhimu wa sekta binafsi katika maendeleo ya nchi. Serikali imeendelea kuweka Sera na Mikakati mbalimbali ya kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Katika mwaka 2020/21, Serikali ilifuta, kupunguza au kuongeza baadhi ya tozo na ushuru ikiwa na lengo la kulinda sekta binafsi ya ndani kama ifuatavyo:

(a) Kuondoa kodi kwa wafanyabiashara wapya kipindi cha miezi sita kuanzia wakati wanapopewa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN). Hatua hii inatofautiana na hali ya awali ambayo mfanyabiashara alifanyia tathmini ya kodi (tax assessment) na kutakiwa kulipa kodi sehemu ya kodi husika mara tu anapopewa TIN;

(b) Kodi ya mapato ya kampuni (Corporate Tax) kwa wawekezaji wapya wa viwanda vya kuzalisha taulo za kike imepungua kutoka kiwango cha asilimia 30 mwaka 2018/19 hadi asilimia 25;

(c) Kupunguza ushuru hadi kufikia asilimia 10 kwenye nywele za bandia zinazotengenezwa ndani ya nchi na kuongeza hadi kufikia asilimia 25 kwenye nywele bandia zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Lengo ni kuwalinda wazalishaji wa ndani ili waweze kupata motisha ya kushiriki kikamilifu katika uzalishaji;

(d) Ushuru wa kuagiza sukari ya kawaida toka nje ulipunguzwa kutoka asilimia 100 hadi asilimia 35;

(e) Kufutwa kwa ushuru katika vifaa vinavyotumika kukata, kung'arisha na kuongeza thamani ya madini ya vito ambapo awali ulikuwa asilimia 10 kwa mwaka mmoja;

(f) Kuondolewa kwa tozo 54 kutoka kwa taasisi mbalimbali za umma zikiwemo za ukaguzi wa maduka mapya ya kuuzia vyakula; usajili wa maduka ya reja reja ya dawa za mifugo; ukaguzi wa viwanda vya samaki; maombi ya alama ya ubora (TBS mark); na tozo ya usajili wa kampuni ya wakala wa forodha (*Clearing Agent*);

(g) Kuendelea na utekelezaji wa masuala muhimu yaliyoibuliwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 na Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara *(Blueprint)* ambapo mkakati wa utekelezaji wake umekamilika na kusambazwa kwa wadau kwa ajili ya utekelezaji. Lengo likiwa ni kuiwezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi;

(h) Kuendelea kubuni mikakati mbalimbali ya kushirikisha wadau wa sekta binafsi. Mfano yalifanyika mapitio ya makubaliano kati ya Serikali na Viwanda Vinne vinavyosindika maziwa yanayokaa muda mrefu bila kuharibika (Ultra Heat Treatment – UHT) vya ASAS LTD, Tanga Fresh Ltd, MilkCom Ltd na AZAM Dairy Products kwa lengo la kuongeza usindikaji wa maziwa kutoka lita 154,100 hadi lita 284,500 kwa siku. Maziwa haya yanapatikana katika mikoa mbalimbali nchini; na

(i) Kuzinduliwa kwa kiwanda cha Kukoboa Kahawa cha GDM Limited kilichopo Mlowo (Mbozi) mkoani Songwe chenye uwezo wa kukoboa tani 10 za kahawa kwa saa.

**3.3.4.6 Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)**

Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya PPP inajumuisha miradi ifuatayo:

(a) Miradi ya Ujenzi wa Viwanda vya Dawa Muhimu na Vifaa Tiba itakayotekelezwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) katika Mikoa ya Pwani, Mwanza na Mbeya ambapo upembuzi yakinifu umekamilika na hatua za kuwapata wabia zinaendelea;

(b) Mradi wa Uendeshaji wa Huduma ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam Awamu ya Kwanza: kukamilika kwa upembuzi yakinifu na kuandaliwa kwa nyaraka za zabuni kwa ajili ya watoa huduma;

(c) Miradi ya ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne na Kituo Changamani cha Biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere upembuzi yakinifu wa miradi hiyo umekamilika;

(d) Mradi wa Kusambaza Gesi Asilia katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara ambapo upembuzi yakinifu wa awali umekamilika;

(e) Ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* ya Tanga – Arusha - Musoma pamoja na matawi ya Engaruka na Minjingu ambapo upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli na matawi yake umekamilika;

(f) Mradi wa ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* ya Mtwara – Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga ambapo mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali yanaendelea;

(g) Mradi wa Ujenzi wa Hosteli za Chuo cha Elimu ya Biashara katika Kampasi za Dodoma na Dar es Salaam ambapo upembuzi yakinifu wa awali umekamilika;

(h) Ujenzi wa Hoteli ya Nyota Tano, ujenzi wa Kituo Changamani cha Biashara (Commercial Complex) na ujenzi wa kituo cha kuhudumia watu maalum (CIP) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) ambapo hatua iliyofikiwa ni kuendelea na upembuzi yakinifu wa awali;

(i) Mradi wa ujenzi wa Hosteli ya wanafunzi wa Chuo cha Uhasibu Kampasi ya Dar es Salaam na Kampasi ya Mbeya ambapo upembuzi yakinifu wa awali umekamilika;

(j) Mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza simu za mkononi chini ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ambapo upembuzi yakinifu umekamilika; na

(k) Mradi wa ujenzi wa hosteli za Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo ambapo upembuzi yakinifu umekamilika.

### 3.3.5 Kuimarisha Usimamizi na Utekelezaji wa Mpango

#### 3.3.5.1 Ufuatiliaji wa Miradi kwa Mwaka 2019/20

Katika Mwaka 2019/20, Wizara ya Fedha na Mipango imeendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Miradi 75 ilifuatiliwa katika sekta za Uchukuzi, Viwanda, Elimu, Afya, Ujenzi, Utawala Bora, Kilimo, Mifugo, Maji, na Biashara, katika mikoa ya Kigoma, Kagera, Simiyu, Mara, Dar es Salaam, na Shinyanga. Miradi hiyo iligharamiwa kwa fedha za Serikali na miradi mingine ilifadhiliwa na Sekta Binafsi. Orodha ya miradi iliyofuatiliwa imeainishwa katika **Kiambatisho II.**

#### 3.3.5.2 Changamoto za Utekelezaji wa Mpango

(a) Kutofikia malengo katika ukusanyaji wa mapato;

(b) Uharibifu wa miundombinu uliosababishwa na mafuriko;

(c) Kupungua kwa shughuli za kibiashara duniani kutokana na athari za COVID-19; na

(d) Ukwepaji kodi kwa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu hususan

kupitia njia za magendo, uhamishaji wa faida (transfer pricing) kwa kampuni zenye mtandao wa kimataifa na kutokutoa na kutodai stakabadhi za kielektroniki (EFD receipt) wakati mauzo yanapofanyika.

#### 3.3.5.3 Hatua Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto

Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeendelea kuchukua hatua zifuatazo:

(a) Kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato vya ndani na kutekeleza miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato ili kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia bajeti yake;

(b) Kufanya ukarabati wa miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko pamoja na kuimarisha ukaguzi wake;

(c) Kuendelea kufuatilia kwa ukaribu mwenendo wa biashara duniani ili kutumia fursa zitokananzo na athari za COVID-19 kwa manufaa mapana ya nchi pamoja na kuchukua hatua za kisera na kiutawala kurejesha biashara zilizoathirika; na

(d) Kuimarisha mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa mapato ili kudhibiti ukwepaji kodi pamoja na kuendelea kuhamasisha umma juu ya umuhimu wa kulipa kodi pamoja na matumizi ya stakabadhi za kielektroniki.

# SURA YA NNE

# MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2021/22

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inaainisha kwa kifupi maeneo ya kipaumbele yatakayozingatiwa katika maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22. Mapendekezo ya Mpango yatakuwa ni ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Aidha, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 utazingatia ukamilishaji wa miradi ya kipaumbele ambayo utekelezaji wake haukukamilika katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21. Hivyo, maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2021/22 yanaakisi utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26.

## 4.2 Misingi ya Mpango na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi

### 4.2.1 Misingi *(Assumptions)* ya Mpango kwa Mwaka 2021/22

Katika mwaka 2021/22, misingi mikuu itakayozingatiwa katika uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ni kama ifuatavyo:

(a) Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama, umoja, utulivu wa ndani na nchi jirani;
(b) Kuhimili athari za majanga ya asili kama vile mafuriko na magonjwa ya mlipuko;
(c) Ushiriki mpana wa sekta binafsi katika maendeleo ya nchi;
(d) Hali nzuri ya hewa itakayowezesha uzalishaji wa chakula cha ziada; na
(e) Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya kimataifa.

### 4.2.2 Shabaha za Ukuaji wa Uchumi

Shabaha kuu za uchumi katika mwaka 2021/22 na katika kipindi cha muda wa kati ni kama ifuatavyo:

(a) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.0 mwaka 2021 na kuendelea kukua kwa wastani wa asilimia 6.3 ifikapo mwaka 2023;
(b) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 hadi 5.0 katika muda wa kati;
(c) Mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) kufikia asilimia 15.9 ya Pato la Taifa mwaka 2021/22 na wastani wa asilimia 16.3 ya Pato la Taifa

ifikapo mwaka 2023/24;

(d) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.5 ya Pato la Taifa mwaka 2021/22 kutoka matarajio ya asilimia 12.9 mwaka 2020/21;

(e) Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) haizidi asilimia 3.0 ili kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(f) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na

(g) Kuboresha ustawi wa maisha ya watu.

### 4.3 Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka 2021/22

#### 4.3.1 Miradi ya Kielelezo

Miradi hii ni muhimu kwa kuwa utekelezaji wake unatarajiwa kutoa matokeo makubwa na ya haraka katika uchumi hususan katika maeneo ambayo huchochea mageuzi ya viwanda, maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Katika mwaka 2021/22, Serikali inatarajia kutekeleza yafuatayo:

(a) Kuendeleza ujenzi wa Reli ya Kati katika kiwango cha kimataifa *(Standard Gauge);*

(b) Ujenzi wa kituo cha kufua umeme wa maji Julius Nyerere – MW 2,115;

(c) Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL);

(d) Mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania);

(e) Mradi wa Kusindika gesi asilia kuwa kimiminika (LNG) – Lindi;

(f) Mradi wa Magadi Soda Engaruka;

(g) Mradi wa Makaa ya Mawe - Mchuchuma na Chuma – Liganga ikijumuisha ujenzi wa reli kwa kiwango cha standard gauge kutoka Mtwara hadi Mbambabay na matawi yake ya Mchuchuma na Liganga;

(h) Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Ruhudji (MW 358);

(i) Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Rumakali (MW 222);

(j) Ujenzi wa Madaraja Makubwa na Barabara za Juu (Interchange) za Daraja la Kigongo - Busisi (Mwanza), Tanzanite (Dar es Salaam) na Interchange ya Kamata (Dar es Salaam);

(k) Bandari ya Uvuvi (Mbegani) na Ununuzi wa Meli za Uvuvi;

(l) Kiwanda cha Sukari Mkulazi;

(m) Mradi wa Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia katika kitalu cha Mnazi *Bay* Kaskazini;

(n) Mradi wa Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia katika kitalu cha Eyasi

Wembere;

(o) Mradi wa Uchimbaji wa madini ya Nickel;

(p) Mradi wa Magadi Soda – Engaruka;

(q) Kuongeza Rasilimali Watu yenye Ujuzi Adimu na Maalumu (Ujuzi wa Kati na Wabobezi) kwa Maendeleo ya Viwanda na Ustawi wa Jamii; na

(r) Uendelezaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi.

### 4.3.2 Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi

#### 4.3.2.1 Kuimarisha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji

Maeneo yatakayopewa msukumo yatajumuisha utulivu wa uchumi na uendelezaji wa reli, barabara, madaraja, usafiri wa majini, usafiri wa anga, nishati, bandari, viwanja vya ndege pamoja na utekelezaji wa Mpango Kazi wa kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji. Katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 maeneo mbalimbali yatapewa kipaumbele ikijumuisha yafuatayo:

##### 4.3.2.1.1 Uendelezaji wa Miundombinu na Huduma

**A. Reli**

(a) Kukarabati njia za reli zilizopo (Meter gauge);

(b) Kuboresha huduma katika njia za reli ikijumuisha reli ya Tanga – Arusha na reli ya Dar es Salaam – Isaka – Mwanza;

(c) Kufufua njia za reli zilizofungwa kuelekea kwenye maeneo ya viwanda;

(d) Ununuzi na ukarabati wa vitendea kazi (injini, mabehewa na mitambo ya matengenezo);

(e) Kuongeza matumizi ya TEHAMA katika uendeshaji na utoaji wa huduma kwa wateja;

(f) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya utoaji wa mafunzo ya reli na teknolojia ya usafirishaji (Railway College of Transport Technology); na

(g) Kuimarisha miundombinu na huduma katika reli ya TAZARA ili kuongeza ufanisi.

**B. Barabara na Madaraja**

(a) Kujenga na kukarabati barabara zenye kufungua fursa za kiuchumi;

(b) Kujenga na kukarabati barabara zinazounganisha Tanzania na nchi jirani;

(c) Kujenga na kukarabati barabara za mikoa;

(d) Kujenga na kukarabati barabara za kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Arusha na Mwanza;

(e) Kujenga Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka katika jiji la Dar es

Salaam;
(f) Kujenga barabara za juu *(Flyover)* katika jiji la Dar es Salaam;
(g) Kuboresha mtandao wa barabara za vijijini na mijini;
(h) Kujenga na kukarabati madaraja makubwa; na
(i) Kuimarisha na kuboresha utoaji huduma za usafiri kwa njia ya barabara.

**C. Usafiri wa Majini**

**(a) Meli**
(i) Kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya kubeba mizigo katika Bahari ya Hindi;
(ii) Kukamilisha ukarabati mkubwa wa meli katika maziwa;
(iii) Kuendelea na ujenzi wa meli za kubeba abiria na mizigo katika maziwa;
(iv) Kuboresha ulinzi na usalama wa usafiri wa majini na kuzuia uchafuzi wa mazingira;
(v) Kuboresha huduma za uwakala wa meli, udhibiti wa nyaraka, uondoshaji na uhakiki wa shehena mahsusi zenye maslahi mapana kwa Taifa; na
(vi) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya utoaji wa mafunzo ya ujenzi wa meli pamoja na teknolojia ya usafiri wa majini (Ship Building and Maritime Technology).

**(b) Vivuko**
(i) Ununuzi na ukarabati wa vivuko;
(ii) Kujenga na kukarabati maegesho ya vivuko; na
(iii) Kununua vifaa vya usalama na uokozi katika bahari na maziwa makuu.

**D. Bandari**
(a) Kuendeleza miundombinu ya bandari zote ikiwemo mitambo ya kisasa ya kuhudumia shehena na mifumo ya TEHAMA; na
(b) Kuimarisha viwango vya ubora katika utoaji wa huduma na kudhibiti tozo kwa huduma za bandari na usafiri wa njia ya maji.

**E. Usafiri wa Anga**
(a) Kuimarisha miundombinu ya viwanja vya ndege vilivyopo na kujenga viwanja vipya;
*(b)* Kuimarisha huduma katika viwanja vya ndege *(ground handling services);*
(c) Kuimarisha huduma na usalama wa usafiri wa anga;
(d) Kuimarisha Kituo cha Umahiri wa Mafunzo ya usafiri wa Anga na Operesheni katika usafirishaji *(Centre of Excellence in Aviation and Transport Operation)*; na

(e) Ujenzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga cha kisasa.

**F. Nishati**

(a) Kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutekeleza miradi mikubwa ya kuzalisha umeme;
(b) Kujenga na kukarabati miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme mijini na vijijini;
(c) Kuimarisha miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia majumbani na viwandani;
(d) Kuendeleza shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia; na
(e) Kuendelea na mipango ya uwekezaji katika vyanzo vya nishati mbadala, jadidifu – *Off Grid* na makaa ya mawe.

**G. Hali ya Hewa**

(a) Kuimarisha miundombinu ya huduma za utabiri wa hali ya hewa;
(b) Kujenga na kuboresha miundombinu ya kutolea mafunzo ya hali ya hewa nchini; na
(c) Kuboresha na kuongeza wigo wa huduma za hali ya hewa kwa watumiaji wa Bahari na Maziwa.

**4.3.2.1.2 Utulivu wa Uchumi**

Maeneo ya kipaumbele yatajumuisha kuwa na uchumi tulivu na unaotabirika.

**4.3.2.1.3 Utawala Bora**

Maeneo yatakayopewa kipaumbele ni:

(a) Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa Mji wa Serikali – Mtumba (Dodoma) ikijumuisha majengo ya Wizara 23 na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
(b) Kuimarisha utawala wa Sheria na utoaji wa haki;
(c) Kuendelea na maboresho ya sekta ya sheria;
(d) Kuhamasisha amani, usalama na utulivu wa kisiasa;
(e) Kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika utumishi wa umma;
(f) Kupambana na rushwa na utakatishaji wa fedha;
(g) Kuimarisha shughuli za Bunge na Mahakama;
(h) Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa rasilimali watu;
(i) Kuimarisha matumizi ya Serikali Mtandao katika utoaji huduma kwa umma;
(j) Kuendelea kutoa elimu kuhusu haki za binadamu na utawala bora;
(k) Kuendelea na usajili wa matukio muhimu ya binadamu hususan vizazi na vifo;

(l) Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa sheria ya nchi ya umiliki wa utajiri na mali asilia;
(m) Kusimamia mipango ya maendeleo endelevu na usawa katika matumizi ya maliasili za nchi katika ukuaji wa uchumi jamii;
(n) Kuendelea kuimarisha mifumo ya udhibiti wa uingiaji, utokaji na utoaji huduma za uhamiaji kwa wageni na raia nchini;
(o) Kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama magerezani sanjari na kuboresha mifumo na programu za Urekebishaji wa wafungwa na shughuli za uzalishaji;
(p) Kuendelea kusajili na kutambua watu wote waishio nchini wakiwemo raia, wageni wakaazi na wakimbizi;
(q) Kuimarisha huduma za zimamoto na uokoaji;
(r) Kuboresha mifumo ya haki jinai ili kukabiliana na uhalifu nchini na kuvutia uwekezaji kwa kuifanya mifumo hiyo kuwa rafiki;
(s) Kuhuisha na kuimarisha mifumo ya TEHAMA (Haki Mtandao) na kujenga Mfumo wa Kusimamia na kuratibu Masuala ya Utajiri na Rasilimali Asilia za Nchi ili kuleta manufaa kwa wananchi;
(t) Kuendelea kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mfumo wa utoaji haki nchini; na
(u) Kuboresha miundombinu ya utoaji Haki nchini.

**4.3.2.2 Biashara na Masoko**

(a) Kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji;
(b) Kuanzisha vituo vya biashara na huduma katika maeneo muhimu ya uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa nje;
(c) Kuimarisha hatua za kitaifa na kikanda zinazosaidia biashara na kupunguza gharama za kufanya biashara;
(d) Kurahisisha biashara za mipakani na mauzo nje kupitia maboresho ya sheria na kanuni;
(e) Kuhamasisha uelewa wa pamoja na kuzingatia sheria za kimataifa na viwango vya kitaalamu;
(f) Kuimarisha upatikanaji na utoaji wa taarifa za kiintelijensia za biashara na masoko;
(g) Kuimarisha miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo;
(h) Kuwezesha upatikanaji wa mitaji;
(i) Kuimarisha kilimo cha mkataba ili kulinda masoko ya mazao ya wakulima;
(j) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika biashara na masoko;
(k) Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro; na
(l) Kujenga uwezo wa wauzaji bidhaa nje ya nchi kwa kuwapatia elimu ya

uaminifu, uadilifu na ubora wa bidhaa.

**4.3.2.3 Mapinduzi ya TEHAMA**

Maeneo yatakayopewa msukumo yatajumuisha:

(a) Kuongeza uwekezaji katika tafiti na maendeleo;
(b) Kuasili teknolojia mpya nchini na kuzitumia kuinua uchumi wa mwananchi;
(c) Kuimarisha uwezo wa taasisi za Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi;
(d) Kuendeleza miundombinu ya mawasiliano ili kuwafikia watumiaji wa mwisho *(lastmile connectivity)*;
(e) Kujenga mazingira wezeshi ya biashara mtandao kwa kuendeleza miundombinu ya postikodi pamoja na miundombinu ya vituo vya kuhifadhi data *(data centers)*;
(f) Kuendeleza miundombinu ya kuhuisha data za kielektroniki *(ICT Equipment Refurbishment)*;
(g) Uanzishwaji wa maeneo maalumu ya uendelezaji Teknolojia na Uvumbuzi katika Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (SEZs);
(h) Kufikisha mawasiliano ya simu na intaneti kwenye maeneo yasiyokuwa na huduma za mawasiliano nchini;
(i) Ujenzi na uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA ili kuboresha huduma za TEHAMA nchini; na
(j) Ujenzi wa miundombinu ya kuendeleza Wa-TEHAMA.

**4.3.3 Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma**

**4.3.3.1 Uzalishaji Viwandani**

Katika mwaka 2021/22 maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na:

(a) Kuimarisha Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (SEZ) na maeneo maalumu ya uwekezaji kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa zitakazouzwa nje (EPZ);
(b) Kufanya tafiti za kina kwa ajili ya maendeleo ya viwanda;
(c) Kuendeleza viwanda vya usindikaji vinavyozalisha bidhaa za petroli (Petro-gas), kemikali, uzalishaji wa dawa kwa matumizi ya binadamu na vifaa vya ujenzi;
(d) Kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya uanzishwaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa;
(e) Ujenzi wa Kongano la Viwanda vya usindikaji Karanga-Dodoma na Kongano la viwanda vya usindikaji Mpunga-Shinyanga kwa ajili ya Wajasiriamali Wadogo;
(f) Ujenzi wa majengo ya viwanda (*Industrial Sheds)* za Wajasiriamali katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Morogoro;

(g) Ujenzi wa *Soga Integrated Industrial Park*; na
(h) Kuwahamasisha wazalishaji wakubwa wa ndani wenye uwezo wa kufanya uvumbuzi na kuhimili vihatarishi vinavyotokana na mazingira ya ushindani.

**4.3.3.2 Uongezaji Thamani**

**A. Kilimo**

(a) Kuendelea na utekelezaji wa Progamu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II);
(b) Kuboresha mifumo ya kitaasisi na Sheria za Kilimo kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya mazao ya kilimo;
(c) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji, maghala na masoko;
(d) Kuimarisha shughuli za utafiti, uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za mazao na pembejeo;
(e) Kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya ushirika;
(f) Kuhamasisha matumizi ya teknolojia bora katika uzalishaji na uhifadhi wa mazao;
(g) Kuimarisha huduma za upimaji matabaka na ubora wa udongo;
(h) Kuimarisha uwezo wa uzalishaji katika kilimo na viwanda vya usindikaji wa mazao ikijumuisha kilimo cha maua, ufugaji samaki, ufugaji nyuki, uzalishaji wa sukari, mafuta, ngozi na nguo; na
(i) Kuwawezesha wakulima wadogo kupata pembejeo, huduma za ugani na masoko kwa kuwaunganisha na wakulima wakubwa.

**B. Mifugo**

Katika kuimarisha Sekta ya mifugo, msukumo mkubwa utawekwa katika maeneo yafuatayo:

(a) Kuimarisha huduma za ugani katika ngazi za Kata na Vijiji ili kumfikia kila mfugaji kwa wakati;
(b) Kuibua tafiti mbalimbali zenye kujibu changamoto za sekta ya mifugo;
(c) Kuboresha afya ya mifugo kwa kuimarisha tiba, kinga na chanjo;
(d) Uzalishaji wa chanjo za magonjwa ya mifugo kwa magonjwa 13 ya kipaumbele ili kuwawezesha wafugaji kupata chanjo za mifugo kwa uhakika na bei nafuu;
(e) Kusimamia ubora wa mbegu za mifugo na huduma ya usambazaji wa mbegu;
(f) Kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa, kuboresha miundombinu na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na biashara ili kuongeza uzalishaji wa nyama na maziwa;
(g) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji, malisho na vyakula vya mifugo;

na

(h) Kuboresha vyuo vya mafunzo vya Mifugo.

**C. Uvuvi**

Kipaumbele kitawekwa katika maeneo yafuatayo:

(a) Kuimarisha na kufungamanisha Uchumi wa Bluu (Blue Economy) wa Sekta ya Uvuvi katika Uchumi wa Taifa;
(b) Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi na kuimarisha miundombinu ya uvuvi ili kuongeza uwezo wa nchi katika uvuvi wa bahari kuu;
(c) Ununuzi wa meli za uvuvi ili kuwezesha Shirika la TAFICO kuweza kuvua katika Bahari Kuu na Ukanda wa Uchumi wa Bahari;
(d) Kujenga na kuimarisha uwezo wa kitaasisi ikijumuisha ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania - TAFICO;
(e) Kuimarisha usimamizi, udhibiti na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi pamoja na uhifadhi wa mazingira na rasilimali za uvuvi;
(f) Kuhamasisha ufugaji wa samaki katika vizimba na mabwawa katika maeneo yote nchini;
(g) Kuimarisha huduma za Maabara ikiwemo Maabara ya Taifa ya Uvuvi, usimamizi, uthibiti wa ubora, usalama na viwango vya mazao ya uvuvi;
(h) Kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi kwa kujenga viwanda vya kuchakata na kusindika mazao ya uvuvi;
(i) Kuimarisha Utafiti, Huduma za Ugani na Mafunzo ya Uvuvi;
(j) Kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali yatokanayo na Sekta ya Uvuvi;
(k) Kuongeza mauzo ya mazao ya uvuvi katika masoko ya ndani na nje ya nchi; na
(l) Kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI).

**D. Uchimbaji wa Madini, Vito vya Thamani na Gesi Asilia**

Maeneo yafuatayo yatapewa kipaumbele:

(a) Kufanya mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na Mikakati ya usimamizi wa Sekta ya Madini;
(b) Kuhamasisha na kusimamia shughuli za uongezaji thamani madini na uwekezaji wa viwanda vya kuchenjua madini;
(c) Kujenga mazingira wezeshi na kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini;
(d) Kuimarisha Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini na Gesi Asilia;
(e) Kuhakikisha upatikanaji wa mapato stahiki ya Serikali;
(f) Kuongeza wigo na kufungamanisha sekta ya madini na sekta nyingine za uchumi;

(g) Kuimarisha na kuhimiza uanzishwaji wa masoko ya madini;
(h) Kuhawilisha ujuzi na teknolojia kutoka nje;
(i) Kuendeleza shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia; na
(j) Kuimarisha taasisi za usimamizi wa sekta ya madini nchini.

**4.3.3.3 Huduma**

(a) Kuongeza uwekezaji katika ujuzi, usafirishaji, umeme, huduma na miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA);
(b) Kuimarisha mazingira wezeshi ya kidigitali kwa ajili ya kuwezesha matumizi ya TEHAMA;
(c) Kuboresha miundombinu kwenye maeneo ya vivutio vya utalii pamoja na kuimarisha ulinzi kwenye maeneo ya hifadhi;
(d) Kuimarisha uhifadhi na kuhimiza matumizi endelevu ya rasilimali za maliasili na malikale ili kuongeza mchango wa rasilimali hizi katika uchumi;
(e) Kuimarisha utangazaji wa vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuongeza idadi ya watalii na mapato;
(f) Kuelimisha na kuhamasisha jamii kushiriki katika uhifadhi wa maliasili na malikale;
(g) Kuimarisha ulinzi wa maisha ya wananchi na mali zao dhidi ya wanyama wakali na waharibifu;
(h) Kuongeza uwezo wa kitaasisi katika maeneo ya ukarimu na utalii;
(i) Kuimarisha usimamizi wa maliasili na malikale;
(j) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kidigitali katika shughuli za Serikali na taasisi binafsi kwa ajili ya kuongeza ufanisi, na kuboresha utoaji wa huduma;
(k) Kuanza kutekeleza utaratibu wa uwekezaji kwenye maeneo maalum ya Wanyamapori (Special Wildlife Investment Concession Areas – SWICA);
(l) Kuendeleza juhudi za kupambana na ujangili kupitia uimarishwaji wa jeshi la uhifadhi ili kuboresha ulinzi na usalama wa rasilimali za wanyamapori, misitu na nyuki;
(m) Kuongeza kasi ya upandaji miti na shughuli za ufugaji nyuki ili kuhifadhi mazingira na kuongeza kipato kwa wananchi na Serikali;
(n) Kushirikisha wadau katika uwekezaji na uendelezaji wa utalii, uanzishwaji wa mabucha, na mashamba ya wanyamapori ili kujipatia kipato na kuchangia ukuaji wa uchumi nchini;
(o) Kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuhifadhi mazingira ikiwemo madhara yatokanayo na uchomaji moto holela katika maeneo ya hifadhi;
(p) Kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuchakata na kufungasha asali na nta ili kuongeza thamani katika mazao ya nyuki na kipato kwa wananchi na mchango wa sekta ya ufugaji nyuki katika Pato la Taifa;

(q) Kukuza mazao ya utalii ya kimkakati husuasan fukwe, meli na mikutano ili kuongeza idadi ya watalii na mapato;
(r) Kuimarisha mazingira wezeshi ya kuendeleza sekta ya bima nchini;
(s) Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya ustawi wa sekta ya benki nchini;
(t) Kuimarisha uwezo wa taasisi za fedha za kugharamia maendeleo ikijumuisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo – TADB na Benki ya Maendeleo TIB; na
(u) Kuimarisha usimamizi, usajili na udhibiti wa huduma za kibenki nchini.

**4.3.4 Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji**

(a) Kuharakisha uunganishaji (integration) wa mifumo ya kidigitali, usalama wa huduma, na ushindani wa soko;
(b) Kuibua mikakati itakayowezesha kuimarisha nafasi ya Tanzania katika Mnyororo wa Thamani wa Dunia;
(c) Kutafuta fursa za biashara kwa lengo la kuwawezesha wafanyabiashara wa Tanzania kunufaika na masoko ya kikanda na kimataifa;
(d) Kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara ikiwa ni pamoja na kupunguza vikwazo visivyo vya kikodi;
(e) Kuboresha mazingira bunifu ili kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI);
(f) Kutenga ardhi/ maeneo ya uwekezaji na kuweka miundombinu ya msingi ili kuvutia uwekezaji;
(g) Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji; na
(h) Kuimarisha uratibu na uhusiano wa kisekta.

**4.3.5 Kuchochea Maendeleo ya Watu**

**4.3.5.1 Afya, Ustawi na Maendeleo ya Jamii**

Maeneo yafuatayo yatapewa kipaumbele:

(a) Kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma za afya ikijumuisha huduma za mama na mtoto na upatikanaji wa chanjo;
(b) Kuendelea kudhibiti maambukizi na magonjwa kama vile malaria, VVU na UKIMWI pamoja na magonjwa yasiyo ya kuambukiza;
(c) Kuhakikisha upatikanaji wa wataalamu bingwa na bobezi, wahudumu wa afya, dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi;
(d) Kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya na ustawi wa jamii;
(e) Kujumuisha masuala ya jinsia katika sera, mikakati, mipango, miongozo na bajeti za kisekta ikiwemo udhibiti wa vitendo vya ukatili kwa wanawake, watoto na wazee;

(f) Kuimarisha upatikanaji, ujuzi na utendaji kazi wa watalaamu wa huduma za afya;
(g) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za afya;
(h) Kuhakikisha ubora, usalama na ufanisi wa tiba asili na tiba mbadala katika kukabiliana na magonjwa mbalimbali;
(i) Kuimarisha tafiti za magonjwa na tiba ili kuboresha utoaji wa huduma za afya;
(j) Kuhamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF) na mifuko mingine ya huduma za bima ya afya;
(k) Kuimarisha na kusimamia utoaji wa msaada wa kisaikolojia kwa makundi mbalimbali ya kijamii yenye uhitaji hususan wahanga wa majanga mbalimbali, watu wenye ulemavu, wazee, watoto walio katika mazingira hatarishi na waraibu wa pombe na madawa ya kulevya; na
(l) Kuimarisha huduma za ustawi wa jamii kwa wazee, watoto na familia na watu wenye ulemavu.

**4.3.5.2 Elimu**

Kipaumbele kitawekwa katika maeneo yafuatayo:

**A. Elimu ya awali, Msingi na Sekondari**

(a) Kuimarisha utoaji wa elimu maalumu;
(b) Kuboresha mazingira ya wathibiti ubora wa shule na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa bora vya utafiti;
(c) Kuendelea kutekeleza Mpango Kambambe wa Elimumsingi bila ada;
(d) Kuimarisha na kuongeza ufaulu katika masomo ya hisabati, sayansi na kiingereza katika ngazi zote za elimu;
(e) Kuimarisha elimu kuhusu historia ya Tanzania; na
(f) Kuimarisha mafunzo ya elimu ya ualimu.

**B. Vyuo vya Ufundi na Teknolojia**

(a) Kufanya ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia (madarasa, maabara, maktaba, hosteli);
(b) Kuongeza upatikanaji wa vitabu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia;
(c) Kujenga vyuo vya ufundi stadi kwa mikoa isiyokuwa navyo; na
(d) Kupitia mitaala na mfumo wa elimu ya ufundi.

**C. Elimu ya Juu**

(a) Kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wenye sifa;
(b) Kukarabati na kuongeza miundombinu ya kufundishia na kujifunzia;

(c) Kuongeza upatikanaji wa vitabu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia;
(d) Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA; na
(e) Kuimarisha utafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu.

**4.3.5.3 Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Maeneo yatakayopewa kipaumbele ni:

(a) Kutambua na kuweka kumbukumbu za vipande vyote vya ardhi nchini;
(b) Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa ikijumuisha ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway), Bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) - EACOP, Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere na maeneo ya Barabara Kuu;
(c) Kuimarisha usalama wa miliki kwa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi;
(d) Kuboresha usimamizi na upatikanaji wa taarifa za ardhi kwa njia ya kielektroniki;
(e) Kuimarisha miundombinu ya upimaji na ramani;
(f) Kuimarisha mipaka ya Tanzania na nchi jirani;
(g) Kuimarisha vyuo vya Ardhi; na
(h) Kuimarisha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini.

**4.3.5.4 Huduma za Maji Safi na Maji Taka**

Maeneo yafuatayo yatapewa kipaumbele:

(a) Kuboresha upatikanaji wa huduma za maji safi na maji taka mijini na vijijini;
(b) Kusimamia matumizi bora ya rasilimali za maji kwa ajili ya umwagiliaji na matumizi ya viwandani;
(c) Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji;
(d) Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa ubora wa maji; na
(e) Kuboresha huduma za usafi wa mazingira.

**4.3.5.5 Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi**

(a) Kuboresha usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi;
(b) Kufuatilia na kusimamia Hifadhi za Baioanuai;
(c) Udhibiti wa uchafuzi wa mazingira;
(d) Kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira kwa wananchi na watendaji;
(e) Kuanza utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021;
(f) Kusimamia, Kuratibu na Kufuatilia Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira ambayo Tanzania ni Mwanachama;
(g) Kutoa vyeti vya Tathmini ya Athari za Mazingira (TAM) kwa miradi na Tathmini ya Mazingira Kimkakati (SEA) na vibali vya udhibiti wa taka

hatarishi;

(h) Kufanya mapitio ya Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi, Mpango Kazi wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira;

(i) Kuhamasisha na kuelimisha kuhusu matumizi ya nishati mbadala ya kuni na mkaa;

(j) Kuhamasisha na Kufuatilia Utekelezaji wa Kampeni ya Taifa ya Upandaji Miti ambapo kila Halmashauri ya Wilaya inatakiwa kupanda miti 1.5 milion kila mwaka;

(k) Kuandaa na kuhamisha utekelezaji wa Mwongozo wa usimamizi na udhibiti wa taka ngumu kwa kutumia dhana Punguza,Tumia tena na Rejeleza; na

(l) Kuandaa Mwongozo wa Usimamizi na Udhibiti wa Uingizaji wa Vifaa vya Kieletroniki na Umeme vilivyotumika.

**4.3.5.6 Kinga ya Jamii**

Maeneo yatakayopewa kipaumbele yatajumuisha:

(a) Kudhibiti vihatarishi vya kijamii na kiuchumi kwa makundi maalumu;

(b) Kuongeza wigo wa ushiriki katika mifuko ya hifadhi za jamii;

(c) Kuimarisha programu za kusaidia kaya maskini;

(d) Kuwezesha upatikanaji wa bima ya afya kwa wote;

(e) Kuongeza Wigo wa Huduma za Msaada wa Kisaikolojia kwa Familia na Jamii; na

(f) Kuhamasisha jamii kufanya mazoezi ili kuimarisha afya na kujikinga na magonjwa.

**4.3.5.7 Usalama wa Chakula na Lishe**

Maeneo yatakayopewa kipaumbele yatajumuisha yafuatayo:

(a) Kuimarisha miundombinu ya kuhifadhi chakula; na

(b) Kuhamasisha unyonyeshaji, ulaji wa mlo kamili, programu za chakula shuleni, kunawa mikono na usafi.

**4.3.6 Kuendeleza Rasilimali Watu**

Katika mwaka 2021/22 kipaumbele kitawekwa katika kujenga uwezo, ujuzi, maarifa na mitazamo chanya kwa nguvukazi ya Taifa ikijumuisha:

(a) Kujenga vyuo vya ufundi stadi katika mikoa yenye uhaba ili kuongeza wataalamu wa ufundi wa kada ya kati nchini;

(b) Kuboresha elimu na mafunzo katika ngazi zote;

(c) Kuboresha taasisi za kukuza na kuendeleza ujuzi na ajira nchini zikiwemo CARMATEC, TIRDO, SIDO na TEMDO

(d) Kuimarisha sayansi, teknolojia na ubunifu ikiwemo tafiti mpya ili kuchochea

maendeleo;

(e) Kukuza ujuzi wa nguvu kazi na kuimarisha upatikanaji wa takwimu za soko la ajira;

(f) Kukuza ubunifu na kuwezeshaji uhawilishaji wa teknolojia kwa vijana na walemavu;

(g) Kuimarisha mifumo na usimamizi wa ithibati na uthibiti wa ubora wa elimu na mafunzo;

(h) Kuhamasisha ushiriki wa jamii katika fursa za elimu na mafunzo; na

(i) Kuwawezesha vijana kiuchumi kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu, ikiwa ni pamoja na kuendeleza ubunifu na vipaji kwa vijana na watu wenye Ulemavu.

**4.3.7 Maeneo Mengine Yatakayopewa Kipaumbele**

**4.3.7.1 Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

(a) Kuimarisha mikakati na teknolojia za kuitangaza Tanzania ndani na nje ya nchi ili kuenzi utendaji wa Serikali, kuvutia watalii na kuhamasisha uwekezaji;

(b) Kuimarisha Usikivu wa redio za Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) katika maeneo mbalimbali nchini yenye usikivu hafifu au kutokuwa na usikivu;

(c) Kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili kitaifa na kimataifa;

(d) Kuendeleza utamaduni, mila na desturi za Mtanzania pamoja na kumbukumbu za harakati za ukombozi wa Bara la Afrika kwa kuzingatia mchango wa Tanzania katika harakati hizo;

(e) Kuimarisha uzalishaji, ubora, ulinzi na masoko ya kazi za sanaa, kitamaduni na ubunifu; na

(f) Kuweka mazingira bora ya kuendeleza michezo ikiwemo miundombinu na wataalamu wa michezo.

**4.3.7.2 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa**

(a) Kuimarisha diplomasia ya kiuchumi;

(b) Kukarabati na kujenga majengo ya ofisi na makazi ya watumishi katika balozi za Tanzania nje ya nchi;

(c) Kuimarisha ushiriki wa nchi katika jumuiya za Kikanda na Kimataifa ikijumuisha EAC, SADC, Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Madola; na

(d) Kujenga majengo ya vitega uchumi katika viwanja vinavyomilikiwa na Serikali nje ya nchi katika maeneo ya kibiashara.

**4.3.7.3 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

Maeneo yatakayopewa kipaumbele kwa mwaka 2021/22 yatajumuisha kuimarisha ushirikiano wa utekelezaji wa miradi ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika sekta za Mawasiliano, Afya, Uchukuzi, Nishati, Elimu, Viwanda, Biashara na Huduma; na kujenga uwezo wa kitaasisi katika utekelezaji wa miradi ya ubia. Shughuli mahsusi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

(a) Ununuzi wa Mbia wa Miradi ya Ujenzi wa Viwanda vya Dawa Muhimu na Vifaa Tiba itakayotekelezwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) katika Mikoa ya Pwani, Mwanza na Mbeya;

(b) Ununuzi wa mtoa huduma wa kudumu wa mradi wa Uendeshaji wa Huduma ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam Awamu ya Kwanza;

(c) Ununuzi wa Mbia wa miradi ya ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne na Kituo Changamani cha Biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere;

(d) Kukamilisha upembuzi yakinifu na kuingia katika hatua ya ununuzi wa mbia wa mradi wa Kusambaza Gesi Asilia katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara;

(e) Kukamilisha upembuzi yakinifu na kuingia katika hatua ya ununuzi wa mbia wa ujenzi wa reli ya *standard gauge* ya Tanga – Arusha - Musoma pamoja na matawi ya Engaruka na Minjingu;

(f) Kukamilisha upembuzi yakinifu na kuingia katika hatua ya ununuzi wa mbia wa mradi wa ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* ya Mtwara – Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga;

(g) Kukamilisha upembuzi yakinifu na kuingia katika hatua ya ununuzi wa mbia wa Mradi wa Ujenzi wa Hosteli za Chuo cha Elimu ya Biashara katika Kampasi za Dodoma na Dar es Salaam;

(h) Kukamilisha upembuzi yakinifu wa awali na kuingia katika hatua ya maandalizi ya upembuzi yakinifu wa mradi wa ujenzi wa Hosteli ya wanafunzi wa Chuo cha Uhasibu Kampasi ya Dar es Salaam na Kampasi ya Mbeya; na

(i) Uidhinishaji wa upembuzi yakinifu na ununuzi wa mbia wa mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza simu za mkononi chini ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

**4.3.7.4 Uzalendo na Ushiriki wa Jamii katika Maendeleo**

Kuimarisha jitihada za kukuza ari ya jamii, uzalendo na kujenga moyo wa kujitolea na kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kutumia nguvukazi na rasilimali zinazowazunguka.

# SURA YA TANO

# UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2021/22

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea kwa ufupi makadirio ya gharama ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22. Makadirio husika yamezingatia utekelezaji wa Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2021/22 – 2025/26 ikiwemo matumizi ya vyanzo bunifu vya mapato ili kufanikisha ugharamiaji wa Mpango. Katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 Serikali iliweka lengo la kutenga kati ya asilimia 30 hadi 40 ya bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Lengo husika lilifikiwa ambapo katika kipindi cha mwaka 2016/17 hadi 2020/21, Serikali ilitenga wastani wa asilimia 38.0 ya bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Lengo la Serikali ni kuendeleza mwenendo huu. Katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021/22, Serikali itaendelea kutenga na kutoa rasilimali fedha katika miradi yenye matokeo makubwa na ya haraka katika uchumi ili kuimarisha ukuaji wa uchumi na ustawi wa maisha ya watu. Aidha, sekta binafsi inatarajiwa kuendelea kuwa mdau muhimu katika ugharamiaji wa Mpango. Mpango utajikita zaidi katika kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu kwa kuchochea ushindani, kukuza sekta binafsi na kuongeza uuzaji bidhaa nje ili kuimarisha ukuaji wa uchumi na ustawi wa maisha ya watu.

## 5.2 Gharama za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2021/22

Kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Serikali itajielekeza katika utekelezaji wa maeneo makuu matano (5) ya kipaumbele ambayo yanajumuisha: Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi; Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma; Kukuza Biashara na Uwekezaji; Kuchochea Maendeleo ya Watu; na Kuendeleza Rasilimali Watu.

Matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 13,255.9 mwaka 2021/22, sawa na asilimia 37 ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 10,370.9, sawa na asilimia 78 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2,885.0, sawa na asilimia 22 ni fedha za nje. Vyanzo vya ugharamiaji wa Mpango vinatarajiwa kuwa shilingi bilioni 6,180.0 kutokana na mapato ya ndani, shilingi bilioni 4,190.9 mikopo ya kibiashara ya ndani na nje na shilingi bilioni 2,885.0 misaada na mikopo nafuu.

Utekelezaji wa miradi ya kielelezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 unategemewa kutumia sehemu kubwa ya bajeti ya

maendeleo. Miradi husika ni pamoja na: Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115; Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); Ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kimataifa *(Standard Gauge)*; Mradi wa Makaa ya Mawe - Mchuchuma na Chuma – Liganga ikijumuisha ujenzi wa reli kwa kiwango cha standard gauge kutoka Mtwara hadi Mbambabay na matawi yake ya Mchuchuma na Liganga; Bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); Mradi wa Kuchakata Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) – Lindi; Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Ruhudji (MW 358); Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Rumakali (MW 222); Ujenzi wa Madaraja Makubwa na Barabara za Juu (Interchange) za Daraja la Kigongo - Busisi (Mwanza), Tanzanite (Dar es Salaam) na Interchange ya Kamata (Dar es Salaam); Bandari ya Uvuvi (Mbegani) na Ununuzi wa Meli za Uvuvi; Kiwanda cha Sukari Mkulazi; Utafutaji wa mafuta katika vitalu vya Eyasi Wembere na Mnazi *Bay* Kaskazini; Mradi wa Uchimbaji wa madini ya Nickel; Mradi wa Magadi Soda – Engaruka; Kanda Maalumu za Kiuchumi; na Kuongeza Rasilimali Watu yenye Ujuzi Adimu na Maalumu (Ujuzi wa Kati na Wabobezi) kwa Maendeleo ya Viwanda na Ustawi wa Jamii.

Miradi mingine ya maendeleo hususan ya viwanda na uwekezaji mkubwa itaendelea kutekelezwa kupitia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka sekta binafsi, taasisi zisizo za kiserikali, taasisi za dini na kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Aidha, baadhi ya miradi ya maendeleo ya kijamii hususan itakayotekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa itagharamiwa kwa kupitia *corporate social responsibility* pamoja na michango ya nguvu za wananchi.

### 5.3 Vyanzo vya Mapato kwa Mwaka 2021/22

Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umeainisha vyanzo mbalimbali vya ndani, nje na bunifu vya ugharamiaji wa Mpango. Katika mwaka 2021/22, Serikali itaendelea kutekeleza kikamilifu mapendekezo ya vyanzo hivyo. Kwa upande wa mapato ya ndani, Serikali itasimamia ukusanyaji wa mapato ya kodi na mapato yasiyo ya kodi kwa: kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ili kukuza biashara ndogo na za kati kwa ukuaji endelevu wa uchumi; kuboresha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari na upanuzi wa wigo wa kodi; kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato kwa kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA; kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato; na kuoanisha na kupunguza tozo na ada mbalimbali.

Kwa upande wa mchango wa Washirika wa Maendeleo, Serikali itaendelea

kutekeleza kikamilifu mwongozo wa ushirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo (Development Cooperation Framework - DCF) pamoja na Mpango Kazi wake. Aidha, Serikali itaimarisha usimamizi wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zinazopelekwa moja kwa moja katika miradi ya maendeleo kwa kusimamia uwasilishwaji wa taarifa kwa wakati ili kufanikisha uhasibu na ukaguzi wa miradi husika kwa lengo la kupata thamani halisi ya fedha husika.

Vile vile, Serikali itaendelea kukopa kwa kuzingatia Mkakati wa Kusimamia Madeni katika Kipindi cha Muda wa Kati (Medium Term Debt Strategy – MTDS) na kuhakikisha kuwa sekta binafsi inapata fursa ya kukopa katika soko la ndani. Mikopo yenye masharti ya kibiashara itaelekezwa katika miradi yenye matokeo makubwa na ya haraka na uwezo wa kulipa mikopo husika kwa wakati. Aidha, Serikali itaendelea kukuza soko la fedha la ndani pamoja na kuwezesha taasisi za ugharamiaji wa maendeleo ili kutoa fursa za mitaji kwa wawekezaji.

### 5.4 Vyanzo Vingine vya Mapato

Serikali itaendelea na jitihada za kuimarisha mazingira wezeshi kwa kutumia vyanzo bunifu kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Vyanzo hivyo ni pamoja na uwekezaji wa Sekta binafsi kwa utaratibu wa PPP, uwekezaji wa moja kwa moja unaolenga kutekeleza vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ikiwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu wezeshi ya uwekezaji na hatifungani za uendelezaji wa miundombinu.

# SURA YA SITA

# UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA

## 6.1 Utangulizi

Sura hii inalezea nyenzo muhimu za ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa miradi, utoaji taarifa na kuhakikisha uwajibikaji. Ili kufanikisha utekelezaji wake, mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa za utekelezaji wa miradi utaandaliwa. Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ni nyenzo muhimu katika kuboresha usimamizi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya kila mwaka. Mfumo huu unaandaliwa kufuatia mapitio ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa, maoni ya wadau na mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambayo yameainisha changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo. Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano utatoa mwongozo wa ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo kwa kubaini na kutanzua changamoto zinazojitokeza ili kuhakikisha utekelezaji wa miradi unafanyika kwa ufanisi.

Katika mwaka 2021/22, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini umejikita katika kutekeleza nyenzo muhimu za mkakati ambazo ni: kuandaa miongozo ya Ufuatiliaji na Tathmini; kuhimiza uratibu; kuhuisha shughuli za miradi; kujenga uwezo; na upatikanaji wa rasilimali. Aidha, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utaimarisha uwekaji wa malengo mahsusi, viashiria vichache na vinavyopimika na shabaha zinazoweza kufikiwa kwa kuzingatia muda na rasilimali zilizopo.

## 6.2 Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17– 2020/21

Serikali imekamilisha taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 na kuandaa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26.

Katika kuhakikisha kuwa Mpango wa Tatu unatekelezwa kwa ufanisi, Serikali inaandaa mkakati wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mpango huo. Aidha, Mkakati huo utakuwa na malengo na shabaha zitakazowezesha kufikiwa na kuhakikisha taarifa zinazopatikana zinafanyiwa kazi kwa wakati, utolewaji wa fedha ili kuendana na ratiba za ufuatiliaji pamoja na kuwezesha majadiliano yenye lengo la kuboresha utendaji kazi wa miradi katika ngazi mbalimbali.

### 6.3 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22

Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021/22 umejikita katika:

(i) **Uratibu:** kuhimiza uratibu katika nyanja zote za utekelezaji wa miradi.

(ii) **Uoanishaji:** kuoanisha shughuli za miradi zinazofanana ili kuleta tija.

(iii) **Maboresho:** kufanya maboresho ya sera, sheria, kanuni na miongozo ili kuhimiza uwajibikaji na ufanisi katika utendaji kazi wa taasisi.

(iv) **Kujenga Uwezo:** Wataalamu wa masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini kuwa na ujuzi unaoendana na kazi husika.

(v) **Matumizi ya Viashiria:** Viashiria vya kitakwimu na visivyo vya kitakwimu vitatumika katika kupima hatua za utekelezaji ikilinganishwa na malengo ya Mpango.

(vi) **Upatikanaji wa Rasilimali**: Kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi na fedha kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo katika ngazi zote.

### 6.4 Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini

Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini zitawawezesha watoa maamuzi katika ngazi mbalimbali kutoa maamuzi sahihi kwa wakati. Matokeo yatakayotokana na Ufuatiliaji na Tathmini ni pamoja na: taarifa za utekelezaji kwa kila robo mwaka, nusu mwaka na kwa mwaka; na vikao vya mrejesho katika ngazi mbalimbali.

### 6.5 Mgawanyo wa Majukumu

Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Umma, Sekta Binafsi na Wananchi ni wadau muhimu katika ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Mgawanyo wa kazi ya ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa ya utekelezaji wa Mpango ni kama ifuatavyo:-

#### 6.5.1 Wizara ya Fedha na Mipango

Wizara ya Fedha na Mipango imekasimiwa jukumu la kuratibu kazi ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kitaifa ya kimkakati na inayotekelezwa na Sekta Binafsi kwa kushirikiana na Wizara, Idara, Taasisi na Mashirika ya Umma na Wakala za Serikali. Aidha, Wizara itachambua taarifa za ufuatiliaji na tathmini, na kuainisha maeneo ya kuboresha utekelezaji ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Vile vile, Wizara itaandaa na kutoa taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa miradi yote inayotekelezwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi, Wakala za Serikali na Sekta Binafsi.

### 6.5.2 Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali

Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali zitawajibika kuandaa Mpango Kazi wa ufuatiliaji na tathmini, taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kila robo mwaka, nusu na mwaka na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (*National Projects Management Information System - NPMIS*). Vitengo vya ufuatiliaji na tathmini vinawajibika kuwa na Mpango Kazi wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo ili kuendana na matakwa ya Mpango Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Vile vile, Wizara, Idara na Wakala za Serikali zinasisitizwa kuviwezesha na kuvijengea uwezo Vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini ili kutekeleza majukumu ya ufuatiliaji na tathmini kwa ufanisi. Aidha, Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma umeainisha masuala muhimu ya kuzingatia wakati wa ufuatiliaji na tathmini, ambayo ni upimaji wa malengo na matumizi ya rasilimali fedha, kuainisha changamoto, vihatarishi na ushirikishwaji wa wadau.

### 6.5.3 Ofisi ya Rais – TAMISEMI

Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaratibu na kutoa taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinawajibika kuandaa Mpango Kazi wa ufuatiliaji na tathmini, ikiwa ni pamoja na kuandaa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo mwaka, nusu mwaka na mwaka na kuwasilisha Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Ofisi ya Rais - TAMISEMI itachambua na kuandaa taarifa jumuishi na kuiwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa hatua stahiki. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI itatumia fursa ya kuandaa taarifa jumuishi kutoa maoni, mapendekezo na ushauri kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya miradi katika ngazi mbalimbali utafanyika kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (*National Projects Management Information System - NPMIS*).

### 6.5.4 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora itaendelea kuhakikisha kuwa vitengo vya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti vinapatiwa rasilimali watu yenye weledi, uadilifu, juhudi na maarifa katika kutekeleza majukumu ya ufuatiliaji na tathmini kwa ufanisi.

### 6.5.5 Sekta Binafsi

Sekta Binafsi kupitia uratibu wa Taasisi ya Sekta Binafsi Nchini (TPSF) na TCCIA zitawasilisha taarifa muhimu zitakazohitajika katika kufanya mapitio ya mifumo ya kisera, kisheria na kitaasisi ili kuboresha mazingira ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Taarifa hizo zitaainisha mwenendo wa uwekezaji wa Sekta Binafsi ikilinganishwa na malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; mafanikio, fursa, changamoto na dosari zilizopo katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22. Vile vile, Sekta Binafsi itawajibika kutoa maoni na mapendekezo ya hatua za haraka za kuchukua ili kukabiliana na changamoto na dosari zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo.

**Kiambatisho I: Ratiba ya Maandalizi ya Mpango 2021/22**

| Shughuli | 2020 | | | | | | 2021 | | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jul | Ago | Sep | Okt | Nov | Des | Jan. | Feb. | Mac | Apr | Mei | Jun | |
| Maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 | | | V | V | | | | | | | | | Wizara ya Fedha na Mipango |
| Kupata maoni ya wadau kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 | | | | | V | | | | | | | | Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika/Taasisi, Wakala za Serikali na Sekta Binafsi |
| Kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 katika hatua za maamuzi Serikalini | | | | | | V | V | | | | | | Waziri wa Fedha na Mipango |
| Kuwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 | | | | | | | V | V | | | | | Waziri wa Fedha na Mipango |
| Kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 | | | | | | | V | V | V | | | | Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika/Taasisi, |

| **Shughuli** | **2020** | | | | | | **2021** | | | | | | **Mhusika** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Jul** | **Ago** | **Sep** | **Okt** | **Nov** | **Des** | **Jan.** | **Feb.** | **Mac** | **Apr** | **Mei** | **Jun** | |
| | | | | | | | | | | | | | Wakala za Serikali na Sekta Binafsi |
| Kupata maoni ya wadau kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 | | | | | | | V | | V | | | | Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika/ Taasisi, Wakala za Serikali na Sekta Binafsi |
| Kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 katika Bunge Zima likikaa kama Kamati ya Mipango | | | | | | | | | V | | | | Wizara ya Fedha na Mipango |
| Kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 na Hali ya Uchumi 2020 katika Kamati ya Bajeti ya Bunge | | | | | | | | | V | | | | Waziri wa Fedha na Mipango |
| Kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 na Hali ya Uchumi 2020 katika Bunge | | | | | | | | | | | | V | Waziri wa Fedha na Mipango |

| **Shughuli** | **2020** | | | | | | **2021** | | | | | | **Mhusika** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Jul** | **Ago** | **Sep** | **Okt** | **Nov** | **Des** | **Jan.** | **Feb.** | **Mac** | **Apr** | **Mei** | **Jun** | |
| Ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2020/21 | | | V | | | V | | | V | | | V | Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara za kisekta |

**Kiambatisho II: Mradi Iliyofuatiliwa katika Mwaka 2019/20**

| Na. | Jina la Mradi | Mkoa | Sekta |
|---|---|---|---|
| 1. | Uzalishaji wa Mbegu Bora wa zao la Mchikichi - Kihinga | Kigoma | Kilimo |
| 2. | Kiwanda cha Kusindika Asali, Samaki, Mazao ya Kilimo (Mbogamboga) na Vyakula vya Mifugo (Third Man Limited) | Kigoma | Viwanda |
| 3. | Ujenzi wa Jengo la Mahakama Kuu na Nyumba za Majaji | Kigoma | Utawala Bora |
| 4. | Ujenzi wa Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 413): Sehemu za Nyakanazi – Kibondo (km 50) | Kigoma | Ujenzi |
| 5. | Mradi wa Ujenzi wa Bandari Kavu Katosho - Kigoma | Kigoma | Uchukuzi |
| 6. | Mradi wa Usanifu na Ujenzi wa Gati la Kibirizi, Ujiji na Ofisi ya Meneja wa Bandari | Kigoma | Uchukuzi |
| 7. | Uendelezaji wa Viwanda Vidogo - SIDO Kigoma | Kigoma | Viwanda |
| 8. | Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo – EP4R) – Ujenzi wa Shule ya Mfano Bwega – Buhigwe | Kigoma | Elimu |
| 9. | Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) - Nyamidaho | Kigoma | Elimu |
| 10. | Kiwanda cha Maji Malagarasi | Kigoma | Viwanda |
| 11. | Mradi wa Ujenzi wa Soko la Kimataifa la Kagunga | Kigoma | Ujenzi/Biashara |
| 12. | Mradi wa Kiwanda cha Kubangua Kahawa - Kanyovu | Kigoma | Viwanda |
| 13. | Ujenzi wa Gati la Sibwesa | Kigoma | Uchukuzi |
| 14. | Hospitali ya Wilaya ya Buhigwe | Kigoma | Afya |
| 15. | Ujenzi wa soko la kisasa - Munanila | Kigoma | Biashara |
| 16. | Ujenzi wa kituo cha afya Munzeze | Kigoma | Afya |
| 17. | Ujenzi wa barabara km 2 - Buhigwe | Kigoma | Ujenzi |
| 18. | Ujenzi wa barabara za lami katika Manispaa ya Bukoba – Kagera | Kagera | Ujenzi |
| 19. | Ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya Uendelezaji wa Viwanda Vidogo (SIDO - Kagera) | Kagera | Viwanda |
| 20. | Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Kagera | Kagera | Elimu |
| 21. | Ujenzi wa Shule ya Sekondari Ihungo – Bukoba Manispaa | Kagera | Elimu |
| 22. | Ujenzi wa Shule ya Sekondari Nyakato - Bukoba Vijijini | Kagera | Elimu |
| 23. | Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya | Kagera | Elimu |

| Na. | Jina la Mradi | Mkoa | Sekta |
|---|---|---|---|
| | Majengo ya Chuo cha Ufundi Stadi cha Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe – KDVTC | | |
| 24. | Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Kitengule (Mita 140) na Barabara za Maingilio (km 18) | Kagera | Ujenzi |
| 25. | Kiwanda cha Vinywaji Vikali Ambiance Distillers (T). Ltd | Kagera | Viwanda |
| 26. | Ujenzi wa Barabara ya Ushirombo – Lusahunga (Km 110) | Kagera | Ujenzi |
| 27. | Ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi Nyakanazi | Kagera | Ujenzi |
| 28. | Kiwanda cha Kuzalisha Maji, Juisi na Mvinyo cha Mayawa | Kagera | Viwanda |
| 29. | Upanuzi na Uboreshaji wa Kiwanda cha Sukari Kagera | Kagera | Viwanda |
| 30. | Mradi wa Ujenzi wa Majengo ya Viwanda - SIDO | Dodoma | Viwanda |
| 31. | Ujenzi wa Hospitali ya Uhuru Chamwino | Dodoma | Afya |
| 32. | Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) – Bahi | Dodoma | Elimu |
| 33. | Mradi wa Ukarabati wa Barabara ya Galigali – Luanda, Mpwapwa | Dodoma | Ujenzi |
| 34. | Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kongwa | Dodoma | Afya |
| 35. | Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Mbande | Dodoma | Afya |
| 36. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya – Busega | Simiyu | Afya |
| 37. | Ujenzi wa Wodi ya Wazazi – Zahanati ya Gininiga, Wilaya ya Busega | Simiyu | Afya |
| 38. | Ujenzi wa Ofisi ya SIDO Mkoa wa Simiyu | Simiyu | Viwanda |
| 39. | Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi - Malampaka | Simiyu | Elimu |
| 40. | Ujenzi wa Stendi ya Mabasi – Simiyu na Barabara yenye urefu wa km 1.5 | Simiyu | Ujenzi |
| 41. | Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Busega | Simiyu | Utawala Bora |
| 42. | Mradi wa Ununuzi wa Mtambo wa Kutengeneza Chaki na Vifungashio | Simiyu | Viwanda |
| 43. | Ujenzi wa Jengo la Mkuu wa Mkoa wa Simiyu | Simiyu | Utawala Bora |
| 44. | Ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Maswa | Simiyu | Elimu |
| 45. | Barabara za Mjini na Vijijini | Simiyu | Ujenzi |
| 46. | Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) – Sapiwi, Simiyu | Simiyu | Elimu |
| 47. | Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto katika | Simiyu | Afya |

| Na. | Jina la Mradi | Mkoa | Sekta |
|---|---|---|---|
| | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu | | |
| 48. | Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bariadi | Simiyu | Elimu |
| 49. | Ujenzi wa Chuo cha Ufundi VETA – Kanadi | Simiyu | Elimu |
| 50. | Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Maswa – Bariadi (km 49.7) kwa Kiwango Cha Lami | Simiyu | Ujenzi |
| 51. | Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa - Ubungo | Dar es Salaam | Utawala Bora |
| 52. | Ujenzi wa Soko la Mburahati | Dar es Salaam | Ujenzi/Biashara |
| 53. | Ujenzi wa Stendi Kuu ya Mabasi – Mbezi Louis | Dar es Salaam | Ujenzi/Biashara |
| 54. | Ujenzi wa Soko la Kisasa - Kisutu | Dar es Salaam | Ujenzi/Biashara |
| 55. | Ujenzi wa Machinjio ya Kisasa - Vingunguti | Dar es Salaam | Mifugo |
| 56. | Ujenzi wa Soko la Kisasa - Tandale | Dar es Salaam | Ujenzi/Biashara |
| 57. | Ujenzi wa Soko la kisasa - Magomeni | Dar es Salaam | Ujenzi/Biashara |
| 58. | Ujenzi wa Soko la kisasa - Kibada | Dar es Salaam | Ujenzi/Biashara |
| 59. | Ujenzi wa soko la Kimkakati Busoka | Shinyanga | Ujenzi/Biashara |
| 60. | Kituo cha Afya Kambarage | Shinyanga | Afya |
| 61. | Ujenzi wa Machinjio ya Kisasa Ndembezi | Shinyanga | Mifugo |
| 62. | Ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji Kahanga | Shinyanga | Kilimo |
| 63. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Bunda | Mara | Afya |
| 64. | Mradi wa Maji Nyantira – Nyansincha | Mara | Maji |
| 65. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Musoma | Mara | Afya |
| 66. | Ujenzi wa soko la Kimkakati Sirari | Mara | Ujenzi/Biashara |
| 67. | Ujenzi wa stendi mpya | Singida | Ujenzi |
| 68. | Mradi wa stendi ya daladala | Singida | Ujenzi na Uchukuzi |
| 69. | Ujenzi wa barabara ya Nyahua – Chaya | Tabora | Ujenzi |
| 70. | Ujenzi wa kituo cha afya Nyahua | Tabora | Afya |
| 71. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Sikonge | Tabora | Afya |
| 72. | Mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda miji ya Tabora, Igunga, Nzega na Miji midogo | Tabora | Maji |
| 73. | Ujenzi wa jengo la utawala katika Halmashauri ya Uvinza | Kigoma | Utawala bora |
| 74. | Kiwanda cha kuchakata nyama cha chobo | Mwanza | Viwanda |
| 75. | Kiwanda cha kuchakata samaki – Nile Perch | Mwanza | Viwanda |